Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# UTAFITI WA KILIMO WA MWAKA 2022/23

## 2022/2023

# MWONGOZO WA MDADISI

**NENO KWA MDADISI**

Mwongozo huu ni Mwongozo wako;
Soma na uelewe maudhui yake yaliyomo katika kupanga kazi yako;
Soma wakati na katikati ya vipindi vya mahojiano;
Soma ukiwa nyumbani.

Mwongozo huu umeandaliwa kwa matumizi yako kama mdadisi wakati wa kukusanya taarifa za Utafiti wa Kilimo wa Mwaka. Mwongozo huu unaelezea dhana za msingi ambazo unapaswa kuzijua juu ya utafiti huu, mbinu za ukusanyaji wa taarifa, na miongozo ya jinsi ya kupata taarifa sahihi, kamili, za kuaminika, na thabiti kutoka kwa wahojiwa.

Mwongozo huu hauwezi kuelezea kwa undani changamoto zote utakazokutana nazo uwandani. Hata hivyo, inatarajiwa kuwa maelekezo utakayopewa na msimamizi wako pamoja na uelewa wa majukumu na wajibu wako kama yalivyojumuishwa katika mwongozo huu vitakusaidia kufanya kazi yako uwandani kwa makini na ufanisi mkubwa.

Umuhimu wa nafasi yako katika zoezi hili unapaswa kusaidia kukutia moyo kufanya kadri uwezavyo katika kutekeleza majukumu na wajibu wako kama Mdadisi.

***Ifanye kazi yako iwe sifa kwako na kwa nchi yako.***

Dkt. Albina A. Chuwa;
Mtakwimu Mkuu wa Serikali;
Ofisi ya Taifa ya Takwimu;
Oktoba, 2023

## Yaliyomo

*VIFUPISHO VYA MANENO* ........................................................................ *65*

*1 UTANGULIZI* ........................................................................ *76*

1.1 Usuli na Malengo ya Utafiti ........................................................................ 76

1.2 Mpangilio wa Utafiti na Washirika katika Utekelezaji ........................................ 87

1.3 Sampuli na Eneo la Utafiti ........................................................................ 109

1.4 Mwaka wa Kilimo ........................................................................ 109

1.5 Sehemu za Utafiti huu ........................................................................ 10

1.6 Vitendea Kazi vya Utafiti ........................................................................ 11

1.7 Usiri wa Taarifa ........................................................................ 11

*2 TARATIBU ZA UTENDAJI UWANDANI* ........................................................ *12*

2.1 Jukumu lako kama Mdadisi ........................................................................ 12

2.2 Uhusiano kati ya wadadisi na msimamizi ................................................ 12

2.3 Jinsi ya kufanya mahojiano ........................................................................ 13

2.4 Jinsi ya kuuliza maswali ........................................................................ 15

2.5 Kurudi kwenye kaya na kukataa mahojiano ................................................ 1516

2.5.1 Ulazima wa kurudi kwenye kaya ........................................................ 1516

2.5.2 Kukataa mahojiano ........................................................................ 16

2.6 Nyenzo na vifaa vya utafiti ........................................................................ 16

**Orodha inayotolewa hapa ni kwa lengo la kupata hesabu ya vifaa vyote vinavyohitajika na kutolewa kwa utafiti. Ikiwa huna zana na vifaa vyote hivyo, tafadhali wasiliana na ofisi kuu/msimamizi kabla ya kuendelea na ukusanyaji wa taarifa. Vifaa vyote vilivyotolewa vinakusudiwa kumsaidia mdadisi kukusanya taarifa kwa ufanisi. Tafadhali vitunze vifaa vyote kwa uangalifu, na utoe taarifa kwa msimamizi wako kwa kifaa chochote ambacho hakipo au hakifanyi kazi vizuri.**

*3 JINSI YA KUKAMILISHA DODOSO* ........................................................ *18*

**3.1 Kutambua eneo na kaya/mhojiwa ....................................................................18**

**3.2 Kanuni za jumla za kujaza dodoso....................................................................18**

**3.3 Jinsi ya kujaza sehemu mahususi za dodoso.........................................................19**

3.3.1 Jalada la mahojiano…………………………………………………………19

3.3.2 Sehemu ya 0: Mchujo na Jalada la mahojiano.................................................................... 19

3.3.3 Sehemu ya 1: Kuanza mahojiano........................................................................................ 1920

3.3.4 Sehemu ya 2: Utambuzi wa wanakaya na mmiliki...............**Error! Bookmark not defined.**20

3.3.5 Sehemu ya 3. Orodha ya Mashamba..................................**Error! Bookmark not defined.**23

3.3.6 Sehemu ya 4: Mashamba msimu wa VULI...................................................................... 2632

3.3.7 Sehemu ya 5: Orodha ya mazao ya msimu wa VULI.............**Error! Bookmark not defined.**35

3.3.8 Sehemu ya 6: Uzalishaji wa Mazao ya MSIMU wa VULI .......**Error! Bookmark not defined.**40

3.3.9 Sehemu 7: Matumizi ya Mazao –MSIMU wa VULI ...............**Error! Bookmark not defined.**46

3.3.10 Sehemu ya 8: Nguvukazi katika kilimo MSIMU wa VULI (ndani ya kaya)**Error! Bookmark not defined.**50

3.3.11 Nguvukazi kutoka nje ya kaya ambayo ilitumika katika msimu wa Vuli**Error! Bookmark not defined.**51

3.3.12 Sehemu 10. Upatikanaji wa mbegu na miche katika msimu wa Vuli**Error! Bookmark not defined.**53

3.3.13 Sehemu ya 11: Upatikanaji na matumizi ya pembejeo za kilimo (Mbolea na Viuatililfu) msimu wa vuli ....................................................................................**Error! Bookmark not defined.**55

3.3.13 Sehemu 12: Orodha ya vishamba vya masika na maelezo**Error! Bookmark not defined.**57

3.3.14 Sehemu ya 13: Orodha ya mazao ya Masika ..................**Error! Bookmark not defined.**59

3.3.15 ........................................................................................**Error! Bookmark not defined.**64

Sehemu 14. Upatikananji wa mbegu na miche msimu wa masika .....**Error! Bookmark not defined.**64

3.3.16 Sehemu ya 15 Usajili wa Shamba..................................**Error! Bookmark not defined.**66

3.3.17 Sehemu ya 16: mawasiliano na Taarifa za kaya ...............**Error! Bookmark not defined.**66

3.3.18 Sehemu ya 17": Upimaji wa Maeneo.............................**Error! Bookmark not defined.**68

Maelezo :..........................................................................**Error! Bookmark not defined.**68

3.3.19 Mwisho wa Mahojiano ................................................................................... 6772

3.3.20 Baada ya Mahojiano ......................................................................................... 6872

***4 Mwongozo wa kutumia CAPI/SUSO na Kifaa cha GPS na Mfumo wa CAPI kwenye Kishikwambi ............................................................................................ 6973***

**4.1 Matumizi ya Mfumo wa CAPI katika Utafiti wa Kilimo wa mwaka 2023 (AASS 2023).** 69~~73~~

**4.2 Utunzaji wa Jumla wa Kishikwambi na vifaa vingine** ........................................ 69~~73~~

**4.3 Kuanza: Washa Kishikwambi na ingia kwenye Programu ya Usaili wa Mdadisi** ... 70~~74~~

**4.4 Mtiririko wa Vitendo kwa Wadadisi** ........................................ 72~~77~~

**4.5 Kuboresha Mfumo** ........................................ 73~~78~~

**4.6 Muhtasari wa Dashboard ya Mdadisi** ........................................ 74~~79~~

**4.7 Uoanishaji (Synchronization)** ........................................ 82~~88~~

**4.8 Udhibiti wa ubora na kuweka alama za ukamilifu wa mahojiano** ........................ 84~~90~~

**4.9 Kupitia sehemu mbalimbali za dodoso** ........................................ 86~~93~~

**4.10 Maoni** ........................................ 88~~95~~

**4.11 Kujibu aina zote za maswali** ........................................ 89~~97~~

**4.12 Ushabihianaji/mwingiliano(interface) na majibu ya maswali** .......................... 96~~105~~

**4.13 Nini cha kufanyika iwapo utapokea mahojiano yaliyokataliwa** ........................ 99~~108~~

**4.14 Upimani wa maeneo kwa kutumia kifaa cha GPS** .... Error! Bookmark not defined.~~109~~

**4.15 Kunasa Eneo kwa kutumia kifaa cha GPS ya kushika mkononi** Error! Bookmark not defined.~~111~~

**4.16 Kupima ukubwa wa eneo kwa kutumia kifaa cha GPS** Error! Bookmark not defined.~~112~~

**4.17 Miiko ya Kuttumia Kishikwambi wakati wa ukusanyaji wa takwimu** .............. 100~~112~~

***5 VIAMBATISHO*** ........................................ *Error! Bookmark not defined.~~113~~*

# VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| AASS | Annual Agriculture Sample Survey |
| ASDP | Agricultural Sector Development Programme |
| CAADP | Comprehensive Africa Agriculture Development Programme |
| CAPI | Computer Assisted Personal Interview |
| DADPs | District Agriculture Development Plans |
| DS | District Supervisors |
| EAs | Enumeration Areas |
| FAO | Food and Agriculture Organisation |
| FYDP | Five Year Development Plan |
| GPS | Global Positioning System |
| HQ | Headquarters |
| MoA | Ministry of Agriculture |
| MKUKUTA | Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| NAADS | National Agricultural Advisory Service |
| NBS | National Bureau of Statistics |
| NSCA | National Sample Census of Agriculture |
| RDS | Rural development strategy |
| RSM | Regional Statistics Manager |
| PAPI | Paper and Pen Interview |
| PPMP | Poverty Monitoring Master Plan |
| SDGs | Sustainable Development Goals |
| SuSo | Survey solutions |
| WCA | World Programme for the Census of Agriculture |

# 1 UTANGULIZI

## 1.1 Usuli na Malengo ya Utafiti

Tangu mwaka 2001, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanya jitihada mbalimbali ikilenga kupunguza umaskini angalau kwa nusu na kufikia maendeleo ya kijamii na kiuchumi ifikapo mwaka 2015 chini ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). MKUKUTA ulikuwa hatua ya pili muhimu ya kitaifa iliyounganisha juhudi mbalimbali za kuliweka suala la upunguzaji umasikini kuwa kipaumbele kikuu katika ajenda ya maendeleo ya Taifa. Kupitia MKUKUTA, upatikanaji wa taarifa kwa wakati na za uhakika kuhusu umaskini unakuwa nyenzo ya kimkakati ya kuwezesha tathmini ya miradi iliyo chini ya MKUKUTA ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa katika kufanikisha malengo ya Mkakati yaliyoainishwa.

Sekta ya kilimo ni miongoni mwa sekta tano muhimu katika uchumi ambayo huchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza umaskini na riziki za wakulima kwa kuongeza kipato na kujitosheleza kwa chakula. Sambamba na MKUKUTA, Wizara za Sekta ya Kilimo (Wizara ya Kilimo; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Mifugo, Zanzibar) iliandaa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP na ASDP II) na mkakati wake wa utekelezaji kupitia Programu za Wilaya za Maendeleo ya Kilimo (DADPs). Mkakati huu umeainisha mipango ya kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuboresha vipato vya wakulima, usalama wa chakula kwenye kaya na kupunguza umasikini kwa ujumla. Uundaji wa ASDP na DADPs umezingatia malengo yaliyoainishwa katika Sera ya Maendeleo Vijijini (RDS) ya mwaka 2003 na mikakati yake, pia kuchangia maendeleo ya viwanda (katika ASDP II). ASDP II ilikusudia kuharakisha utekelezaji wa viwanda kupitia kuongeza tija katika mazao ya kilimo ambayo hutumika kama malighafi katika usindikaji wa mazao ya kilimo.

Mipango hii inafuatiliwa na kutathminiwa ili kupima ufanisi wake katika kupunguza umaskini. Ili kuwezesha ufuatiliaji na tathmini ya mchango wa ASDP na Mkakati wa Maendeleo Vijijini (Rural Development Strategy-RDS) katika kupunguza umaskini, Serikali ilifanya Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (National Sample Census of Agriculture-NSCA) kwa mwaka 2002/03, 2007/08 na 2019/20. Sensa hizi zilikuwa sehemu ya programu ya muda mrefu ya utafiti, ambayo ni sehemu ya Programu Kabambe ya Kufuatilia Umasikini (the Poverty Monitoring Master Plan (PMMP). Matokeo ya sensa hizo yalitoa taarifa kuhusu hali ya kitaifa ya uzalishaji, utoaji wa huduma na matumizi ya rasilimali ili kuongoza utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali.

Katika kuendeleza juhudi za serikali za kufuatilia maendeleo katika sekta ya kilimo, NBS kwa kushirikiana na Mpango wa nchi 50 zenye uchumi wa chini 2030 (*the 50 by 2030*

*Initiative)* inatekeleza Utafiti wa Kilimo wa Mwaka Tanzania kwa mwaka 2023 (the Tanzania Annual Agriculture Sample Survey of 2023 –AASS 2023).

Utafiti wa Kilimo wa Mwaka (AASS 2023) unalenga kutoa takwimu za kufuatilia maendeleo katika sekta ya kilimo Tanzania, pamoja na kutoa taarifa zinazoaminika kuwezesha kukokotoa na kupanga baadhi ya viashiria muhimu vya ngazi ya kimataifa (vikiwemo SDGs 2.3.1 na 2.3.2), kikanda (vikiwemo vile vya makundi ya utendaji wa CAADP 2.4, 3.1i, 3.1ii, 3.1iv, 3.1vi, 3.2i, 3.2ii, 4.1i na 3.2iii) na ngazi ya kitaifa. Sekta ya kilimo nchini ina mchango mkubwa kwenye sekta ya viwanda na chanzo cha maisha kwa takribani asilimia 65 ya wananchi, na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu 2021/22-2025/26 (FYDP III 2021/22-2025/26) umeainisha viashiria vya kiutendaji na malengo yanayopaswa kufikiwa ifikapo mwaka 2026. Viashiria hivi vingi hupimwa kupitia tafiti za kilimo.

## 1.2 Mpangilio wa Utafiti na Washirika katika Utekelezaji

AASS 2023 itatekelezwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa ushirikiano na Wizara ya Kilimo (MoA) na kwa msaada wa kitaalam kutoka Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO). Ukusanyaji wa taarifa utafanywa na jumla ya timu XX za uwandani. Kila timu imeundwa na wadadisi wanne (4) na msimamizi wa timu mmoja (1) (angalia majukumu na msimamizi katika Sura ya II, sehemu ya 1 hapa chini), ikimaanisha kwamba utafiti utahusisha jumla ya wadadisi XX na wasimamizi XX wa timu.

Aidha, wasimamizi wa udhibiti wa ubora wa XX (QC) watasimamia taratibu za udhibiti wa ubora na watakuwa huru katika kazi zao na watazungukia timu moja hadi nyingine kufanya ukaguzi wa kushtukiza, kurudia mahojiano kwa maswali machache ya muhimu, uangalizi, nk. Hatimaye, jumla ya watumishi wa makao makuu XX, waioko Dodoma, watawajibika kwa ngazi ya tatu ya ukaguzi wa taarifa (baada ya wadadisi na wasimamizi wa taarifa). Muhtasari wa idadi ya watumishi unaoneshwa katika Jedwali 1.

*Jedwali 1: Nguvu kazi ya uwandani ya AASS 2023*

| Watendaji | Idadi |
|---|---|
| Wadadisi | |
| Wasimamizi wa Timu | |
| Wasimamizi wa Udhibiti Ubora | |
| Wakaguzi wa taarifa Makao Makuu | |
| Jumla | |

Kila timu itakwenda kwenye maeneo yao ya kuhesabia (Enumeration Area- EAs) kwa gari. Kabla ya kuanza kwa shughuli yoyote ya ukusanyaji wa taarifa katika EA, msimamizi wa timu atawajulisha Serikali za mitaa/vijiji kuhusu shughuli zijazo za ukusanyaji taarifa katika kijiji/mtaa chao/wao. Pia msimamizi kwa kushirikiana na viongozi wa mtaa/kijiji ataratibu ili kuwezesha upatikanaji wa kaya katika EA na kuhakikisha kuwa wengi wao kadri iwezekanavyo wanapatikana siku watakapotembelewa. Kwa kila EA, ukusanyaji wa taarifa utafanyika kama ifuatavyo:

1. Wadadisi watahoji kaya walizopokea kutoka kwa wasimamizi wa timu zao kuchekecha (screen) kaya zote kwenye EA zao. Katika hatua hiyo, wataweza tu kukamilisha Sehemu ya 0 - Mchujo. Wadadisi watahitaji kuoanisha (synchronize) vishikwambi vyao kila baada ya muda ili waweze kutuma taarifa za uchekechaji wa kaya kikamilifu kwa wasimamizi wao. Awamu hii inaweza kuchukua siku 1 hadi siku moja na nusu kwa kila EA;

2. Msimamizi wa timu atapitia majibu ya kaya zote kama zilivyopokelewa kutoka kwa wadadisi na kuziidhinisha/kuzikataa kutegemeana na ufasaha wa ujazaji wake. Msimamizi wa timu atakapokuwa ameridhika na ubora wa taarifa ya sehemu ya mchujo wa kaya, ataangalia ustahiki wa kila kaya zitakazochaguliwa kwa ajili ya utafiti (na usahihi wa shughuli ya upimaji wa eneo). **Kaya za kilimo zinazostahiki ni kaya zilizoripoti kilimo cha mazao au shughuli za kufuga mifugo katika kipindi cha mwaka wa kilimo (1 Oktoba 2022-30 Septemba 2023), na ambazo hulima angalau mita za mraba 25 (25m$^2$), (lakini chini ya hekta 20), au walifuga angalau ng’ombe 1 (lakini chini ya 50), au mbuzi, kondoo, au nguruwe 5 (lakini chini ya 100), au kuku au bata 50 (lakini chini ya 1,000).** Baada ya hapo Msimamizi wa timu atachagua bila mpangilio kaya 12 katika kaya za kilimo kwa kila EA, katika kaya hizo 12, kaya 5 tu zitachaguliwa kwa kipimo cha eneo/mashamba (Mashamba ya kaya hizo tano yatastahiki kupimwa: Kama tu yatakuwa yamepandwa mazao wakati wa msimu wa Masika pindi kaya zitakapotembelewa). Awamu hii inaweza kuchukua hadi siku 0.5 kwa EA;

3. Msimamizi wa timu atatuma kaya 12 zilizochaguliwa kwenda kwa Wadadisi, ili waweze kuanza mahojiano ya utafiti. Awamu hii ya mwisho ya mahojiano inaweza kuchukua hadi siku 1.5 kwa EA.

### 1.3 Sampuli na Eneo la Utafiti

### 1.4

### 1.5 Mwaka wa Kilimo

Mwaka wa Kilimo wa Tanzania unaanza tarehe 1 Oktoba mpaka 30 Septemba ya mwaka unaofuata. Utafiti utajikita katika mwaka wa kilimo wa 2022/23 (tarehe 1 Oktoba 2022 - 30 Septemba 2023), ikihusisha misimu yote miwili ya Vuli (msimu mfupi wa mvua) na Masika (msimu mrefu wa mvua). Idadi ya mifugo itakuwa kama ilivyokuwa tarehe **1 Agosti, 2023**. Utafiti utatumia mbinu ya ziara moja. Ili kushughulikia vyema tofauti za msimu na kuboresha ubora wa taarifa kwa ujumla, taarifa za uzalishaji wa mazao ya misimu ya Vuli na Masika itatolewa katika moduli tofauti za dodoso wakati wa mahojiano. Takwimu za shughuli za uzalishaji wa mifugo, uvuvi, ufugaji wa samaki na ufugaji wa samaki zitakusanywa kwa muda wa marejeleo wa miezi 12, kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023.

### 1.6 Sehemu za Utafiti huu

Mzunguko wa kwanza wa AASS-2023 utakusanya taarifa zifuatazo:

Sehemu ya 0: Mchujo

Sehemu ya 1: Mwanzo wa Mahojiano

Sehemu ya 2: Orodha ya wanakaya na Utambuzi wa Wamiliki wa Mashamba

Sehemu ya 3: Orodha ya Mashamba

Sehemu ya 4: Orodha ya Vishamba Msimu wa Vuli

Sehemu ya 5: Orodha ya Mazao Msimu wa Vuli

Sehemu ya 6: Orodha ya Vishamba Msimu wa Masika

Sehemu ya 7: Orodha ya Mazao Msimu wa Masika

Sehemu ya 8: Uzalishaji wa Mazao ya Kudumu

Sehemu ya 9: Matumizi ya Mavuno ya Mazao

Sehemu ya 10: Upatikanaji wa Mbegu na Miche Msimu

Sehemu ya 11: Matumizi na Upatikanaji wa Pembejeo (Mbolea na Viuatilifu)

Sehemu ya 12: Mifugo Iliyotunzwa na Mabadiliko yake

Sehemu ya 13: Gharama za Uzalishaji za Mifugo

Sehemu ya 14: Uzalishaji wa Maziwa

Sehemu ya 15: Uzalishaji wa Mayai

Sehemu ya 16: Bidhaa Zingine za Mifugo

Sehemu ya 17: Uzalishaji wa Viumbe Maji

Sehemu ya 18: Kazi

Sehemu ya 19: Shughuli Nyingine za Kiuchumi

Sehemu ya 20: Usajili wa Mashamba

Mwisho wa Mahojiano

## 1.7 Vitendea Kazi vya Utafiti

AASS 2022/23 inachukua mbinu ya ziara moja na inajumuisha dodoso moja. Kwasababu ya mbinu mchanganyiko ya sampuli iliyowasilishwa katika sehemu ya 1.3 hapo juu, dodoso hili litajumuisha sehemu ya mchujo ambayo itawezeshwa kutambua kaya zote za kilimo zinazostahiki katika EAs zenye kaya zisizozidi 200, au sehemu ya mchujo haitaonekana katika EAs zenye zaidi ya kaya 200 (ambapo kaya zenye sifa zimechaguliwa moja kwa moja na kwa bahati nasibu kutoka kwenye orodha ya kaya zinazojishughulisha na kilimo kwenye Sensa ya Watu na Makazi ya 2022).

Dodoso litatumika kukusanya takwimu za utambulisho wa kaya, taarifa za wanakaya, shughuli zote za uzalishaji wa mazao katika msimu wa Vuli na Masika, shughuli za uzalishaji wa mifugo, uvuvi, ufugaji wa samaki, shughuli nyingine za kiuchumi na kazi.

## 1.8 Usiri wa Taarifa

Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2022/23 unafanywa chini ya Sheria ya Takwimu Sura 351 ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Sheria ya Takwimu Na. 9 ya mwaka 2007 ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, zinazozipa ofisi hizo dhamana ya kusimamia ukusanyaji, uchakataji na uhifadhi wa takwimu kwa usiri na kutumika kwa matumizi ya kitakwimu tu. Hivyo, taarifa zote zitakazokusanywa kama majina, umiliki wa mashamba n.k hazitatolewa kwa mtu yeyote.

# 2 TARATIBU ZA UTENDAJI UWANDANI

## 2.1 Jukumu lako kama Mdadisi

Mdadisi ndiye mtekelezaji mkuu wa shughuli za ukusanyaji taarifa na mawasiliano ya moja kwa moja na kaya (wahojiwa). Hivyo basi, wadadisi wamebeba jukumu muhimu la kuhakikisha kuwa mahojiano yote yanasimamiwa na kukamilika. Kama wadadisi, ni muhimu kujenga mahusiano na maelewano mazuri na wahojiwa kabla ya kuanza kufanya mahojiano. Zaidi ya hapo, wadadisi lazima wafuate maelekezo yaliyomo katika mwongozo huu na nyenzo nyingine za ziada, wawe na uelewa wa sheria na kanuni za ofisi zinazohusiana na ukusanyaji wa taarifa na pia kufahamu dhana na misamiati iliyotumika.

Wadadisi wanapaswa kuichukulia kazi ya kuhoji kaya kama kazi tatu tofauti lakini zinazohusiana ambazo ni:

1. Kuuliza maswali kwa urahisi na kwa usahihi.
2. Kuandika/kurekodi majibu ya mhojiwa.
3. Kukagua ukamilifu, mantiki na uthabiti katika fomu.

## 2.2 Uhusiano kati ya wadadisi na msimamizi

AASS 2023 ina ngazi tatu za usimamizi ambazo ni:

i. *Usimamizi wa Ngazi ya Wilaya*

   Wasimamizi wa Wilaya (DS) watahakikisha kazi zote zinafanyika ipasavyo katika ngazi ya wilaya. Watakuwa na jukumu la kuangalia kama madodoso/fomu zote zimejazwa ipasavyo na kisha kuziwasilisha Ofisi ya Makao Makuu.

ii. *Usimamizi wa Ngazi ya Mkoa*

   Wasimamizi wa Mikoa (RSM) wana jukumu la kuhakikisha shughuli zote za ukusanyaji taarifa katika mkoa zinakamilika kwa ufanisi. Hili linaweza kufanyika kwa kuwatembelea wadadisi na kukagua kazi za wadadisi.

iii. *Usimamizi wa Ngazi ya Makao Makuu*

   Wasimamizi wa Makao Makuu wanasaidia wasimamizi wa mikoa na kusimamia kazi zote za ukusanyaji taarifa katika mikoa na kuwa kiungo kati ya Ofisi ya Makao Makuu na Mikoa.

Wasimamizi wa wilaya watakuwa uwandani mara kwa mara ili kusimamia kazi za kila siku za *ukusanyaji taarifa*. Mara chache, wasimamizi ngazi ya mkoa (RS/RSM) na makao

makuu (HQ) *watawatembelea wadadisi na kukagua maendeleo ya kazi*. Katika zoezi la ukusanyaji taarifa, wadadisi na wasimamizi wanatarajiwa kufanya kazi kwa uelewano na kujadili mara kwa mara maendeleo, *changamoto* na mahitaji ya *msaada* wowote katika kazi yao.

Wakati wa kutembelea uwandani, msimamizi wako atakuwa na kazi mahususi za kukamilisha. Msimamizi anaweza kutaka:

i) Kuangalia jinsi unavyofanya mahojiano.

ii) Kuangalia madodoso yote yaliyokamilika tangu ziara yake ya mwisho.

iii) Kufanya tena mahojiano kwa idadi ndogo ya kaya ili kuangalia usahihi wa taarifa ulizokusanya kutoka kwenye kaya.

Katika matukio ambayo msimamizi anakaa katika mahojiano yako au *kuorodhesha/kuhoji* upya kaya uliyotembelea, usichukulie kazi za wasimamizi kama tishio au kuingilia kazi yako kwani kila kazi ya mdadisi itatathminiwa kwa usawa. Vilevile, ili kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa utafiti, msimamizi wako pia atatathminiwa na msimamizi wake.

Kabla ya mdadisi hajamaliza kuhoji kaya, msimamizi atajadiliana nao mpango wao wa kazi. Hii ni muhimu ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa *shughuli za utafiti* na kwa wakati. Wadadisi wanahimizwa sana kujadili na wasimamizi wao changamoto zozote ambazo huenda walikumbana nazo wakati wa kukusanya taarifa, muda wa kazi uliopangwa, ziara zinazofuata za kaya na maelezo yao, vifaa vinavyohitajika na taarifa nyingine zozote muhimu. Msimamizi anaweza pia kupanga saa na tarehe ya ziara inayofuata ya mdadisi. Wakati miadi imepangwa, mdadisi lazima awepo na kwa wakati ili kukutana na msimamizi na kufikia kaya kwa wakati.

## 2.3 Jinsi ya kufanya mahojiano

Ni muhimu kwamba mdadisi awe na/akuze stadi za namna ya kufanya mahojiano zitakazosaidia kusaili vizuri na kwa utulivu. Zaidi ya hapo, mdadisi lazima awe tayari kubadilika kulingana na mazingira tofauti katika kaya na kujua jinsi ya kujibu haraka na kwa ufanisi. Hapa kuna baadhi ya miongozo:

a. Onesha bashasha na ushawishi mzuri kwa mhojiwa kuanzia mwanzo (maelewano mazuri). Kuwa mwenye urafiki na ustaarabu, lakini usipoteze muda katika kujadili mambo madogo yasiyo na mantiki.

b. Inashauriwa kuanza mahojiano kwa salamu au utangulizi wowote *wa heshima.*

c. Tumia dakika chache katika mazungumzo ya jumla au toa maoni juu ya kitu ambacho kinafurahisha katika ya mazingira ya eneo, ambacho mhojiwa anaweza kujivunia.

d. Mhakikishie mhojiwa kuhusu usiri wa taarifa anazotoa. Soma tamko kamili la ridhaa kama *ilivyoandikwa* kwa ujumla wake, na upate idhini ya mhojiwa kabla ya kuanza mahojiano.

e. Uliza maswali yote, hata kama unafikiri unajua majibu.

f. Uliza maswali kwa mpangilio kamili kama yanavyoonekana kwenye skrini ya kishikwambi.

g. Uliza maswali kama yalivyoandikwa katika fomu ya kuorodhesha kaya na kwenye dodoso. Kuwa mwangalifu usibadilishe maana yake au kuuliza maswali *elekezi* ambayo yanaweza kumfanya mhojiwa aamini kuwa kuna jibu sahihi/sio sahihi.

h. Inashauriwa *kufanya mahojiano kwa faragha*. Epuka kufanya mahojiano ya kikundi, lakini mhojiwa anaweza kushauriana na wanakaya wengine ili kuweza kupata taarifa sahihi. Zungumza na mwenye shamba aliyetambuliwa wakati wa awamu ya kuorodhesha kaya au mwanakaya mwingine yeyote ambaye anaweza kujibu maswali kwa usahihi (watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi na wanaofahamu shughuli za kilimo za kaya wanaweza kuhojiwa). Iwapo hutapata mwanakaya yeyote mwenye *uelewa na shughuli za kilimo za kaya*, weka miadi na itembelee kaya *tena hadi mara* mbili.

i. Sikiliza kwa makini majibu ya mhojiwa. Unaweza kupata majibu ya maswali kadhaa kwa mara moja. Usitoe maoni juu ya maswali ya utafiti. Usioneshe mshangao, kukubaliana au kutokubaliana na majibu ya mhojiwa.

j. Hakikisha umeingiza jibu la mhojiwa kwa usahihi kabla ya kuendelea na swali linalofuata.

k. Ikiwa mhojiwa hajaelewa swali, daima ni muhimu kurudia, na kwa maneno rahisi.

l. Ikiwa mhojiwa anaonekana kusita au kusitasita kujibu maswali, taja umuhimu na thamani ya taarifa za utafiti. Eleza kwamba taarifa anazozitoa ni siri, na majibu yaliyotolewa hayawezi kutumika kwa madhumuni ya kodi, uchunguzi au *udhibiti. Mhojiwa ana haki ya kutojibu swali,* hivyo using'aganie kupata jibu ikiwa kwa utashi wako umeona haiwezekani.

m. Hakikisha kuwa maswali yote yameulizwa kabla ya kukamilisha mahojiano.

n. Usijadili mambo ya siasa, au mambo mengine yenye utata.

o. Unaweza kupanga miadi ya kutembelea tena kaya ikiwa mhojiwa ataomba hivyo.

p. Kuwa tayari kuonesha kitambulisho chako wakati wowote mhojiwa akihitaji.

q. Kila mara mshukuru mhojiwa wakati mahojiano yanapokamilika na wajulishe kwamba unathamini mchango wao katika kufanikisha utafiti.

## 2.4 Jinsi ya kuuliza maswali

Madodoso yanahitaji ufafanuzi juu ya mada muhimu za uzalishaji wa Kilimo, na mdadisi wa eneo la utafiti anatarajiwa/anapaswa kuuliza maswali kwa usahihi kwa kutumia lugha ya Kiswahili au lugha ya wenyeji. Mdadisi vilevile anatarajiwa/anapaswa kuyafahamu/kuyaelewa maswali kwa umakini na **lazima aepuke** kumsomea Mhojiwa maswali neno kwa neno. Katika hali hiyo, Mdadisi lazima awe mwangalifu anapouliza maswali nyeti (kwa mfano mapato na umiliki wa ardhi, n.k). Kwa urahisi wa rejea, orodha ya baadhi ya misamiati na tafsiri zake inaweza kuingizwa kwenye dodoso ili kusaidia kutoa maelezo ya haraka kwa ajili ya uhakiki wa papo kwa papo.

## 2.5 Kurudi kwenye kaya na kukataa mahojiano

### 2.5.1 Ulazima wa kurudi kwenye kaya

Wakati wa mahojiano/kuhoji, unaweza/huenda usipate mwanakaya yeyote anayehusika katika kaya. Andika maelezo katika daftari lako na utenge muda wa kutembelea tena kaya hiyo. Jaribu kutembelea kaya angalau mara tatu. Ni muhimu pia kumtaarifu/kumjuulisha

msimamizi wako juu ya kaya zinazorejewa, sababu na mipango iliopo ya kutembelea/kuirejea tena kaya.

### 2.5.2 Kukataa mahojiano

Idadi kubwa ya watu hushiriki kikamilifu katika tafiti za kitaifa, na hivyo kukataa huwa ni nadra sana. Hata hivyo, kuna uwezekano wa kupata/kukuta mhojiwa ambaye anakataa/anasita kidogo kutoa taarifa kwa sababu ya kutojua umuhimu wa taarifa anayoitoa. Katika hali kama hiyo, Mdadisi anaweza kujaribu kuwashawishi kuondokana na msimamo wao, kuwahakikishia juu ya utunzaji siri wa taarifa watakazotoa na kuwafahamisha kuwa taarifa hizo zitatumika kwa madhumuni ya kitakwimu pekee. Pia, jambo muhimu ambalo linaweza kuchangia hali ya kaya kukataa kuhojiwa ni mtazamo au tabia za mdadisi, ambaye muda wote anatakiwa kubaki mtulivu na kuonesha heshima na bashasha. Mdadisi hapaswi kubishana au kukasirika. Badala yake, anapaswa kumfahamisha mhojiwa kwa upole kuhusu umuhimu wa taarifa zinazotolewa katika uandaaji wa sera. Ikiwa bado watakataa kuhojiwa, washukuru, ondoka kwenye kaya na umpe taarifa msimamizi wako.

## 2.6 Nyenzo na vifaa vya utafiti

Orodha inayotolewa hapa ni kwa lengo la kupata hesabu ya vifaa vyote vinavyohitajika na kutolewa kwa utafiti. Ikiwa huna zana na vifaa vyote hivyo, tafadhali wasiliana na ofisi kuu/msimamizi kabla ya kuendelea na ukusanyaji wa taarifa. Vifaa vyote vilivyotolewa vinakusudiwa kumsaidia mdadisi kukusanya taarifa kwa ufanisi. Tafadhali vitunze vifaa vyote kwa uangalifu, na utoe taarifa kwa msimamizi wako kwa kifaa chochote ambacho hakipo au hakifanyi kazi vizuri.

| | **Kifaa** | **Mpokeaji** |
|---|---|---|
| 1. | Kishkwambi chenye ulinzi wa kioo na kifuniko | Wadadisi na Msimamizi |
| 2. | Kifaa cha Majira nukta/GPS na Betri | Wadadisi na Msimamizi |
| 3. | Kifaa cha kuhifadhia Umeme (Power Bank) | Wadadisi na Msimamizi |
| 4. | Madaftari | Wadadisi na Msimamizi |
| 5. | Penseli/Peni | Wadadisi na Msimamizi |
| 6. | Kichongeo | Wadadisi na Msimamizi |
| 7. | Kifutio | Wadadisi na Msimamizi |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Viatu vya Mvua | Wadadisi na Msimamizi |
| 9. | Makoti ya Mvua | Wadadisi na Msimamizi |
| 10. | Mikoba | Wadadisi na Msimamizi |
| 11. | Bando/Vifurushi vya internet | Wadadisi na Msimamizi |
| 12. | Vizibao | Wadadisi |
| 13. | Vikokotoa | Wadadisi |
| 14. | Muongozo wa Mdadisi | Wadadisi |
| 15. | Dodoso (Kivuli cha dodoso) | Wadadisi |
| 16. | Fomu ya kuorodhesha | Wadadisi |

# 3 JINSI YA KUKAMILISHA DODOSO

## 3.1 Kutambua eneo na kaya/mhojiwa

Maeneo ya Kuhesabia Watu (Enumeration Areas-EAs) yana orodha ya vijiji vilivyotambuliwa mwaka 2022 wakati wa Sensa ya Watu na Makazi ya 2022. Hivyo, mipaka ya maeneo ya kaya na vijiji inapaswa kuwa kama ilivyokuwa mwaka wa 2022. Hata hivyo, utapewa utambulisho wa eneo la kaya kama vile majina ya vijiji, kata, wilaya na mkoa. Taarifa hizi zitaonekana kwenye ukurasa wa jalada wa dodoso la kielektroniki. Mara tu unapoipata kaya, thibitisha kuwa uko mahali sahihi. Zaidi ya hapo, thibitisha utambulisho wa eneo pamoja na mhojiwa husika wakati wa mahojiano, na kama makosa yamegunduliwa, weka majina na mageresho sahihi.

## 3.2 Kanuni za jumla za kujaza dodoso

Kabla ya kuanza mahojiano, ni muhimu kuhakikisha kuwa vifaa vyote vya mahojiano (kishikwambi, kitunza umeme, kifaa cha GPS, simu, n.k) viko katika hali nzuri ya kufanya kazi kwa:

i. Kuhifadhi kishikwambi kwenye jalada lake muhimu;
ii. Kuchaji kishikwambi na kitunza umeme kila jioni (Kumbuka: Kishikwambi kinahitaji saa 1-2 ili kujaa chaji vizuri).

Wakati wa kujaza dodoso, wadadisi wanapaswa kuzingatia kanuni zifuatazo:

i. Hakikisha kuwa vipengele/sehemu zote za dodoso zimejazwa vizuri.
ii. Kwa jibu la "null", acha wazi SIO "sifuri".
iii. Baada ya kukamilisha dodoso, lipitie kabla ya kuondoka kwenye kaya na uthibitishe kwamba taarifa zote zinazohitajika zimejazwa ipasavyo.
iv. Maswali yote yanapaswa kuulizwa kwa mwenye/mtunza shamba au kwa mwanakaya mwingine yeyote mtu mzima ambaye anafahamu vyema shughuli za uzalishaji wa kilimo katika kipindi cha marejeleo.

***Kumbuka*: Vifupisho vyote vya vipimo na maneno vimetolewa. Kwa mfano: Ek .= Ekari, Ha. = Hekta, Na. = Namba.**

Kuna matukio, na mara nyingi ni ya kawaida, ambapo wakulima hukadiria kiasi kwa katika vipimo visivyo vya kawaida (au vipimo vya kienyeji) badala ya vile vipimo vya kawaida

(kwa mfano, Kilo, Lita, Ekari, Hekta nk.). Pale inapowezekana, mhimize mhojiwa kutumia vipimo vya kawaida. Iwapo hii haiwezekani, rekodi vipimo vya kienyeji vilivyotolewa na mhojiwa.

## 3.3 Jinsi ya kujaza sehemu mahususi za dodoso

### 3.3.1 Jalada la mahojiano

Ukurasa wa jalada una taarifa zilizojazwa awali kuhusu taarifa za kijiografia, na kitambulisho cha mkuu wa kaya kinapopatikana (wakati EA ina zaidi ya kaya 200 na kaya za kilimo zimechaguliwa moja kwa moja kutoka kwenye sampuli mama ya Sensa ya Watu na makazi ya mwaka 2022 - jina la mkuu wa kaya na maelezo ya mawasiliano yatatolewa na kuwekwa kwenye mfumo ili kurahisisha eneo la wasailiwa). Kabla ya mahojiano, mdadisi anapaswa kutafuta eneo la kaya kwa kufuata maelezo ya eneo lililotolewa na mara atakapofika kwenye  kaya, anapaswa kuthibitisha maelezo ya eneo na mhojiwa na ikiwa makosa yamegunduliwa, masahihisho yafanyike.

### 3.3.2 Sehemu ya 0: Mchujo na Jalada la mahojiano

Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 1.3 hapo juu, uorodheshaji wa kaya zote katika EAs zenye kaya zisizozidi 200, mchujo wa kaya zenye vigezo na uchaguzi wa sampuli utafanyika kwa mpangilio kabla ya kuanza kwa mahojiano. Katika kila EA iliyochaguliwa ambayo inakidhi vigezo, wadadisi wataorodhesha kaya zote katika CAPI/SuSo na baada ya kukamilisha, watawasilisha taarifa kwa msimamizi wao SuSo. Msimamizi atachuja orodha iliyopokelewa kutoka kwa kila EA na kuchagua kaya zote zinazokidhi vigezo. Kutoka kwenye orodha ya kaya zilizokidhi vigezo, msimamizi atatumia mbinu ya sampuli (bahati nasibu) ili kuchagua kaya kumi na mbili zinazojishughulisha na kilimo kwa kila EA ili kuhojiwa. Wadadisi watagawanywa kwenye kaya zilizochaguliwa kwa ajili ya kufanya mahojiano kupitia CAPI/SuSo. Kwa EAs zenye zaidi ya kaya 200, hakuna uorodheshaji utakaofanywa, badala yake, kaya zinazokidhi vigezo zitachaguliwa kwa mfumo wa bahati nasibu moja kwa moja kutoka kwenye Mfumo wa Sampuli ya Sensa ya Watu na Makazi ya 2022 na kazi zinazohitajika kufanywa zitatumwa moja kwa moja kwa wadadisi kwa mahojiano.

### 3.3.3 Sehemu ya 1: Mwanzo wa Mahojiano

Sehemu hii inatoa miongozo kwa mhojiwa kuhusu mambo ya kufanya baada ya kuitambua kaya inayohojiwa. Kwanza, baada ya kufika kwenye kaya, salimia utakaowakuta, jitambulishe kwa kuelezea madhumuni ya utafiti juu y. Mhakikishie mhojiwa kuwa taarifa unayotaka kuikusanya itatumika kwa madhumuni ya kitakwimu/utafiti pekee, na itakuwa ni SIRI.

Orodha ya kuhakiki (checklist) imetolewa kumwezesha mdadisi kuhakiki taarifa za kaya na mahali ilipo kupitia maongezi yake na mhojiwa. Tafadhali kumbuka kuwa, swali namba 1 HALITASOMWA kwa sauti kwa mhojiwa. Baada ya kupata mwanakaya wa kumuhoji, omba ridhaa ya kuanza mahojiano nae kama inavyosomeka katika kishikwambi.

**Swali la 06: Je, kuna mwanakaya yeyote katika kaya yako/shamba lako alijishughulisha na shughuli za kilimo cha mazao wakati wa MSIMU WA VULI au MASIKA katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Muulize mhojiwa kama kuna mwanakaya yeyote alijihusisha na shughuli za kilimo katika mwaka wa kilimo 2022/23 na weka geresho husika. Kumbuka kubainisha kwa kurejea msimu husika.

**Swali la 07: Je, kuna mwanakaya yeyote katika kaya yako/shamba lako alimiliki au kutunza mifugo katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Katika Swali hili, muulize mhojiwa kama kuna mwanakaya yeyote alitunza mifugo au wanyama jamii ya ndege katika kipindi cha mwaka wa kilimo 2022/23 na uweke geresho husika.

**Swali la 08: Je, kuna mwanakaya yeyote katika kaya yako/shamba lako alijishughulisha na shughuli za ufugaji wa nyuki katika mwaka wa kilimo 2022/23**?
Katika swali hili, muulize mhojiwa kama kuna mwanakaya yeyote alijishughulisha na ufugaji wa nyuki kwa mwaka wa kilimo 2022/23.

**Swali la 09: Je, kuna mwanakaya/mtu yeyote katika kaya yako/shamba lako alijishughulisha na shughuli za ukuzaji wa viumbe maji katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Katika swali hili, muulize mhojiwa kama yeye au mwanakaya yeyote alijishuhulisha na ukuzaji wa viumbe maji katika mwaka wa kilimo 2022/23. Shughuli hizi zinajumuisha ufugaji wa samaki au/na unenepeshaji wa kaa na viumbe wengine wa majini kama vile majongoo wanaofugwa kwenye vizimba, bwawa la asili (inaweza kuwa bwawa dogo au kubwa) pamoja na kilimo cha mwani. Jaza geresho linalohusika.

***Imepangwa katika CAPI: CAPI VAR0: ikiwa, jibu ni 'Ndiyo' katika swali na 6 na/au 7 na/au 9? Ikiwa hali hiyo itatimizwa, kaya hiyo inastahiki kuhojiwa***
Muda na tarehe ya mahojiano itazalishwa/itajitokeza moja kwa moja katika SuSo/CAPI.

### 3.3.4 SEHEMU YA 2: ORODHA YA WANAKAYA NA UTAMBUZI WA WAMILIKI WA MASHAMBA

Sehemu hii inakusanya taarifa za wanakaya. Wanakaya ni watu ambao kwa kawaida huishi na kula pamoja (kushirikiana katika kupata mahitaji yao ya kila siku).

**Swali la 1: Tafadhali naomba unitajie majina ya watu wote ambao kwa kawaida wanaishi kwenye kaya hii ukianza na jina la mkuu wa kaya.**
Swali hili linataka uorodheshe majina kamili ya wanakaya wote ukianza na jina la mkuu wa kaya. Safu mlalo ya kwanza itajazwa taarifa za mkuu wa kaya na kisha wanakaya wengine wanaweza kupangwa kama ifuatavyo (au kwa mpangilio utakaotolewa na mhojiwa): mke/mume, watoto, wazazi (kuanzia Baba na kisha Mama), ndugu wa mkuu wa kaya na kisha wanakaya wengine ambao si ndugu lakini wanaishi na kula pamoja kwenye kaya (kama vile wafanyakazi wa ndani). Wakati wa kuorodhesha wanakaya, mhojiwa anapaswa kudadisi zaidi kwa mhojiwa ili kuhakikisha kama wanakaya wote halali wameorodheshwa kwa usahihi bila kuachwa.

***Kwa kila mwanakaya jaza swali namba 1 [Jina] na 2 [Jinsi] kwanza, kisha endelea na maswali mengine na ukamilishe taarifa za mwanakaya mmoja mmoja.***

**Swali la 2: Je, [Jina] ni mwanaume au mwanamke?**
Kwa kila mwanakaya aliyeorodheshwa, weka geresho la jinsi yake kama inavyostahili yaani *“1” kwa mwanaume na “0” mwanamke.*

**Swali la 3: Nini uhusiano wa [JINA] na mkuu wa kaya?**
Jaza geresho la uhusiano na mkuu wa kaya katika safu wima kutoka kwenye mageresho yaliyoorodheshwa. Geresho namba 1 ni kwa ajili ya mkuu wa kaya ambaye anatambulika na wanakaya wengine katika kaya husika kama kiongozi wao, hii inawezekana pia ikatokana na umri, n.k. Geresho namba 2 linahusu mwenza (wenza) wa mkuu wa kaya, na Geresho namba 3 linahusisha watoto wa mkuu wa kaya, geresho namba 4-7 yanatambulisha wanakaya wengine (ndugu wa damu na ndugu wengine wa mkuu wa kaya) kama inavyostahili.

**Swali la 4: Je, [Jina] ana umri gani?**
Umri wa mwanakaya unajazwa kwenye swali hili. Umri ni kipindi cha maisha kati ya tarehe ya kuzaliwa na tarehe ya siku ya mahojiano. Jaza umri ulio kamili, kwa mfano umri wa miaka 32 na miezi 9 jaza miaka 32; mwanakaya mwenye umri wa chini ya mwaka mmoja jaza 0.

**Swali la 5: Je, [JINA] alifanya kazi katika shughuli yoyote ya kilimo katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Swali hili litaulizwa kwa kila mwanakaya mwenye umri wa miaka 5 na Zaidi. Uliza kama mwanakaya alijihusisha na shughuli zozote za kilimo katika mwaka wa kilimo 2022/23 kisha jaza geresho linalohusika.

**Swali la 6: Je, [JINA] huwa anafanya maamuzi muhimu kuhusu shamba?**

Swali linalenga kubainisha wanakaya walio na umri wa miaka 15 na zaidi, na wanaofanya maamuzi muhimu ya kiuchumi au maamuzi ya kawaida ya kila siku kuhusu shamba. *Maamuzi muhimu ni pamoja na aina ya mazao yatakayopandwa, aina ya pembejeo zitakazotumika, ukubwa wa uzalishaji, ukodishaji wa ardhi, mauzo ya mazao na mifugo, miongoni mwa mengine. Maamuzi ya mara kwa mara ni pamoja na maamuzi ya wakati shughuli za shamba kama vile palizi, kudhibiti wadudu, kunywesha maji na kulisha mifugo, miongoni mwa mengine yanayofanywa.*

Wanakaya waliothibitisha kuwa watoa maamuzi watawekewa geresho "1" na "0" vinginevyo.

**Imepangwa katika CAPI- CAPI-VAR1: ni swali la 6=1? Maswali ya 7 hadi 9 yanatumika iwapo Swali la 6=1 pekee.**

**Swali la 7: Je, [JINA] amewahi kuhudhuria shule?**

Muulize mhojiwa kama [**JINA**] amewahi kuhudhuria shule na weka geresho linalohusika. Swali hili litaulizwa kwa wanakaya ambao wanafanya maamuzi kuhusu shamba tu.

**Swali la 8: Je, ni kiwango gani cha juu cha elimu [JINA] alichohitimu?**

Swali linakusanya taarifa juu ya elimu ya wanakaya. Muulize mhojiwa kuhusu kiwango cha juu cha elimu ambacho [JINA] amekamilisha. Baada ya kupata majibu jaza geresho linalohusika. *Kwa mfano: Kwa wale waliosoma hadi darasa la tatu lakini hawakumaliza, basi kiwango chao cha juu cha elimu kitakuwa "elimu ya msingi isiyokamilika".*

**Swali la 9: Je, [JINA] amewahi kupata mafunzo yoyote rasmi yanayohusiana na kilimo ikijumuisha mafunzo ya huduma ya ugani?**

Swali hili linakusanya taarifa za wanakaya ambao wamewahi kupata mafunzo rasmi ya kilimo, ikijumuisha mafunzo kutoka kwa watoa huduma za ugani. Muulize mhojiwa kama [JINA] amewahi kupata mafunzo rasmi au ya ugani katika kilimo. Baada ya kupata majibu ya mhojiwa, jaza geresho husika.

**Swali la 10: Je, kuna mwanakaya yeyote katika kaya hii aliwahi kushiriki kwenye programu zifuatazo?**

Muulize mhojiwa iwapo [JINA] amewahi kushiriki katika program tofauti ambazo zimeorodheshwa katika dodoso. Msomee mhojiwa program zote zilizoorodheshwa moja baada ya nyingine, kisha jaza geresho linalohusika. Jibu zaidi ya moja linakubalika.

### 3.3.5 SEHEMU YA 3: ORODHA YA MASHAMBA

Madhumuni ya sehemu hii ni kukusanya taarifa za mashamba yote yaliyotumika na kaya katika mwaka wa kilimo 2022/23 kwa ajili ya shughuli za kilimo pamoja na taarifa za

ukubwa wa eneo la shamba. Kumbuka kwamba jumla ya eneo la shamba ni sawa na eneo lote la ardhi lililotumika na kaya kwa ajili ya kilimo.

Mashamba yote yaliyotumika (ikijumuisha mashamba yaliyokodiwa, yaliyoazimwa, yaliyopokelewa kama zawadi, nk) na kaya kuanzia **Oktoba 2022 hadi Septemba 2023** yataorodheshwa bila kujali matumizi yake. Mashamba yote ambayo yalitumika kwa sehemu, yaliyoachwa, yaliyopumzishwa kwa muda au maeneo ambayo hayakutumika pia yatajumuishwa.

***Angalizo: Kabla ya kumuuliza mhojiwa taarifa za mashamba hakikisha umemuelewesha vizuri maana ya shamba.***

Kwa madhumuni ya Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2022/23,
Shamba ni kipande chochote cha ardhi chenye aina yoyote ya umiliki kilichozungukwa na ardhi nyingine, maji, barabara, msitu au mazingira yenye sura nyingine ambayo sio sehemu ya shamba hilo au yaliyo sehemu ya shamba hilo yenye aina tofauti ya umiliki.

**Swali la 00: Utambulisho wa shamba:**

Safuwima ya utambulisho wa shamba itapewa namba ambayo ndiyo inayotambulisha shamba katika msimu husika. Utambulisho wa shamba ni muhimu sana, kwa kuwa ndicho kitambulisho cha kipekee cha shamba na taarifa zake zote katika sehemu nyingine za dodoso huanishwa kwa kutumia utambulisho wa shamba. muulize mhojiwa akutajie mashamba yote ambayo kaya iliyatumia katika mwaka wa kilimo 2022/23, bila kujali matumizi yake. Mashamba yaliyopo ndani ya eneo la kuhesabia (EA) yanapaswa kuorodheshwa mwanzo, yakifuatiwa na yale ambayo yapo nje ya eneo la kuhesabia.

**Swali la 1: Jina la shamba**

Kwa kila shamba linalosimamiwa na kaya katika mwaka wa kilimo 2022/2023, muombe mhojiwa akutajie jina la shamba husika, ikiwezekana jina ambalo pengine tayari linatumika kwa kutambulisha shamba hilo. Kama shamba halina jina mwambie mhojiwa akutajie jina ambalo litakuwa rahisi kwake kulikumbuka wakati wa mahojiano. Mashamba yanaweza kupewa majina kutokana na mazao makuu yaliyopandwa, eneo lilipo au sifa mahsusi katika eneo husika kama vile mabonde, mto nk.

**Swali la 2a: Je, shamba la [JINA LA SHAMBA] lipo wilaya ya [JINA LA WILAYA]?**

Suala linataka kujua, kama shamba husika liko katika wilaya ambayo kaya inaishi au la. Jaza geresho 1 ikiwa jibu ni ndiyo na 0 ikiwa jibu ni hapana

**Swali la 2b: Je [JINA LA SHAMBA] lipo mkoa gani?**

Swali hili linaulizwa endapo tu shamba husika halipatikani katika wilaya inapoishi kaya. Weka geresho husika kutokana na mkoa ambao shamba linapatikana.

**Swali la 2c: Je, [JINA LA SHAMBA] lipo wilaya gani?**

Ikiwa geresho la swali la 2a=0, uliza wilaya ambayo SHAMBA linapatikana na weka geresho linalohusika.

**Swali la 3: Je, ulitumia [JINA LA SHAMBA] katika MSIMU WA VULI /MSIMU WA MASIKA au MISIMU YOTE katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Muulize mhojiwa kama shamba lilitumika katika msimu wa Vuli au Masika au misimu yote miwili katika mwaka wa kilimo 2022/23 na weka geresho linalohusika.

**Swali la 4a: Je, shamba la [JINA LA SHAMBA] lina ukubwa gani?**
Muulize mhojiwa kukadiria ukubwa wa eneo la shamba ikiwezekana katika vipimo rasmi kama vile mita za mraba, ekari au hekta na andika kipimo sahihi. Ikiwa kuna nyaraka za eneo kama vile hati miliki, omba kuona hati na jaza ukubwa wa eneo kama inavyoonesha katika hati.

**Swali la 5a: Je, kaya ililitumiaje [JINA LA SHAMBA] katika MSIMU wa VULI kwa mwaka wa kilimo 2022/23?**
Swali hili linataka kujua Shamba lilitumikaje katika msimu wa vuli katika mwaka wa kilimo 2022/23, mfano uzalishaji wa mazao, ukuzaji viumbe maji n.k. Swali hili litaulizwa tu kama geresho katika swali la 3 ni 1na 3.

**Swali la 5a_1: Asilimia ya shamba la [JINA LA SHAMBA] iliyotumika kwa [MATUMIZI]**
Ikiwa Swali la 5a litajibiwa, muulize mhojiwa asilimia ya [SHAMBA] iliyotumika kwa kila aina ya matumizi yaliyotajwa katika Swali la 5a na jaza jibu sahihi. Kwa mfano, kama mhojiwa atakupa matumizi makuu matatu kama vile makazi, uzalishaji wa mazao na majengo ya shamba basi orodhesha matumizi yote. hakikisha kuwa jumla ya asilimia kwa matumuzi ya shamba hayazidi asilimia mia moja (100).

***Imewekwa katika CAPI-CAPI-VAR2: Je, [KISHAMBA] kilitumika kupanda mazao katika MSIMU wa VULI wa 2022/23 uliopita? Ndiyo=1, kama Hapana = 0.***

**Swali la 5b: Je, kaya ililitumiaje [JINA LA SHAMBA] wakati wa MASIKA katika mwaka wa kilimo 2022/23??**
Swali hili linataka kujua Shamba lilitumikaje katika msimu wa Masika katika mwaka wa kilimo 2022/23. Swali hili litaulizwa tu kama geresho j katika swali la 3 ni 2 na 3.

**Swali la 5b_1: Je, ni asilimia ngapi ya [JINA LA SHAMBA] iliwekwa kwa kila matumizi?**
Ikiwa Swali la 5b litajibiwa, muulize mhojiwa asilimia ya [SHAMBA] iliyotumika kwa kila aina ya matumizi yaliyotajwa katika Swali la 5b na jaza jibu sahihi. Kwa mfano, kama mhojiwa atakupa matumizi makuu matatu kama vile makazi, uzalishaji wa mazao na

majengo ya shamba basi orodhesha matumizi yote. hakikisha kuwa jumla ya asilimia kwa matumuzi ya shamba hayazidi asilimia mia moja (100).

**Swali la 6A: Je, kulikuwa na miundombinu yoyote ya umwagiliaji kwenye [SHAMBA] hili katika MSIMU uliopita wa VULI wa 2022/23?**
Swali hili linalenga kubainisha uwepo wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba wakati wa msimu wa marejeleo. *Umwagiliaji unamaanisha ni namna ya kuiwekea ardhi maji mbali na ile hali ya kunyeshewa na mvua, kwa ajili ya kuboresha malisho au uzalishaji wa mazao. Umwagiliaji kwa kawaida humaanisha kuwepo kwa miundombinu na vifaa vya kuweka maji kwenye mazao, kama vile mifereji ya umwagiliaji, pampu, vinyunyizio au mifumo ya asili ya kumwagilia. Pia inajumuisha kumwagilia mimea kwa kawaida (kwa mkono) kwa kutumia ndoo, makopo ya kumwagilia au vifaa vingine. Mafuriko ya ardhi yasiyodhibitiwa kutokana na mito au vijito kufurika haichukuliwi kuwa umwagiliaji (Angalia WCA 2020 kwa maana ya misamiati).*

*Maelekezo: Majibu yanapaswa kujumuisha njia za umwagiliaji zinazosimamiwa kikamilifu (ikimaanisha njia ya usambazaji maji juu ya ardhi, vinyunyizio na njia za umwagiliaji za asili) na umwagiliaji unaosimamiwa kwa sehemu (ikimaanisha kudhibiti maji ya mafuriko na kuyatumia kumwagilia mazao au kuyaelekeza nyanda za chini zenye miundombinu).*

Muulize mhojiwa kama kulikuwa na miundombinu yoyote ya umwagiliaji shambani wakati wa msimu wa marejeleo na weka geresho sahihi linalohitajika. *Ikiwa hakuna (Hapana=0), ruka hadi Swali 8A.*

**Swali la 7A: Je, ni njia gani ya kumwagilia mimea/kumwaga maji kwenye mimea ilitumika kwenye [SHAMBA] hili katika MSIMU wa VULI uliopita wa 2022/23?**
*Kama Swali la 6A=1 "Ndiyo", muulize mhojiwa mbinu ya umwagiliaji iliyotumika shambani katika msimu wa marejeleo na weka geresho sahihi.*

*Tafsiri:*
**Swali la 8A: Je, ni vishamba vingapi vya mazao (pamoja na mashamba yasiyolimwa na bustani ya nyumbani) yalikuwa kwenye [SHAMBA] hili katika MSIMU wa VULI uliopita wa 2022/23?**
Muulize mhojiwa ni vishamba vingapi viko/vilikuwa kwenye shamba katika msimu wa rejewa, kisha rekodi. *Kishamba kinafafanuliwa kama kipande cha ardhi ambacho hakijagawanywa na chochote ambapo mazao maalum au mchanganyiko wa mazao hupandwa au ambayo hulimwa au kusubiri kupandwa.* Kwa hiyo, dadisi ili kuhakikisha kuwa mhojiwa anahesabu mashamba yote yaliyolimwa na mazao pamoja na mashamba ambayo yameachwa bila kulimwa kwa muda.

**Swali la 3B: Je, unatumia [SHAMBA] hili katika MSIMU unaoendelea wa MASIKA?**
Muulize mhojiwa kama wanatumia shamba kwa msimu wa masika unaoendelea wa mwaka 2023 na weka geresho linalohusika. Kama *Swali 3B ni Hapana-0, ruka na nenda Swali 9.*

**Swali la 4B: Je, [SHAMBA] hili linalotumika katika MSIMU wa MASIKA unaoendelea lina eneo wa ukubwa gani?**
Muulize mhojiwa akadirie eneo la shamba, ikiwezekana katika vipimo vya kawaida kama vile mita za mraba, ekari au hekta. Ikiwa sivyo, rekodi kipimo cha eneo kama ilivyotolewa na mhojiwa. Ikiwa eneo limerekodiwa kwenye nyaraka ya eneo, kama vile hati miliki, omba kuona hati na kurekodi eneo hilo. Iwapo eneo la shamba lililotumika katika msimu wa Masika ni sawa na lilivyokuwa katika msimu wa Vuli, tumia geresho "0=sawa na Vuli".

**Swali la 5B: Je, ni kwa namna gani kaya ilitumia [SHAMBA] hili katika MSIMU wa MASIKA unaoendelea na ni kwa asilimia ngapi ya eneo la [SHAMBA] kwa kila shughuli?**
Uliza kutoka kwa mhojiwa **matumizi makuu matatu ya shamba** na asilimia ya eneo la shamba kwa kila shughuli iliyofanyika kipindi cha msimu wa marejeleo. Kwa mfano, kama mhojiwa atakupa matumizi makuu matatu kama vile makazi, uzalishaji wa mazao na majengo ya shambani, hakikisha kwamba jumla ya asilimia ya shamba kwa shughuli hizo tatu inafikia asilimia 100.

***CAPI-VAR 3 imepangiliwa kwenye CAPI kwa ajili ya mashamba yanayotumika kupanda mazao katika msimu unaoendelea wa Masika. Ndiyo=1.***

### 3.3.6 Sehemu ya 4: Orodha ya vishamba msimu wa VULI

Madhumuni ya Sehemu hii ni kupata orodha kamili ya vishamba ndani ya mashamba yaliyomilikiwa na/au yaliyotumika (pamoja na yale yaliyokodishwa, yaliyokopwa, yaliyotolewa kama zawadi nk) na kaya wakati wa msimu wa Vuli kwa mwaka wa kilimo 2022/23.

***Kumbuka***
*Kishamba kinatafsiriwa kama eneo la ardhi ambalo ni sehemu ya shamba ambapo zao moja au mazao mchanganyiko yanalimwa au ambalo limeachwa bila kulimwa au linasubiri kupandwa.*

Sehemu hii inalenga kukusanya taarifa za matumizi ya kishamba, eneo lililolimwa, mfumo wa uzalishaji (zao moja au mchanganyiko/mseto), matumizi ya mbolea na madawa ya kilimo katika kishamba. Kabla ya kukusanya taarifa za kishamba, hakikisha kwamba

mhojiwa anakumbuka au ana taarifa za kutosha kuhusu shamba linalojumuisha vishamba husika.

Ni vema Mdadisi achukue tahadhari yakutochanganya majina ya vishamba ndani ya shamba husika yaani kila kishamba kinapaswa kupatiwa jina la kipekee. Vinginevyo, mfumo wa CAPI utatoa taarifa endapo majina yatajirudia.

**Swali la 00: Utambulisho wa kishamba**

Vishamba vyote ndani ya kila shamba vinapaswa kupewa utambulisho wa kishamba kwa madhumuni ya kufanya marejeo na kwa sehemu zingine zinazofuata katika utafiti. Kwa mfano, ikiwa shamba la kwanza (1), ambalo jina lake ni "mto" lina vishamba vitatu (3), basi kila kimoja kitapatiwa namba ya utambulisho kuanzia 1 hadi 3. Kisha vyote vitaorodheshwa, na kila kishamba kuchukua safu mlalo yake.

**Swali la 1: Jina la kishamba**

Kama ilivyobainishwa awali kwamba mdadisi hapaswi kurudia majina ya vishamba yanayofanana ndani ya shamba moja, Hivyo inashauriwa, anza kwa kuandaa orodha ya vishamba, kisha kamilisha kukusanya taarifa za kishamba kimoja. Kishamba kinaweza kupatiwa majina kulingana na msimu, namba ya kishamba (mfano Vuli Plot 1), mazao makuu, eneo, alama maalum kama vile mito, mabwawa na miundombinu mingine kwenye kishamba.

**Swali la 2: Katika MSIMU wa VULI wa Mwaka wa Kilimo 2022/23, kishamba cha [JINA LA KISHAMBA] cha shamba la [JINA LA SHAMBA] kilitumikaje?**

Kwa kila kishamba muulize mhojiwa namna kilivyotumika wakati wa msimu husika, na kisha chagua geresho sahihi linalohusika.

**Swali la 3: Je, kishamba cha [JINA LA KISHAMBA] cha shamba la [JINA LA SHAMBA] kilikuwa na ukubwa kiasi gani wakati wa MSIMU WA VULI wa 2022/23?**

Katika swali hili, mdadisi hatarajiwi kupima eneo la kishamba kwa kutumia kifaa cha GPS; badala yake atamuuliza mhojiwa ili akadirie eneo la [kishamba] katika kipimo kinachokubalika (kama vile ekari, hekta au mita za mraba) kadri inavyowezekana. Ni muhimu kuchukua tahadhari ili kuhakikisha kwamba: Eneo la kila kishamba lililokadiriwa lisizidi eneo la shamba husika. Aidha, jumla ya eneo lote la vishamba linapaswa kuwa pungufu ya au sawa na jumla ya eneo la shamba lote lililokadiriwa. Ujumbe wa tahadhari utaonekana katika CAPI ikiwa masharti haya hayatazingatiwa.

**Swali la 4: Je, kishamba cha [KISHAMBA] kilikuwa cha zao moja au mazao mchanganyiko katika MSIMU WA VULI uliopita wa mwaka wa kilimo 2022/23?**

*Swali hili litaulizwa ikiwa geresho katika swali la 2 ni 1 au 2.* Swali hili linataka kujua aina ya uzalishaji kwenye kishamba, katika msimu wa kilimo uliotajwa iwapo yalilimwa mazao mchanganyiko au zao moja.

***Kumbuka:***

***Zao linalojitegemea*****:** Hili ni zao pekee lililolimwa katika kishamba. Zao hilo linaweza kuwa ni la muda au la kudumu (Mfano kishamba kilichopandwa zao la mahindi tu au kishamba kilichopandwa miti ya parachichi tu)

***Mazao mchanganyiko*****:** Haya ni mazao tofauti ambayo hulimwa pamoja katika kishamba Mazao yatakuwa yamelimwa mchanganyiko endapo tu mazao mawili au zaidi yanayotofautiana (ya muda na / au ya kudumu) yamepandwa/yamelimwa pamoja kwenye kishamba. Idadi, aina na uwiano katika mchanganyiko kwa ujumla vitategemea mazingira yaliyopo au kwa kuangalia sababu kama vile udongo, mvua na hali ya hewa.

***Shamba/eneo lililopumzishwa***: Ni ardhi ambayo haijapandwa, kwa kawaida kwa msimu mmoja au zaidi. Mara nyingi, ardhi hiyo huachwa ili kuboresha rutuba ya udongo. Mashamba yasiyolimwa yanaweza kukatwa nyasi, kulimwa, au kunyunyiziwa kemikali ili kudhibiti magugu na wadudu. Mara nyingi, mashamba yaliyopumzishwa hayabaki tupu. Aidha, wakati mwingine hupandwa mimea kidogo au uoto ili kulinda shamba dhidi ya mmomonyoko wa ardhi.

**Swali la 5a: Je, kulikuwa na miundombinu ya umwagiliaji kwenye kishamba cha [KISHAMBA] wakati wa MSIMU wa VULI kwa mwaka wa kilimo 2022/23?**

Swali hili linataka kujua uwepo wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba katika mwaka wa kilimo wa 2022/23. Swali hili litaulizwa ikiwa geresho katika swali la 2 ni 1 "bustani ya nyumbani/kishamba cha nyumbani" au 2 "kililimwa mazao" Muulize mhojiwa kama kulikuwa na miundombinu yoyote ya umwagiliaji katika kishamba tajwa wakati wa msimu husika na kisha jaza geresho sahihi.

**Swali la 5b: Kwa makadirio ni asilimia ngapi au sehemu gani ya kishamba cha [KISHAMBA] ilimwagiliwa wakati wa MSIMU wa VULI katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

Swali hili litaulizwa ikiwa geresho katika swali la 5a ni 1 *"*Ndiyo". Muulize mhojiwa akadirie asilimia ya kishamba iliyomwagiliwa katika msimu husika na jaza jibu sahihi. *Mfano,* kishamba kilikuwa na ekari 30, kati ya hizo ekari 20 ndio zilimwagiliwa hivyo asilimia ya eneo lililomwagiliwa itakuwa ni 66.7 (20/30*100).

**Swali la 6: – Je, ni njia gani kuu ya kumwagilia mimea kwenye kishamba cha [KISHAMBA] ilitumika wakati wa MSIMU WA VULI katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

Swali hili litaulizwa ikiwa geresho katika swali la 5a ni 1 "Ndiyo", muulize mhojiwa njia kuu ya umwagiliaji iliyotumika katika kishamba wakati wa msimu husika.

***Maelezo ya mgeresho ya njia za umwagiliaji***

1. "Umwagiliaji kwa kutumia ndoo au chombo cha kunyweshea maji"- Ni umwagiliaji wa kawaida wa mkono kwa kutumia ndoo, jaba, kopo au kifaa kingine kinachofanania
2. "Umwagiliaji kwa kutumia sprinkler"- Inamaanisha mtandao wa mabomba ambayo maji hupitia chini kwa msukumo mkubwa kabla ya kumwagilia mmea kupitia kupitia matundu/nozeli za kifaa cha urushaji
3. "Umwagiliaji kwa kutumia mfumo wa matone (drip)"- Inamaanisha mfumo wa umwagiliaji wa kutawanya maji kwa msukumo wa chini kupitia mtandao wa mabomba ya chini kwa kutiririsha maji kidogokidogo kwa kila mmea
4. "Umwagiliaji kwa kutumia kufurika/Umwagiliaji wa usawa (surface)"- Ni mfumo wa kufunika ardhi kwa sehemu au yote kwa maji kwa madhumuni ya umwagiliaji. Inajumuisha matumizi ya mifereji ya maji, mikondo ya maji na umwagiliaji wa mabondeni.
5. "Nyingine (Taja)"- Kama kuna njia nyingine yoyote ya umwagiliaji ambayo haijatajwa katika njia zilizowekwa hapo juu jaza geresho 5 na taja njia hiyo.

**Swali la 7: Je, ulitumia mbolea ya asili kwenye kishamba hiki cha [SHAMBA] wakati wa MSIMU wa VULI kwa Mwaka wa Kilimo 2022/2023?**

Swali hili litaulizwa ikiwa geresho katika swali la 2 ni 1 "bustani ya nyumbani/kishamba cha nyumbani" au 2 "kililimwa mazao" Muulize mhojiwa kama walitumia mbolea yoyote ya asili kwenye mazao katika kishamba tajwawakati wa msimu wa vuli na chagua geresho sahihi.

***Kumbuka***

***Mbolea za asili*** ni zile zinazotokana na masalia ya mimea au wanyama. Aidha, mbolea hizo zinajumuisha samadi, mboji n.k..

**Swali la 8: Ni mbolea zipi za asili zilitumika kwenye kishamba hiki cha [KISHAMBA] wakati wa MSIMU wa VULI kwa Mwaka wa Kilimo 2022/23?**

Swali hili litaulizwa ikiwa geresho katika swali la 7 ni 1 "Ndiyo", Muulize mhojiwa aorodheshe aina zote za mbolea za asili zilizotumika kwenye kishamba tajwa na kisha chagua mageresho yote yanayohusika.

***Maana ya aina za mbolea***

**1. *Samadi ngumu:*** Ni mchanganyiko wa kinyesi kigumu cha wanyama wa kufugwa, wakati fulani inajumusha kiasi kidogo cha mkojo bila takataka zozote.

**2.** ***Samadi laini:*** Ni mchanganyiko wa kinyesi kibichi na kikavu cha wanyama, pamoja na au bila kuchanganywa na maji na/au kiasi kidogo cha takataka.
**3. Mabaki ya Mazao:** Ni mbolea inayotokana na mabaki ya mazao shambani baada ya mavuno.
4. ***Mboji: Ni*** Mbolea inayotokana na masalia ya viasili vya wanyama, mimea vilivyooza.
5. ***Mbolea maji taka***: Ni mbolea inayotokana na mabaki maji taka.
6. ***Mbolea kichocheo (Busta):*** *Pia hujulikana kama mbolea ya kibaolojia inayotokana na viumbe hai* au vilivyolala, kama vile bakteria na fangasi, ambayo hutoa virutubisho ili kuchochea ukuaji wa mimea.

**Swali la 9: Je, ulitumia mbolea za kiwandani kwenye kishamba hiki cha [KISHAMBA] wakati wa MSIMU WA VULI kwa mwaka wa kilimo 2022/23?**
Swali hili litaulizwa ikiwa geresho katika swali la 2 ni 1 "bustani ya nyumbani/kishamba cha nyumbani" au 2 "kililimwa mazao". Muulize mhojiwa kama walitumia mbolea yoyote ya kemikali/viwandani kwenye mazao katika kishamba tajwa na kisha chagua geresho linalohusika.

***Tafsiri:***
***Mbolea za kemikali/viwandani:*** Zinajumuisha vitu visivyo hai, hasa chumvi, vyenye virutubisho vinavyohitajika na mimea kama., nitrojeni (N), fosforasi (P), potasiamu (K) au muunganiko wowote wa virutubisho hivyo.

**Swali la 10: Je, ni mbolea zipi za viwandani (kemikali) zilitumika kwenye kishamba hiki cha [KISHAMBA] wakati wa MSIMU WAVULI kwa mwaka wa kilimo 2022/23?**
Swali hili litaulizwa ikiwa geresho katika swali la 9 ni 1 "Ndiyo", Muulize mhojiwa aorodheshe aina zote za mbolea za kemikali/kiwandani zilizotumika kwenye kishamba cha tajwa na kisha chagua mageresho yote yanayohusika.

***Maelekezo kwa mdadisi****: Iwapo mhojiwa alitumia mbolea ya kemikali/viwandani lakini hawezi kuitambua kwa usahihi, uliza kifungashio kama kinapatikana, kisha andika aina ya mbolea.*

**Swali la 11: Je, ulitumia viuwatilifu vyovyote kuua wadudu kwenye kishamba hiki cha [KISHAMBA] wakati wa MSIMU WAVULI kwa mwaka wa kilimo 2022/23?**
Swali hili litaulizwa ikiwa geresho katika swali la 2 ni 1 "bustani ya nyumbani/kishamba cha nyumbani" au 2 "kililimwa mazao". Muulize mhojiwa kama alitumia viuatilifu vyovyote kwenye kishamba tajwa kisha chagua geresho linalohusika.

***Kumbuka***
Viuatilifu ni dawa zinazozuia, uharibifu au kudhibiti viumbe waharibifu ("wadudu") au magonjwa, au kulinda mimea au mazao wakati wa uzalishaji, uhifadhi na usafirishaji.

**Swali la 12: Je, ulitumia viuatilifu gani kwenye kishamba hiki cha [KISHAMBA] wakati wa MSIMU wa VULI kwa Mwaka wa Kilimo 2022/23?**
Swali hili litaulizwa ikiwa geresho katika swali la 11 ni 1 "Ndiyo", Muulize mhojiwa aorodheshe aina zote za viuwatilifu vilivyotumika kwenye kishamba tajwa na kisha chagua mageresho yanayohusika.

***Tafsiri:***
1. ***Dawa za kuua wadudu:*** dawa ya kuua au kufukuza wadudu.
2. ***Dawa ya kuua magugu ya unga:*** Ni dawa ya unga inayotumika kuua au kuzuia mimea isiyohitajika kwenye kishamba.
3. ***Dawa ya magugu (kimiminika):*** Ni dawa ya maji inayotumika kuua au kuzuia mimea isiyohitajika kwenye kishamba.
4. ***Dawa ya kuzuia ukungu/fungasi:*** Ni dawa inayotumika kuzuia ukungu au fungasi kwenye mimea.
5. ***Dawa ya panya:*** Dawa inayotumika kuua au kufukuza panya kwenye kishamba.

**Maelekezo kwa mdadisi***: Iwapo mhojiwa alitumia kiuatilifu lakini hawezi kukitambua kwa usahihi, uliza kifungashio kama kinapatikana, kisha uandike aina ya kiuatilifu.*

### 3.3.7 SEHEMU YA 5: ORODHA YA MAZAO MSIMU WA VULI

Sehemu inalenga kukusanya taarifa kuhusu orodha ya mazao yote ya muda na ya kudumu yaliyolimwa katika msimu wa vuli wa mwaka wa kilimo 2022/23. Taarifa za majina na mageresho ya mazao, uwiano wa jumla ya eneo lililo na mazao, muda wa kupanda, aina na kiwango cha mbegu/miche iliyotumika, njia za upandaji na idadi ya miti yenye tija iliyopatikana.

**Swali la 1: Tafadhali orodhesha mazao ya muda na mazao ya kudumu Pamoja na miti ya matunda kwenye kishamba cha [KISHAMBA] wakati wa MSIMU WA VULI kwa mwaka wa kilimo 202 2/23**
Katika swali hili, muulize mhojiwa kuorodhesha mazao yote yaliyopandwa kwenye kishamba tajwa katika shamba husika wakati wa msimu wa vuli wa mwaka wa kilimo 2023. Uliza mazao yoteyaliyopandwa bila kujali kama yalivunwa au la. Mdadisi atapaswa kumdadisi mhojiwa kuhusu mazao yoyote ambayo huenda hajayaorodhesha.

**Muhimu**
Ikiwa zao moja litachukua sehemu kubwa ya kishamba na mengine machache yaliyotawanyika, hali hiyo itachukuliwa kama kilimo cha zao moja. Hata hivyo, ikiwa mazao tofauti yalipandwa kwenye uwiano unaokaribiana kishamba hicho kitachukuliwa kuwa kimepandwa mazao mchanganyiko.

Anza na kishamba cha kwanza katika [shamba la kwanza na ingiza kila zao lililotajwa, kisha uliza kuhusu mazao kwenye kishamba kinachofuatia. Endelea hivyo hadi vishamba vya mashamba yote yamekamilika.

***Tafsiri***

***Mazao ya muda/msimu*** ni mazao yaliyopandwa na kuvunwa ndani ya msimu mmoja, wakati ***mazao ya kudumu*** ni yale ambayo yakishapandwa yanaweza kuvunwa zaidi ya msimu mmoja bila kupandwa tena. Mazao yote yaliyoorodheshwa yataainishwa kuwa ya muda au ya kudumu, na utenganishaji huu utatumika katika sehemu hii na nyinginezo. Uainishaji wa mazao kwamba ni muda au kudumu utabainishwa katika CAPI, na taarifa inaweza kuwekwa katika sehemu tofauti hata kama mazao yote mawili ya muda yalichanganywa kishamba kimoja.

**Swali 2: Je, katika MSIMU WA VULI wa mwaka wa kilimo 2022/23 kwa wastani ni asilimia ngapi ya eneo la [KISHAMBA] ilipandwa [ZAO]?**

Swali hili litaulizwa tu kwa vishamba vyenye mazao mchanganyiko (*ikiwa sehemu ya 4 swali la 4* geresho ni 2 "Mazao mchanganyiko*"),* na linalenga kubainisha uwiano wa kila zao kwa kishamba kilichopandwa mazao mchanganyiko. Eneo lenye mazao mchanganyiko linaweza kufanyiwa makadirio kwa njia yoyote inayoshauriwa, ili jumla ya asilimia za maeneo iwe mia moja (100).

**Swali 3: Je, ni mwezi gani ulipanda [ZAO] kwenye kishamba cha [KISHAMBA] wakati wa M SIMU WAVULI kwa mwaka wa kilimo 2022/23?**

Swali hili linahusu tu **mazao ya muda mfupi (mazao ya msimu)**. Kwa kila [zao] la msimu ambalo limeorodheshwa, muulize mhojiwa mwezi na mwaka ambao zao lilipandwa , na jaza geresho sahihi..

**Swali 4: Je, ulitumia mbegu za aina gani kwenye zao la [ZAO] wakati wa MSIMU WA MASIKA kwa mwaka wa kilimo 2022/23?**

Kwa kila zao la muda mfupi, muulize mhojiwa aina ya mbegu/miche au vipando vilivyotumika katika msimu wa VULI kwa Mwaka wa Kilimo 2022/23 kisha jaza geresho linalohusika.

**Ufafanuzi wa aina za mbegu**

1. **Mbegu zilizoboreshwa*:*** Ni zile mbegu ambazo zimeboreshwa na zinaweza kuwa zimethibitishwa kuwa zimefikia kiwango cha kitaifa cha kijenetiki kinachakubarika au bado hazijathibitishwa kwa viwango vya kitaifa.
2. **Mbegu za asili*:*** Ni mbegu zinazotokana na uchaguzi wa wakulima wenyewe. Aina hizi za mbegu kwa kawaida ni stahimilivu kwa kuzoea na kukabiliana na hali na changamoto za eneo husika. Aidha, aina hizi za mbegu hutambuliwa kwa ufasaha na wakulima.

3. **Mbegu bora iliyotumika tena:** Ni mbegu ambayo imepatikana kutoka kwenye mavuno ya mazao ambayo yalipandwa kwa kutumia mbegu bora katika msimu uliopita

**Swali la 5: Je, ulivuna [ZAO] kwenye kishamba cha [KISHAMBA] wakati wa MSIMU wa VULI kwa Mwaka wa Kilimo 2022/2023?**

Kwa kila zao katika kishamba, muulize mhojiwa kama alivuna kiasi chochote, na kisha chaguageresho linalohusika. Mdadisi anapaswa kumdadisi mhojiwa kwa umakini mkubwa ili asiache kutaja sehemu yoyote ya mazao yaliyovunwa hasa kutoka kwenye mazao ambayo yaliharibiwa kwa kiasi kikubwa na yale mazao yaliyovunwa yakiwa katika hali ya ubishi.

**Swali la 6: Je, kwa nini haukuvuna [ZAO] kwenye kishamba cha [KISHAMBA] wakati wa MSIMU WA VULI kwa mwaka wa kilimo 2022/23?**

Ikiwa Swali la 5=0 “Hapana”, muulize mhojiwa sababu za kutovuna zao katika kishamba wakati wa msimu wa vuli na kisha jaza mageresho yote yanayohusika.

**Swali la 7: Je, ni mwezi gani ulivuna [ZAO] kutoka kwenye kishamba cha [KISHAMBA] hiki wakati wa MSIMU wa VULI kwa Mwaka wa Kilimo 2022/23?**

Kwa kila zao kwenye kishamba, muulize mhojiwa mwezi/miezi na mwaka aliovuna zao na jaza mageresho yote yanayohusika.

**Swali la 7a: Je, ni katika hali gani ulivuna zao la [ZAO] katika kishamba cha [KISHAMBA]?**

Swali hili linataka kujua mazao yaliyovunwa yalikuwa katika hali gani. Mfano mhojiwa anaweza vuna mahindi yakiwa bado hayajakauka **“**Mahindi mabichi kwenye gunzi” au yakiwa yamekauka “Mahindi makavu nafaka”.

**Swali la 8: Je, ni kiasi gani cha zao la [ZAO] kwa ujumla ulivuna kutoka kishamba cha [KISHAMBA] katika hali ya [HALI YA ZAO] katika MSIMU WA VULI mwaka wa kilimo 2022/23?**

Swali hili linalenga kukusanya taarifa kuhusu jumla ya kiasi cha zao kilichovunwa kutoka kwenye kishamba. Taarifa ya kiasi kilichovunwa itachukuliwa kulingana na hali ya zao, na vipimo vilivyotumika. Kwa jinsi inavyowezekana, taarifa ya kiasi kilichovunwa inapaswa itolewe kwa vipimo rasmi. Hata hivyo, ikiwa mhojiwa hawezi kutaja katika vipimo rasmi, tumia vipimo atakavyokupa. Kwa kila zao lililovunwa kutoka kwenye kishamba jaza hali, kiasi kilichovunwa na aina ya kipimo kilichotumika.

**Swali la 9: Je, takriban ni asilimia ngapi ya kishamba [KICHAMBA] kilichopandwa Zao la [ZAO] kilivunwa Katika MSIMU wa VULI wa Mwaka wa Kilimo 2022/23?**

Swali hili linalenga kukusanya taarifa kuhusu uwiano wa kishamba [KISHAMBA] kilichopandwa zao la [ZAO] ambacho kilivunwa kwa sehemu au chote wakati wa mahojiano. Kama Swali la 5=1, muombe mhojiwa akadirie ni asilimia ngapi ya eneo lililopandwa lilivunwa.

***Maelekezo kwa mdadi:*** Kwanza uliza jumla ya ukubwa (thibitisha kama eneo lilisharipotiwa awali) wa kishamba, kisha uuliza ukubwa uliotumika kwa shughuli mbalimbali, na sehemu iliyovunwa kwa kila zao [ZAO].

**Swali la 10: Kwanini hukuvuna eneo lote lililopandwa [ZAO] kwenye kishamba cha [KISHAMBA]?**

Iwapo Swali la 5=0, muulize mhojiwa sababu ya kutovuna zao husika katika kishamba husika, na kisha chagua mageresho ya sababu kuu mbili.

**Swali la 11: Je, zao la [ZAO] kwenye kishamba cha [KISHAMBA] lilipandwa kwa upandaji wa mpangalio au kutawanywa?**

Swali hili linatumika kwa mazao ya kudumu pekee. Kwa kila [ZAO] katika kishamba muulize mhojiwa kuhusu namna ya upandaji ulivyotumika kwenye kishamba katika msimu husika. Kuna aina kuu mbili za upandaji ambazo ni kupanda kwa mpangilio na kupanda kwa kutawanyika/bila mpangilio. Jaza geresho linalofaa.

***Tafsiri:***

***Upandaji wa mpangilio*** hujumuisha mimea, miti na vichaka vilivyopandwa kwa utaratibu na mpangilio, kama vile kwenye bustani.

***Upandaji wa mtawanyiko/bila mpangilio*** ni upandaji wa mimea usiofuata utaratibu wala mpangilio ambao ni vigumu kukadiria eneo lililopandwa. Mara nyingi mimea hiyo hutawanyika kwa kukaribiana na kushikana.

**Swali la 12: Je, kulikuwa na mimea/miti mingapi ya [ZAO] kwenye kishamba cha [KISHAMBA] katika MSIMU wa VULI wa Mwaka wa Kilimo 2022/23?**

Swali hili litaulizwa kwa mazao ya kudumu pekee. Kwa kila [ZAO] katika kishamba [KISHAMBA], jaza idadi ya miti/mimea iliyopandwa kwenye kishamba [KISHAMBA]. Ikiwa mhojiwa hawezi kutoa hesabu, basi jana-99.

**Swali la 13: Je, ni mimea mingapi ya zao [ZAO] ilikua katika umri wa uzalishaji katika MSIMU wa VULI wa Mwaka wa Kilimo 2022/23?**

Swali hili litaulizwa kwa mazao ya kudumu pekee. Kwa kila zao [ZAO] katika [KIWANJA], jaza idadi ya miti/mimea iliyokua katika umri wa kuzaa (umri ambao mti/mmea uko tayari kutoa mazao yanayovutia kama vile matunda, kuni, utomvu n.k) kwenye kishamba [KISHAMBA]. Ikiwa mhojiwa hawezi kutoa hesabu, basi jaza -99.

**Swali la 14: Je, ulipanda zao la [ZAO] katika MSIMU wa VULI wa Mwaka wa Kilimo 2022/23?**
Swali hili litaulizwa kwa mazao ya kudumu pekee. Muulize mhojiwa kama walipanda [ZAO] lolote katika kishamba [KISHAMBA] katika msimu wa husika, na kisha chagua geresho husika.

### 3.3.8 Sehemu ya 6: Orodha ya vishamba msimu wa Masika

### 3.3.9 Sehemu ya 7: Orodha ya mazao Msimu wa Masika

Sehemu ya 6 na ya 7 maswali pamoja na maelezo yake yanafanana na yale ya Sehemu ya 4 na ya 5 katika Msimu wa Vuli. Jaza *Sehemu ya 6 "Orodha ya Vishamba Msimu wa Masika'* kwa kufuata maelekezo kama yalivyotolewa katika kujaza *Sehemu ya 4 "Orodha ya Vishamba Msimu wa Masika"* na pia jaza *Sehemu ya 7 "Orodha ya Mazao Msimu wa Masika"* kwa kufuata maelekezo kama yalivyotolewa katika kujaza *Sehemu ya 5 "Orodha ya Mazao Msimu wa Masika".*

### 3.3.9 Sehemu ya 8: Uzalishaji wa kudumu wa mazao

Sehemu hii inakusanya takwimu za uzalishaji wa mazao yaliyovunwa kutokana na mazao ya kudumu katika mwaka wa kilimo wa 2022/2023**. *Mazao ya kudumu*** ni mazao ambayo yakishapandwa huchukua zaidi yam waka mmoja shambani na hayahitaji kupandwa tena baada ya mavuno ya kila mwaka. Mara nyingi mazao ya kudumu huwa ni ya miti, kwa mfano Minazi, Michungwa, Mikarafuu n.k.

**Swali la 00: Utambulisho wa shamba**
Huu tuajazwa kiotomatiki katika CAPI.

**Swali la 00: Utambulisho wa Zao**
Kwa kila [ZAO] katika [KISHAMBA] kilichoorodheshwa, gereosho la zao litajazwa kiotomatiki katika CAPI.

***Imepangwa katika CAPI: Taarifa zote za shamba-kishamba-zao zitakuwa zimejazwa mapema kutoka kwenye orodha ya mazao.***

**Swali la 1: Je, ulivuna kiasi chochote cha zao la [ZAO] kwenye kishamba cha [KISHAMBA] katika mwaka wa kilimo 2022/2023?**
Kwa kila [ZAO] katika [KISHAMBA], muulize mhojiwa kama alivuna kiasi chochote za zao, na jaza taarifa kwa usahihi. Mdadisi anapaswa kuhoji kwa kina ili asiache sehemu yoyote ya mazao yaliyovunwa, hasa ikiwa kuna mazao ambayo yaliharibiwa kwa kiasi kikubwa na kupata mavuno kwa kiasi kidogo au mazao mapya yaliyovunwa kiasi.

**Swali la 2: Kwanini hukuvuna zao la [ZAO] kutoka kishamba cha [KISHAMBA] katika mwaka wa kilimo wa 2022/23?**
Ikiwa Swali la 1=0, waulize sababu kwa nini hawakuvuna [ZAO] katika [KISHAMBA] wakati wa mwaka wa kilimo 2022/23 na chagua mageresho yote yanayohusika.

**Swali la 3: Je, ni mwezi gani ulivuna zao la [ZAO] kutoka kwenye kishamba cha [KISHAMBA] katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Kwa kila [ZAO] kwenye [KISHAMBA], muulize mhojiwa mwezi/miezi ya kuvuna na jaza majibu sahihi.

**Swali la 3a: Je, ni katika hali gani ulivuna zao la [ZAO] katika kishamba cha [KISHAMBA]?**
Swali hili linalenga kujua hali ya zao wakati wa mavuno iwapo lilivunwa likiwa katika hali ya kukomaa au likiwa changa. Kwa mfano, zao la mnazi linaweza kuvunwa likiwa katika hali ya madafu au nazi. Kwa kila zao ambalo linaweza kuvunwa katika hali tofauti, muulize mhojiwa iwapo [ZAO] hilo lilivunwa katika hali gani.

**Swali la 4a: Je, kiasi gani cha zao la [ZAO] kwa ujumla ulivuna katika kishamba cha [KISHAMBA] katika hali ya [HALI YA ZAO] katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Swali hili linalenga kujua kiasi cha [ZAO] kilichovunwa kwenye [KISHAMBA] kwa kuzingatia hali ya zao. Kwa kadiri inavyowezekana, mavuno yanapaswa kuripotiwa katika vipimo vya kawaida. Hata hivyo, ikiwa mhojiwa hawezi kujua kiasi katika vipimo vya kawaida, tumia vipimo vilivyotolewa. Mdadisi ahakikishe kwamba anasoma na kuelewa masharti yote ya mazao yaliyotolewa katika kiambatisho. Kwa [ZAO] lililovunwa kutoka kwenye [KISHAMBA], jaza hali ya zao, kiasi kilichovunwa na kipimo kilichotumika kuvunwa kwenye nafasi iliyotengwa. *(Angalia maagizo ya jinsi ya kujaza safu katika* *Sehemu ya 3.3.7* *"Orodha ya mazao ya Vuli"*).

### 3.3.10 Sehemu ya 9: Matumizi ya mavuno ya mazao

Sehemu hii inakusanya takwimu za matumizi ya mazao ya muda na ya kudumu yaliyovunwa kuanzia msimu wa Vuli na Masika wa mwaka wa kilimo 2022/2023. Sehemu inalenga kukadiria mgao wa mavuno kwa matumizi mbalimbali kama vile kuhifadhi, mauzo, matumizi ya nyumbani, kutoa zawadi, fidia ya pembejeo za uzalishaji, malisho ya mifugo, mbegu zilizobaki na usindikaji.

**Swali la 00: KITAMBULISHO CHA ZAO**
*Itajazwa kiotomatiki katika CAPI Swali la 00: JINA LA ZAO Imepangwa katika CAPI: Orodhesha mazao yote yaliyovunwa kutoka Sehemu ya 5 na 7 (yaani, ikiwa Sehemu ya 5 Swali la 5=1) na Sehemu ya 7 (ikiwa ni sehemu ya 7 Swali la 5=1).*

***Imeratibiwa katika uzalishaji wa jumla wa CAPI-CAPI: Huhifadhi jumla ya uzalishaji wa zao hilo, katika misimu yote ya Vuli na Masika, na katika mashamba yote yanakolimwa.***

Kwa kila zao husika, msomee mhojiwa a kiasi cha "jumla ya uzalishaji" katika mwaka wa kilimo uliopita wa 2022/2023, kwa hivyo ni rahisi kwa mhojiwa kutathmini asilimia ya matumizi tofauti kutokana na uzalishaji huo. .

**Swali la 1: Je, kwa sasa una akiba ya zao la [ZAO] iliyovunwa katika mwaka wakilimo 2022/23, yaani kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?**

Muulize mhojiwa kama wana akiba ya [ZAO] lolote lililovunwa kutoka katika mwaka wa kilimo 2022/23 wakati wa mahojiano, na jaza geresho sahihi.

*Kumbuka usihusishe mazao ambayo hayakuvunwa katika mwaka wa kilimo 2022/23 lakini yamehifadhiwa.*

**Swali la 00: Uhifadhi**

*Imepangwa katika CAPI: Inachukua thamani ya mfuatano tupu ikiwa s1q01==0 na kuchukua thamani ya mfuatano ", ikijumuisha wingi katika hifadhi?" ikiwa s9q01==1*

**Swali la 2: Je, kaya/shamba yako/lako ilitumia/lilitumia mazao ya [ZAO] yaliyopo kwenye [HIFADHI] kwa madhumuni yoyote yafuatayo?**

Muulize mhojiwa kama [MAZAO] yaliyovunwa, ikiwa na yaliyopo katika [HIFADHI] kwa sasa yalitumika au yatatumika kwa madhumuni yaliyoorodheshwa, na jaza geresho sahihi kwa matumzi yote yanayo husika.

**Swali la 3: Ni asilimia ngapi au sehemu gani ya [ZAO] iliyovunwa katika mwaka wakilimo 2022/23 iliuzwa bila kusindikwa [] ikuhisisha mazao yaliyo hifadhiwa kwa sasa**

*Kumbuka kwamba mazao yaliyovunwa nje ya mwaka wa kilimo 2022/23 hayafai kujumuishwa.*

*Ufafanuzi:*

Bidhaa ***haijachakatwa/ghafi*** ikiwa haijabadilisha umbo. Bidhaa ***iliyosindikwa*** ni ile ambayo muundo wake wa asili umebadilishwa (km. Kutoka mahindi hadi unga wa mahindi ).

**Swali la 4: - Ni thamani gani kwa ujumla ya mauzo yote ya zao la[ZAO] ambayo hayajasindikwa??** ikiwa Qn 3>0, muulize mhojiwa makadirio ya thamani ya mauzo yote ya [ZAO] ambayo hayajasindikwa katika mwaka wa kilimo 2022/23 ikijumuisha thamani ya bidhaa, mauzo ya mkopo na mauzo yaliyokusudiwa (mauzo bado hayajafanywa ya mazao yaliyo hifadhiwa). Swali linalenga kukadiria jumla ya thamani ya mauzo yote ya mazao ambayo hayajasindikwa.

*Maelekezo kwa Mdadisi: Kama ilivyo kwa swali 3 hapo juu, rekodi thamani ya mauzo ya mazao katika hali ghafi. Kwa mfano, kama kaya ilisindika sehemu ya mahindi yao (Kilo 10 za nafaka) kuwa unga wa mahindi (iliyopatikana ni kilo 8) na kuuza unga, tafadhali ripoti hali ya zao kabla ya kusindika. yaani kilo 10 za mahindi ya nafaka.*

**Swali la 5: Ni asilimia ngapi au sehemu gani ya zao la [ZAO] iliyovunwa katika mwaka wa kilimo 2022/23 ilitumiwa na wanakaya kabla au baada ya kusindikwa?**
Swali hili linataka kukadiria uwiano wa jumla ya mavuno ya [ZAO] katika msimu wa kilimo 2022/23 ambayo litumiwa katika kaya. Mdadisi anatakiwa kuhoji kwa kina matumizi ya mara kwa mara ya zao hilo ndani ya kaya, ikiwa ni pamoja na **matumizi yaliyokusudiwa** ya zao lolote katika hifadhi. Mwambie mhojiwa kukadiria asilimia ya jumla ya mavuno ya [ZAO] ambayo yalitumiwa na kaya, ikiwa ni pamoja na kile wanachokusudia kutumia kutoka kwa mazao yoyote kwenye hifadhi, na kujaza geresho sahihi. Ikiwa [ZAO] lilichakatwa kwa ajili ya matumizi, lijumuishe hapa kama sehemu ya bidhaa ghafi (tazama maagizo katika Swali la 4 hapo juu).

**Swali la 6: Ni asilimia ngapi au sehemu gani ya zao la [ZAO] iliyovunwa katikaaka wa kilimo 2022/23 ilitolewa kama zawadi kwa kaya nying?**
Kwanza, muulize mhojiwa kama kaya ilitoa baadhi ya [ZAO] iliyovunwa katika mwaka wa kilimo wa 2022/23 kama zawadi/mahali, kisha andika asilimia ya jumla ya mavuno [ZAO] ambayo yalitolewa. Iwapo [ZAO] lilichakatwa kabla ya kutoa, lijumuishe hapa kama sehemu ya bidhaa ghafi (tazama maagizo katika Swali la 4 hapo juu).

**Swali la 7: Ni asilimia** ngap **au sehemu gani ya [ZAO] iliyovunwa katika mwaka wa kilimo 2022/2023 ilitumika kulipia ardhi, nguvu kazi au pembejeo?**
Kwanza, muulize mhojiwa kama kaya ilitumia baadhi ya [ZAO] iliyovunwa kuanzia mwaka wa kilimo 2022/23 kulipia ardhi, nguvu kazi au pembejeo, kisha iandike asilimia ya jumla ya mavuno ya [ZAO] ambayo yalitumika kwa malipo hayo. Iwapo [ZAO] lilichakatwa kabla ya kutoa kama malipo, lijumuishe hapa kama sehemu ya bidhaa ghafi (tazama maagizo katika Swali la 4 hapo juu).

**Swali la 8: Ni asilimia gani au sehemu gani ya [ZAO] iliyovunwa katika mwaka uliopita 2022/2023 ilitumika kwa ajili ya lishe ya mifugo?**
Kwanza, muulize mhojiwa kama kaya ilitumia baadhi ya [ZAO] iliyovunwa katika mwaka wa kilimo 2022/23 kama chakula cha mifugo, kisha andika asilimia ya jumla ya mavuno [ZAO] ambayo yalitumika kama chakula cha mifugo. Usijumuishe kiasi cha mavuno ya [ZAO] yanayotumika kama chakula cha mifugo kutokana na uharibifu wa wadudu.

**Swali la 9**: **Ni asilimia** ngapi **au sehemu gani ya zao la [ZAO] iliyovunwa katika mwaka wa kilimo 2022/2023 ilitumika kwa ajili ya mbegu katika msimu uliofuata?**
Kwanza, muulize mhojiwa kama kaya ilibakiza baadhi ya [ZAO] iliyovunwa kutoka mwaka wa kilimo 2022/23 kama mbegu kwa ajili ya matumizi katika msimu unaofuata, kisha andika asilimia ya jumla ya mavuno [ZAO] ambayo yalitumika kama mbegu.

**Swali la 10: Ni asilimia ngapi au sehemu gani ya [ZAO] iliyovunwa katika mwaka uliopita 2022/2023 ilichakatwa kwa ajili ya kuuzwa?**
Kwanza, muulize mhojiwa kama kaya ilisindika baadhi ya [ZAO] lililovunwa kwa mwaka wa kilimo 2022/23 kwa ajili ya kuuzwa, kisha andika asilimia ya jumla ya mavuno ya [ZAO] ambayo yalichakatwa kwa ajili ya kuuzwa.

Swali la 11: **Ni asilimia ngapi au sehemu gani ya [ZAO] iliyovunwa katika mwaka wa kilimo 2022/2023 ilitumika kwa ajili ya madhumuni mengine yoyote ambayo hayajatajwa?**
Kwanza, muulize mhojiwa kama kaya ilitumia baadhi ya [ZAO] lillovunwa kwa mwaka wa kilimo 2022/23 kwa madhumuni mengine isipokuwa yale ambayo tayari yametajwa, kisha andika asilimia ya jumla ya mavuno [ZAO] ambayo yalitumika kwa madhumuni mengine.

### 3.3.11 Sehemu ya 10. Upatikanaji wa mbegu/miche/vipando

~~**Maelezo:**~~
Sehemu hii inalenga kukusanya taarifa za ~~wingi~~ kiasi, gharama na vyanzo vya mbegu, miche au vipando ~~iliyotumika~~ vilivyotumika katika mwaka wa kilimo wa 2022/2023.
~~**Swali la 00: Kitambulisho cha mazao**~~

~~***Imepangwa katika CAPI: orodhesha hapa mazao yote ya muda na ya kudumu ambayo yamepandwa katika mwaka wa kilimo uliopita wa 2022/23.***~~

**Swali la 1:~~Ni kiasi gani cha jumla cha mbegu, miche au vipandikizi vilivyopandwa katika  MSIMU WA VULI wa 2022/23 uliopita?~~Je, kwa ujumla ni kiasi gani cha mbegu, miche, vipando vya zao la [ZAO] kilipandwa wakati wa MSIMU WAVULI wa 2022/23?**

Iwapo VAR2_ALLFIELDS = ni kweli, muulize mhojiwa kiasi cha mbegu/miche/vipando [ya ZAO] iliyopandwa katika msimu uliopita wa Vuli na jaza kiasi kisha weka geresho la kipimo husika.

**Swali la 2: ~~Ni kiasi gani cha jumla cha mbegu, miche au vipandikizi vilivyopandwa katika MSIMU wa MASIKA wa 2022/23 uliopita?~~Je, kwa ujumla ni kiasi gani cha mbegu, miche, vipando vya zao la [ZAO] kilipandwa wakati wa MSIMU WA MASIKA wa 2022/23?**

Iwapo VAR2_ALLFIELDS = ni kweli,~~muulize mhojiwa kuhesabu kiasi cha mbegu/miche [ya ZAO] ambayo ilipandwa katika msimu uliopita wa Masika na arekodi wingi na aweke alama ya kipimo kinacholingana.~~Muulize mhojiwa kiasi cha mbegu/miche/vipambo ya zao husika iliyopandwa katika msimu uliopita wa Masika na jaza kiasi kisha weka geresho la kipimo husika.

**Swali la 3~~: Nini chanzo cha mbegu, miche au vipandikizi vya [ZAO] vilivyotumika katika mwaka huu wa kilimo wa 2022/2023 uliopita?~~Je,nini kilikuwa chanzo cha mbegu, miche,au vipando kwa zao la [ZAO],kilicho tumika katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

Swali hili linaulizwa~~ tu~~kwa mazao ya muda na ya kudumu yaliyopandwa katika mwaka wa ~~kumbukumbu~~ kilimo wa 2022/23. Muulize mhojiwa ni wapi walipata mbegu/miche/vipando ya zao husika.~~chagua zote zinazohusika~~ Jibu zaidi ya moja linakubalika.

**Swali la 4: ~~Je, mbegu, miche au vipandikizi vya [ZAO] ulilonunua katika mwaka wa kilimo uliopita wa 2022/2023 vyote vilipewa ruzuku, kwa kiasi fulani au kutopewa ruzuku?~~Je, [kipimo] kwa zao la [ZAO] ulizonunua katika mwaka wa kilimo 2022/23 zote zilikuwa za ruzuku, zilikuwa za ruzuku kwa sehemu tu,au hazikuwa za ruzuku kabisa?**

Swali hili litaulizwa ikiwa ~~Kama~~jibu la Swali la 3ni geresho 5 "ununuzi kutoka kwa wafanyabiashara/wachuuzi",6"ununuzi kutoka taasisi za Serikali" au 7 "ununuzikutokachama cha wakulima".~~Lina Yoyote (5,6,7),~~Muulize mhojiwa kama walinunua mbegu/miche/vipando ya zao husika~~kwa bei ya ruzuku, iliyopewa ruzuku au isiyolipiwa jua katika mwaka wa marejeleo, na geresho kama inafaa.~~zote zilikuwa za ruzuku, zilikuwa za ruzuku kwa sehemu tu, au hazikuwa za ruzuku kabisa katika mwaka wa 2022/23.

**Swali la 5a: ~~Je, ni kiasi gani cha jumla cha mbegu, miche au vipandikizi vya [ZAO] visivyopewa ruzuku ambavyo ulinunua kwa mwaka wa kilimo uliopita wa 2022/2023?~~Je, kwa ujumla ni kiasi gani cha [kipimo] kwa zao la [ZAO] ulizonunua bila ruzuku kwa mwaka wa kilimo 2022/23?**

Iwapo Swali la 4, geresho ni 2 "kwa sehemu iliyo nunuliwa ilikua na ruzuku",3"hakuna iliyonunuliwa iliyokuwa na ruzuku", 98 "Sijui", muulize mhojiwa kiasi cha mbegu/miche/vipando ya zao husika isiyopewa ruzuku ambayo walinunua katika mwaka wa kilimo 2022/23, ~~andika kiasi~~na uweke geresho la kipimo husika~~kinacholingana~~.

**Swali la 5b: ~~Ni kiasi gani cha jumla cha mbegu, miche au vipandikizi vya ruzuku [ZAO] ulichonunua kwa mwaka wa kilimo wa 2022/2023 uliopita?~~Je, kwa jumla ni kiasi gani cha [kipimo] kwa zao la [ZAO] ulichonunua kwa ruzuku kwa mwaka wa kilimo 2022/23?**

Iwapo Swali la 4. ~~Kwenye orodha~~ geresho ni 1 "yote ilionunuliwa ilikua na ruzuku",2 "kwa sehemu iliyo nunuliwa ilikua na ruzuku", muulize mhojiwa kiasi cha mbegu/miche/vipando ilokuwa na ruzukuambayo alinunua katika mwaka wa kilimo 2022/23, andika kiasi na uweke ~~nambari ya kipimo husika~~geresho la kipimo husika.

**Swali la 6a~~: Bei ya wastani ya mbegu, miche au vipandikizi vya [ZAO] ulizonunua pasipo ruzuku kwa mwaka uliopita wa 2022/2023 ni kiasi gani?~~Kwa wastani ni bei gani kwa kipimo cha [kipimo] kwa zao la [ZAO] ulizonunua bila ruzuku kwa mwaka wa kilimo 2022 /23?**

~~Iwapo Swali la 4. Kwenye orodha (2,3,98), muulize mhojiwa wastani wa bei ya mbegu/miche isiyopewa ruzuku ya [ZAO] ambayo walinunua katika mwaka wa kumbukumbu na rekodi.~~ Iwapo Swali la 4, geresho ni 2 “kwa sehemu iliyo nunuliwa ilikua na ruzuku”, 3“hakuna iliyonunuliwa iliyokuwa na ruzuku”, 98 “Sijui”, muulize mhojiwa wastani wa beiya mbegu/miche/vipando ya zao husika isiyopewa ruzuku ambayo walinunua katika mwaka wa kilimo 2022/23, ~~andika kiasi~~na uweke geresho la kipimo husika ~~kinacholingana~~.

**Swali la 6b: ~~Bei ya wastani ya mbegu, miche au vipandikizi vya [ZAO] uliyonunua pasipomruzuku kwa mwaka uliopita wa 2022/2023 ilikuwa bei gani?~~Kwa wastani bei gani kwa kipimo, cha [kipimo] kwa zao la [ZAO] ulizo nunua kwa ruzuku kwa mwaka wa kilimo 2022/ 23?**

~~Kama Swali la 4. Kwenye orodha (1,2), muulize mhojiwa wastani wa bei ya mbegu/miche ya ruzuku ya [ZAO] ambayo walinunua katika mwaka wa marejeleo na rekodi.~~Iwapo Swali la 4. ~~Kwenye orodha~~ geresho ni 1 “yote ilionunuliwa ilikua na ruzuku”,2 “kwa sehemu iliyo nunuliwa ilikua na ruzuku”, muulize mhojiwa wastani wa bei ya mbegu/miche/vipando ya zao husika iliyokua na ruzuku ambayo walinunua katika mwaka wa kilimo 2022/23, rikodi bei na kipimo husika.

***Zingatia: Ruzuku ni kiwango cha fedha au fidia ambayo Serikali au Mashirika inatoakwa wakulima kwa madhumuni ya kupunguza gharama za pembejeo kwa wakulima (mfano: mbolea, mbegu, madawa n.k).***

### 3.3.12 Sehemu ya 11. Matumizi na upatikanaji wa pembejeo (mbolea na viuatilifu) Maelezo:

Sehemu hii inalenga kukusanya taarifa kuhusu upatikanaji na matumizi yapembejeo za kilimo kama vile mbolea na viuatilifu kwa kaya za kilimo. ~~Kaya za kilimo zinaulizwa taarifa kuhusu aina, wingi, manunuzi, gharama na vyanzo vya mbolea na viuatilifu vilivyotumika katika mwaka wa kilimo wa 2022/2023~~. Taarifa zitakazokusanywa ni pamoja na aina ya pembejeo, kiasi, gharama za vyanzo vya pembejeo zilizotumika katika mwaka wa kilimo wa 2022/23.

**~~Swali la 00: Geresho wa kuingiza~~**

~~CAPI/SUSO huzalisha misimbo kiotomatiki~~

~~**Swali la 00: Aina ya ingizo**~~

~~***Imepangwa katika CAPI: Orodhesha mbolea na viuatilifu vyote vilivyotumika katika mwaka wa kilimo wa 2022/23 uliopita (tazama kifungu cha 4 na kifungu cha 6).***~~

**Swali la 1:** ~~**Je, ni kiasi gani cha [AINA YA PEMBEJEO] ambayo shamba lako lilitumia katika mwaka wa kilimo uliopita wa 2022/23?**~~ **Je,ni kiasi gani cha [AINA YA PEMBEJEO] ambacho kaya/shamba yako/lako ilikitumia katika mwaka wa kilimo 2022/23, yaani kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?**

Swali hili litaulizwa kwa kaya zote~~za shamba~~zilizotumia mbolea ~~(hai na isokaboni)~~ za asili na za viwandani na ~~kemikaliza~~ madawa ya kilimo katika mwaka wa kilimo ~~uliopita~~ wa 2022/2023.

Kwa kila ya pembejeo~~[AINA YA PEMBEJEO] inayotumika~~ iliyotumika muulize mhojiwa ~~kuhesabu~~ataje kiasi alichotumia ~~**(Usiripoti kiasi kilichopunguzwa)**~~katika mwaka wa ~~marejeleo~~ wa kilimo 2022/23, ~~rekodi~~ jaza ~~wingi~~kiasi na ~~msimbo~~geresho la kipimo ~~kinachofaa~~husika.

***Kumbuka: Kwa dawa ambazo huchanganywa na maji ili kutumika kiasi ambacho kinahitajika hapa ni kile ambacho hakijachanganywa na maji (dawa halisi).***

**Swali la 2:** ~~**Ulipataje [AINA YA PEMBEJEO] ambazo zilitumika katika mwaka wa kilimo wa 2022/23 uliopita?**~~**Je, ulipataje [AINA YA PEMBEJEO] ambayo ilitumika katika mwaka wa kilimo wa 2022/23?**

Kwa kila aina ya pembejeo~~[INPUT TYPE]inayotumika~~iliyotumika, muulize mhojiwa aliipata kutoka wapi, ~~chagua zote zinazotumika~~ jibu zaidi ya moja linakubalika.

**Swali la 3:** ~~**Je, [AINA YA PEMBEJEO] uliyonunua katika mwaka wa kilimo wa 2022/2023 uliopita zote zilipewa ruzuku, zilizopewa ruzuku kwa kiasi au zisizo ruzuku?**~~**Je,[AINA YA PEMBEJEO] ulizonunua katika mwaka wa kilimo wa 2022/23 zilikuwa na ruzuku zote,kwa sehemu,au hazikuwa na ruzuku kabisa?**

~~*Iwapo Swali la 2. Lina Yoyote (4,5,6) && @rowcode.InList(8,21),* muulize mhojiwa kama alinunua [AINA YA PEMBEJEO] kwa bei ya ruzuku, iliyopewa ruzuku kwa sehemu au isiyosimamiwa na jua katika mwaka wa marejeleo. , na kanuni inavyofaa.~~Swali hili litaulizwa ikiwa ~~Kama~~jibu la Swali la 2 ni geresho 4 “ununuzi kutoka kwa wafanyabiashara/wachuuzi”, 5 “ununuzi kutoka taasisi za Serikali” au 6 “ununuzi kutoka chama cha wakulima”.Muulize mhojiwa kama pembejeo alizonunuazote zilikuwa za ruzuku, zilikuwa za ruzuku kwa sehemu tu, au hazikuwa za ruzuku kabisa katika mwaka wa 2022/23.

**Swali la 4a:** ~~**Kwa jumla, ni kiasi gani cha [AINA YA PEMBEJEO] ambacho hakina ruzuku ambacho shamba lako limenunua kwa mwaka wa kilimo wa 2022/23 uliopita?**~~**Je, kwa Ujumla, ulinunua kiasi gani cha [AINA YA PEMBEJEO] ambayo haikuwa na ruzuku katika mwaka wa kilimo wa 2022/23?**

~~*Ikiwa Swali la 3. Katika orodha (2,3,98) || (Swali la 2.Lina yyote kati ya (4,5,6) && @rowcode.InList (1,7)),* muulize mhojiwa kiasi cha [AINA YA PEMBEJEO] ambacho hakikupewa ruzuku ambacho walinunua katika mwaka wa marejeleo, rekodi kiasi~~. Iwapo Swali la 3, geresho ni 2 "kwa sehemu iliyo nunuliwa ilikua na ruzuku", 3"hakuna iliyonunuliwa iliyokuwa na ruzuku", 98 "Sijui", muulize mhojiwa kiasi cha pembejeoisiyokuwa na ruzuku ambayo alinunua katika mwaka wa kilimo 2022/23na uweke geresho la kipimo husika.

**Swali la 4b: ~~Kwa jumla, ni kiasi gani cha ruzuku ya [AINA YA PEMBEJEO] shamba lako limenunua kwa mwaka wa kilimo wa 2022/23 uliopita?~~** Je, **kwa ujumla, kaya yako/shamba lako ilinunua/lilinunua kiasi gani cha [AINA YA PEMBEJEO] ambayo ilikuwa na ruzuku katika mwaka wa kilimo wa 2022/23?**

~~*Ikiwa Swali la 3. Kwenye orodha (1,2),* muulize mhojiwa kiasi cha ruzuku [AINA YA PEMBEJEO] alichonunua katika mwaka wa marejeleo, rekodi kiasi hicho.~~ Iwapo Swali la 3 geresho ni 1 "yote ilionunuliwa ilikua na ruzuku",2 "kwa sehemu iliyo nunuliwa ilikua na ruzuku", muulize mhojiwa kiasi cha pembejeo husika alionunua ambayo ilikua na ruzuku kwa mwaka wa kilimo 2022/23, andika kiasi na uweke geresho la kipimo husika.

**Swali la 5: ~~Mdadisi: uliza kama mhojiwa anapendelea kutoa jumla ya thamani ya [AINA YA PEMBEJEO] iliyonunuliwa au bei ya uniti.~~Mdadisi: muulize mhojiwa kama angependelea kutaja jumla ya thamani ya [AINA YA PEMBEJEO] aliyonunua au thamani kwa kipimo.**

~~*Haya ni maagizo kwa mdadisi.* Mweleze mhojiwa kuwa ungependa kukadiria jumla ya thamani ya [AINA YA PEMBEJEO] pembejeo iliyonunuliwa katika mwaka wa marejeleo wa kilimo, na uwaulize kama wanapendelea kutoa maelezo kuhusu jumla ya thamani au bei ya jumla ya [AINA YA PEMBEJEO] iliyonunuliwa. Chagua chaguo sahihi.~~

Mdadisi anatakiwa amuulize muhojiwa kama angependelea kutaja jumla ya thamani ya pembejeo au bei kwa kipimo kwa mwaka wa kilimo wa 2022/2023.

**Swali la 6a: ~~Je, jumla ya thamani isiyo ya ruzuku ya [AINA YA PEMBEJEO] uliyonunua kwa mwaka wa kilimo wa 2022/23 uliopita ilikuwa kiasi gani?~~ Je, kwa ujumla thamani ya [AINA YA PEMBEJEO] ulizonunua bila ruzuku kwa mwaka wa kilimo wa 2022/23 ilikuwa kiasi gani?**

~~Iwapo itajibiwa (Swali la 4a) && Qn 5=1, muulize mhojiwa kuhesabu jumla ya thamani ya [AINA YA PEMBEJEO] isiyopewa ruzuku ambayo kaya ilinunua katika mwaka wa kilimo wa ulinzi na rekodi.~~Iwapo Swali la 5, geresho ni 1 "Jumla ya thamani", muulize mhojiwa thamani ya pembejeo husika ambayo alinunua bila ya ruzuku katika mwaka wa kilimo 2022/23.

**Swali la 6b: Je, jumla ya thamani ya ruzuku ya [AINA YA PEMBEJEO] uliyonunua kwa mwaka wa kilimo wa 2022/23 uliopita ilikuwa kiasi gani?Je, kwa ujumla thamani ya [AINA YA PEMBEJEO] ulizonunua kwa ruzuku kwa mwaka wa kilimo wa 2022/23 ilikuwa kiasi gani?**

Iwapo itajibiwa (Qn 4b) && Qn 5=1, muulize mhojiwa kuhesabu jumla ya thamani ya ruzuku ya [AINA YA PEMBEJEO] ambayo kaya ilinunua katika mwaka wa kilimo wa ulinzi na rekodi. Iwapo Swali la 5, geresho ni 1 "Jumla ya thamani", muulize mhojiwa thamani ya pembejeo husika ambayo alinunua kwa ruzuku katika mwaka wa kilimo 2022/23.

**Swali la 7a: Je, wastani wa bei ya kitengo kisicho na ruzuku ya [AINA YA PEMBEJEO] uliyonunua kwa mwaka wa kilimo wa 2022/23 uliopita ulikuwa kiasi gani? Je, kwa wastani bei ya [AINA YA PEMBEJEO] ulizonunua bila ruzuku kwa kipimo kwa mwaka wa kilimo wa 2022/23 ilikuwa kiasi gani?**

Iwapo itajibiwa (Swali la 4a) &&Swali la 5=2, muulize mhojiwa kwa wastani wa bei ya kitengo cha [AINA YA PEMBEJEO] isiyopewa ruzuku ambayo kaya ilinunua katika mwaka wa kilimo wa ulinzi na rekodi.Iwapo Swali la 5, geresho ni 2 "Bei kwa kipimo", muulize mhojiwa bei kwa kipimocha pembejeo husika ambayo alinunua bila ya ruzuku katika mwaka wa kilimo 2022/23.

**Swali la 7b: Je, wastani wa bei ya ruzuku ya [AINA YA PEMBEJEO] uliyonunua kwa mwaka wa kilimo wa 2022/23 uliopita ulikuwa kiasi gani? Je,kwa wastani bei ya [AINA YA PEMBEJEO]ulizonunua kwa ruzuku kwa kipimo kwa mwaka wa kilimo wa 2022/23 ilikuwa kiasi gani?**

Iwapo itajibiwa (Swali la 4b) &&Swali la 5=2, muulize mhojiwa wastani wa bei ya ruzuku ya [AINA YA PEMBEJEO] ambayo kaya ilinunua katika mwaka wa kilimo wa ulinzi na rekodi.Iwapo Swali la 5, geresho ni 2 "Bei kwa kipimo", muulize mhojiwa bei kwa kipimo ya pembejeo husika ambayo alinunua kwa ruzuku katika mwaka wa kilimo 2022/23.

### 3.3.13 Sehemu ya 12. Umiliki wa Mifugo iliyotunzwa na mabadiliko yake

**Maelezo:**

Sehemu hii inalenga kujua idadi na aina ya mifugo iliyotunzwa au iliyomilikiwa na kaya, kuongezeka (waliozaliwa, walionunuliwa, waliopokelewa kama zawadi) na kupungua (waliouzwa, waliokufa, waliochinjwa, waliotolewa na kaya mf. Kama mahari au mchango kwa jamii, ) kwa makundi ya mifugo katika mwaka wa kilimo wa 2022/23.. nashughulikia hisa za wanyama wanaofugwa na kaya ya shamba, bila kujali hali ya umiliki wa mifugo hiyo, katika kipindi cha marejeleo cha miezi 12. Data juu ya mabadiliko ya hisa katika

mwaka wa kumbukumbu pia inanaswa kwa mifugo yote. Moduli hii inasimamiwa kwa kaya zote za shamba zilizoripotiwa kufuga mifugo. Kaya hizi huchujwa kiotomatiki katika CAPI ikiwa ***Qn s1q07=1***. Inatarajiwa kwamba mwanakaya ambaye ana ufahamu kuhusu maelezo haya ya mifugo atajibu maswali, lakini wanaweza pia kusaidiwa na wanakaya wengine.

**Angalizo**

**Mifugo inayomilikiwa na kaya lakini inatunzwa na kaya nyingine itahesabiwa kwenye kaya inayoitunza na siyo kaya inayomiliki**.

**Swali la 1a: Kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023, je kaya/shamba ilifuga mifugo au kuku kati ya zifuatazo, bila kujali mmiliki ni nani?**

Katika mwaka wa kilimo 2022/23, je, kaya/shamba yako/lako ilikuwa na mifugo au mifugo jamii ya ndege wa aina zifuatazo? (BILA KUJALI MMILIKI NI NANI)

Maelezo: Swali hili linataka kujua aina ya mifugo au mifugo jamii ya ndege iliyotunzwa au iliyomilikiwa na kaya, katika mwaka wa kilimo wa 2022/23.

*Haya ni maagizo kwa* Mdadisi, adika aina ya mifugo iliyomilikiwa au kutunzwa katika kaya/shamba katika mwaka wa kilimo 2022/23. .mweleze mhojiwa kuwa unataka kuwauliza kuhusu aina za mifugo waliyofuga katika kipindi cha marejeleo. Mwaka wa kilimo 2022/23 Ili kuhakikisha kuwa taarifa zinazohitajika hazikosekani, chunguza ili kuhakikisha kuwa hawapotezi wanyama wowote ikiwa mwanzoni watajibu "Hapana". Kwa mfano, kaya inayomiliki kuku mmoja inaweza isichukulie kuwa ni mifugo. Ikiwa watajibu "Hapana", waulize kuhusu aina inayofuata ya mifugo. Kwa kila aina ya [JINA LA MIFUGO], mfugo muulize mhojiwa kama kaya ilitunza au kumiliki mifugo yoyote katika kipindi cha marejeleo mwaka wa kilimo 2022/23 na jaza aina ya mifugo aliyonayo. inavyostahili.

**Kumbuka ikiwa kaya au shamba ilimiliki au kutunza mifugo katika mwaka wa kilimo 2022/23 hata kama haipo kama ilivyokuwa tarehe 01, Oktoba, 2023, kaya /shamba itatakiwa kutaja aina ya mifugo iliyotunzwa/ iliyomilikiwa katika mwaka wa kilimo 2022/23. mdadisi kumhoji mhojiwa uwepo wa mifugo iliyokuwa kipindi cha mwaka wa kilimo 2022/23 kuchunguza na kurekodi ikiwa walimiliki au kuhifadhi [JINA LA MIFUGO] wakati wowote katika kipindi cha marejeleo (hata kama hawana sasa). Swali la 00: Jina la Geresho LS**

Imeratibiwa katika CAPI kwa aina zote za mifugo.

**Swali la 1b: Je, kaya/shamba hili ilikuwa na idadi [JINA LA MIFUGO] hadi tarehe 1 Oktoba 2023?**

Je, kaya hii/shamba hili ilikuwa na [JINA LA MIFUGO]  wangapi kama ilivyokuwa tarehe 1 Oktoba 2023 ?

Kwa kila ~~[JINA LA MIFUGO],~~ aina ya mfugo jaza idadi ya ~~wanyam~~a mifugo kama ilivyokuwa tarehe 01 Oktoba,2023 ~~wanaofugwa hadi wakati wa marejeleo~~ au jaza ~~rekodi~~ 0 kama kaya haikuwa na mifugo tarehe 01 Oktoba,2023~~. haimiliki/haimiliki [JINA LA MIFUGO] lakini ilifanya hivyo wakati fulani katika mwaka wa marejeleo. Kumbuka kwamba kwa baadhi ya makundi ya wanyama (mf: ng'ombe na kuku) idadi tofauti hurekodiwa na aina (VS asili imeboreshwa).~~

**Swali la 1c: ~~Je, kaya/shamba hili lilihifadhi ngapi [JINA LA MIFUGO] mwaka jana kwa muda sawa, hadi tarehe 1 Oktoba 2022?~~**

Je, kaya hii/shamba hili ilikuwa/lilikuwa na  [JINA LA MIFUGO], wangapi mwaka uliopita

wa kati wa kipindi kama hiki, kama ilivyokuwa tarehe 1 Oktoba 2022?

Swali hili linataka kujua idadi ya mifugo iliyomilikiwa na kutunzwa na kaya/shamba kama ilivyokuwa mwaka uliopita tarehe 01 Oktoba, 2022. Kwa kila aina ya mfugo jaza idadi ya mifugo iliyokuwepo tarehe 01 Oktoba, 2022 ~~[JINA LA MIFUGO], andika idadi ya wanyama waliofugwa tangu mwanzo wa kipindi cha marejeleo~~ au jaza ~~rekodi~~ 0 kama kaya haikuwa na mifugo tarehe 01 Oktoba, 2022. ~~rekodi 0 kama kaya haikuhifadhi/kumiliki [JINA LA MIFUGO]. Kumbuka kwamba kwa baadhi ya makundi ya wanyama (mf: ng'ombe na kuku) idadi tofauti hurekodiwa na aina (VS asili imeboreshwa).~~

**Swali la 1d: ~~Je, kaya yako inamiliki [JINA LA MIFUGO] yote inayohifadhi shambani kuanzia tarehe 1 Oktoba 2023~~?**

Je, kaya yako inamiliki  [JINA LA MIFUGO], wote iliowatunza kama ilivyokuwa tarehe 1

Oktoba 2023?

Swali hili linataka kujua kama kaya inamiliki mifugo iliyoitunza kama ilivyokuwa tarehe 01 Oktoba, 2023. Kwa kila aina ya mfugo ~~[JINA LA MIFUGO],~~ muulize mhojiwa kama kaya inamiliki mifugo yote iliyoitunza,  jaza geresho husika. ~~kama muda wa marejeleo na rekodi inavyofaa~~. *~~Swali la 1c & 1d zinatumika kwa umiliki wa sekta ndogo pekee (IF Holding_TYPE=2) na ikiwa idadi iliyoripotiwa ya wanyama katika s12q01b ni kubwa kuliko 0.~~*

**Swali la 2a: ~~Je, shamba lina mkataba wa uzalishaji na/au uuzaji wa [JINA LA MIFUGO] inayokuzwa?~~**

Je, shamba hili lina mkataba wa uzalishaji na/au uuzaji wa [JINA LA MIFUGO]%~~rostertitle%~~ wanaofugwa

**Angalizo**

**Mkataba ni makubaliano baina ya pande mbili au zaidi yanayofanyika kwa mdomo au maandishi yenye nguvu ya kisheria**

Swali la 2a litaulizwa kwa mashamba makubwa tu ~~kwa umiliki wa sekta kubwa pekee (IF Holding_TYPE=2).~~ Kwa kila aina ya mfugo ~~[JINA LA MIFUGO],~~ muulize mhojiwa kama shamba lina ~~kaya ina~~ mkataba wa uzalishaji/au uuzaji (hii inaweza kujumuisha mkataba wa kuuza wanyama hai au bidhaa za wanyama kwa duka, taasisi, soko, n.k) Jaza geresho husika~~na kanuni inavyofaa.~~

**Swali la 2b: ~~Je, mkataba unashughulikia 100% ya [JINA LA MIFUGO] inayokuzwa na shamba (mkataba wa kipekee)?~~** Je, mkataba huu unahusu asilimia 100 ya [JINA LA MIFUGO] wanaofugwa na shamba (mkataba wa kipekee)

~~Ikiwa~~ **Iwapo Swali la 2a geresho ni** 1, "Ndiyo" ~~kuhusu ufunikaji wa mkataba na msimbo inavyofaa.~~ Muulize mhojiwa kama mkataba wa uzalishaji au uuzaji ni asilimia 100. Mfano shamba linaweza kuingia makubaliano na kampuni/kiwanda kuwa uzalishaji wa mazao yote ya mifugo yatauziwa kwa hiyo kampuni au kiwanda

~~*Maagizo ya Wadadisi: Maswali yafuatayo yanalenga kukusanya taarifa za kina kuhusu mabadiliko ya idadi ya wanyama katika mwaka wa kumbukumbu, kurekodi maingizo yote (waliozaliwa, walionunua, zawadi zilizopokelewa n.k.) na kutoka (mauzo, vifo, hasara, kuchinja, michango n.k.). Habari inakusanywa kwa wanyama wote.* (Kuzaliwa + Kununuliwa + Zawadi/Kupokea) – (Mauzo+ Vifo + Hasara + Kuchinjwa + Kutolewa/Mchango).~~

**Swali la 3: ~~[JINA LA MIFUGO] wangapi walizaliwa katika mwaka wa kilimo kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?~~**

Je, ni [JINA LA MIFUGO] wangapi walizaliwa katika mwaka wa kilimo 2022/23?

Kwa kila aina ya mfugo ~~[JINA LA MIFUGO]~~ amba~~l~~o kaya iliripoti ~~kufuga~~ kutunza /kumiliki katika Swali la 1b, uliza na jaza ~~urekodi~~ idadi ya~~-~~ ~~wanyama~~ mifugo yote ~~wote waliozaliwa~~ iliyozaliwa katika mwaka wa kilimo 2022/23 ~~marejeleo~~, hata kama baadhi yao ~~wamekufa~~ walikufa ndani ya kipindi ~~wakati fulani~~ cha mwaka wa kilimo 2022/23 ~~marejeleo~~.

**Swali la 4: ~~Je, shamba hili lilinunua [JINA MIFUGO] ngapi likiwa hai kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?~~**

Je, kaya/shamba hii/hili ilinunua/lilinunua [JINA LA MIFUGO] wangapi hai katika mwaka

wa kilimo 2022/23?

Swali hili linataka kujua idadi ya mifugo iliyonunuliwa hai katika mwaka wa kilimo 2022/23. Kwa kila [JINA LA MIFUGO] ambalo kaya iliripoti kufuga/kumiliki katika Swali la 1b, uliza na jaza ~~urekodi~~ idadi ya~~-~~ ~~wanyama~~ mifugo yote ~~wote waliozaliwa~~ iliyonunuliwa hai katika mwaka wa kilimo 2022/23 ~~marejeleo~~, hata kama baadhi yao ~~wamekufa~~ walikufa ndani ya kipindi ~~wakati fulani~~ cha mwaka wa kilimo 2022/23 ~~marejeleo~~.

*. Ikiwa hakuna iliyonunuliwa, jaza 0 na uende swali namba 6.*

**Swali la 5: ~~Bei ya wastani ya [JINA LA MIFUGO] iliyonunuliwa kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023 ilikuwa kiasi gani?~~**

Je, bei ya kila [**JINA LA MIFUGO**] mmoja katika mwaka wa kilimo 2022/23 ilikuwa kiasi

gani?

Swali hili linataka kujua wastani wa bei ya kila mfugo ulionunuliwa katika mwaka wa kilimo 2022/23. Muulize mhojiwa wastani wa bei ya ~~[JINA LA MIFUGO]~~ kila mfugo ambao kaya ilinunua katika mwaka wa ~~marejeleo.~~kilimo 2022/23

**Swali la 6: ~~[JINA LA MIFUGO] ngapi zilipokelewa bila malipo au kama zawadi au mahari kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?~~**

Je, kaya/shamba ilipokea/lilipokea [**JINA LA MIFUGO**] wangapi bure au kama zawadi au ma

hari katika mwaka wa kilimo 2022/23?"

Swali hili linataka kujua idadi ya mifugo ambayo kaya/shamba ilipokea bure, kama zawadi au mahari katika mwaka wa kilimo 2022/23

Uliza na ~~uandike~~ jaza idadi ya mifugo [JINA LA MIFUGO] yote ambayo ~~yamepokelewa~~ imepokelewa na kaya kama zawadi, ~~za bure~~ (bila malipo) au mahari katika mwaka wa ~~marejeleo~~.kilimo 2022/23. Kama hakuna jaza 0 nenda swali linalofuata

**Swali la 7: ~~Je, shamba hili limeuza Wanyama wangapi [JINA LA MIFUGO] kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?~~**

Je, Kaya hii/Shamba hili imeuza/limeuza [JINA MIFUGO] wangapi hai katika mwaka wa kilimo 2022/23?"

Swali hili linataka kujua idadi ya mifugo hai ambayo kaya/shamba iliuza katika mwaka wa kilimo 2022/23

Uliza na ~~urekodi~~ jaza idadi ya mifugo hai[JINA MIFUGO] na kaya/shamba katika mwaka ~~marejeleo~~ wa kilimo 2022/23. Kama hakuna jaza 0 nenda swali la 9

**Swali la 8a: ~~Mdadisi, amuulize mhojiwa ikiwa anapendelea kutoa jumla ya thamani ya [JINA LA MIFUGO] iliyonunuliwa au bei ya kila moja.~~**

MDADISI: MUULIZE MHOJIWA KAMA ANAPENDELEA KUTOA THAMANI KWA UJUMLA YA [JINA LA MIFUGO] WALIOUZWA/ ILIYOUZWA AU BEI YA KILA MMOJA."

Mdadisi anatakiwa amuulize muhojiwa kama angependelea kutaja jumla ya thamani ya mifugo au bei kwa mfugo kwa mwaka wa kilimo wa 2022/2023. Jaza geresho husika ~~Chagua chaguo sahihi.~~

**Swali la 8b: ~~Jumla ya mapato kutoka kwa mauzo haya ya [JINA LA MIFUGO] kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023 yalikuwa yapi?~~** Je, mapato ya jumla yalikuwa kiasi gani kutokana na mauzo ya [JINA LA MIFUGO] katika mwaka wa kilimo 2022/23?

Iwapo ~~zaidi ya mfugo mmoja moja limeripotiwa limeuzwa katika~~ Swali la 7 jibu ni kubwa zaidi ya 0 (kuuzwa), andika jumla ya thamani ya ~~wanyama~~ mifugo ~~WOTE~~ yote iliyouzwa hai ~~walio hai waliouzwa (na si thamani ya mmoja tu)~~. Ikiwa kaya ilifanya biashara ya mifugo kwa ajili ya mazao au malipo mengine ~~ya asili~~ yasiyo ya fedha taslimu, thamani ya fedha ya malipo yasiyo ya fedha taslimu~~ ya asili~~ inapaswa ~~kuhesabiwa na~~ kuongezwa kama sehemu ya jumla ya kiasi kilichopokelewa kwa mauzo ya mifugo.

**Swali la 8c: ~~Bei ya wastani ya [JINA LA MIFUGO] iliyouzwa kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023 ilikuwa kiasi gani?~~** Je, wastani wa bei ya kuuza [JINA LA MIFUGO] mmoja kwa mwaka wa kilimo 2022/23 ilikuwa kiasi gani?

Swali hili linaulizwa ikiwa mhojiwa alichagua kutoa bei kwa mfugo ~~ya kitengo cha [LIVESTOCK NAME]~~ iliyonunuliwa katika mwaka wa kilimo 2022/23 ~~marejeleo, yaani, mradi tu chaguo la 2 (bei moja) lilichaguliwa katika Qn 8a~~. Muulize mhojiwa wastani wa bei kwa ~~[JINA LA MIFUGO]~~ mfugo ambayo kaya iliuza katika mwaka wa ~~marejeleo~~. kilimo 2022/23

**Swali la 9: ~~Ni wangapi [JINA LA MIFUGO] walikufa (magonjwa, matukio ya asili, n.k) kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?~~ Je, ni [JINA LA MIFUGO] wangapi walikufa (kutokana na magonjwa, matukio ya asili, n.k.) tangu Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?**

Mdadisi uliza idadi ya mifugo iliyokufa kutokana na magonjwa au majanga ya asili kwa mfano mafuriko, kimbunga, ukame n.k katika mwaka wa kilimo wa 2022/23. Ikiwa kuna mifugo yoyote iliyokufa jaza idadi kamili

**Swali la 10: ~~Je, ni [JINA LA MIFUGO] ngapi zilipotea (kuibiwa, kupotea n.k.) kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?~~ Je, ni [JINA LA MIFUGO] wangapi walipotea (kutokana na wizi, kutoonekana, n.k.) katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

~~Uliza kama wanyama wowote walipotea (kama waliibiwa, wamepotea, n.k.) katika mwaka wa marejeleo na urekodi nambari kwa kila [JINA LA MIFUGO].~~ Swali hili linataka kujua idadi ya mifugo iliyopotea kutokana na wizi, kutoonekana n.k katika mwaka wa kilimo wa 2022/23. Muulize mhojiwa idadi ya mifugo iliyopotea kutokana na wizi na kutoonekana n.k Ikiwa kuna mifugo iliyopotea jaza idadi kamili ya mifugo hiyo.

**Swali la 11: ~~Je, shamba hili limechinja [JINA MIFUGO] ngapi kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?~~ Je, shamba hili limechinja [JINA LA MIFUGO] wangapi katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

~~Uliza na urekodi idadi ya waliochinjwa shambani [JINA LA MIFUGO] na katika vichinjio katika mwaka wa marejeleo.~~ Swali hili linataka kujua idadi ya mifugo iliyochinjwa na kaya/shamba katika mwaka wa kilimo wa 2022/23. Muulize mhojiwa idadi ya mifugo iliyochinjwa na kaya/shamba Ikiwa kuna mifugo iliyochinjwa jaza idadi kamili ya mifugo hiyo.

**Angalizo: Mifugo iliyochinjwa inajumisha mifugo yote iliyochinjwa nyumbani au machinjioni.**

**Swali la 12: ~~Je, wastani wa [JINA LA MIFUGO] ulikuwa upi kabla ya kuchinjwa?~~ Je, kwa wastani [JINA MIFUGO] walikuwa na uzito gani kabla hawajachinjwa?**

~~Uzalishaji wa nyama unaweza kukadiriwa kutokana na jumla ya uzito wa mzoga wa wanyama wanaochinjwa shambani pamoja na wanyama wanaochinjwa kwenye kichinjio kwa niaba ya kumiliki. Uliza na uandike namba na uzito wa mzoga wa wanyama kabla ya kuchinjwa, pamoja na kitengo kilichotajwa na mhojiwa.~~

Swali hili linataka kujua kwa wastani mfugo/mifugo ulikua na uzito wa kiasi gani kabla ya kuchinjwa. Muulize mhojiwa kwa makini ili kuweza kupata makisio sahihi ya wastani wa uzito wa mfugo/mifugo. Jaza geresho sahihi la kipimo

**Swali la 13: ~~Takriban, ni kiasi gani cha nyama ya [JINA LA MIFUGO] ililiwa na shamba kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?~~ Kwa makadirio, ni asilimia ngapi ya nyama ya [JINA LA MIFUGO] ilitumiwa na kaya hii/shamba hili kwa mwaka wa kilimo 2022/23?**

I~~kiwa nambari ni chanya katika Swali la 11, mwombe mhojiwa akadirie asilimia ya [JINA LA MIFUGO] iliyochinjwa na kuliwa na kaya katika mwaka wa marejeleo.~~

Swali hili linataka kujua ni asilimia ngapi ya nyama ya mifugo iliyotumiwa na kaya kwa mwaka wa kilimo wa 2022/23.Muulize mhojiwa akadirie asilimia ya nyama ya mfugo iliyotumika na kaya. Mfano kaya ilichinja ngombe mmoja na kupata nyama kilo

200., kati ya hizo kilo 10 zilitumika na kaya na kilo 190 ziliuzwa, kwa hiyo asilimia ya nyama iliyotumika na kaya ni asilimia 5 (10/200*100=5%)

**Swali la 14: ~~Je, shamba liliuza [JINA LA MIFUGO] iliyochinjwa au nyama yake kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?~~ - Je, kaya hii/shambahili iliuza/liliuza [JINA LA MIFUGO] walio wachinja au nyama yao katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

~~Ikiwa nambari ni chanya katika Swali la 11, uliza kama baadhi ya [JINA LA MIFUGO] waliochinjwa au nyama yao iliuzwa katika mwaka wa marejeleo.~~ Swali hili linataka kujua kama kaya/shamba iliuza mfugo uliyochinjwa au nyama ya mfugo uliyochinjwa kwa kipindi cha mwaka wa kilimo wa 2022/23. Swali hili litaulizwa iwapo idadi ya mifugo iliyochinjwa katika swali la 11ni moja au zaidi. Jaza geresho husika

**Swali la 15: ~~Takriban, ni sehemu gani ya [JINA LA MIFUGO] iliyochinjwa iliuzwa na shamba kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?~~ Je, kwa makadirio, ni asilimia ngapi ya [JINA LA MIFUGO] waliochinjwa au nyama waliuzwa /iliuzwa na kaya hii/shamba hili katika mwaka wa kilimo 2022/23?"**

Ikiwa jibu la swali la 14 ni ndio, Muulize mhojiwa na jaza asilimia ya mifugo ambayo kaya/ shamba ilichinja au nyama iliyouzwa kwa kipindi cha mwaka wa kilimo 2022/23. ~~iluweiano wa jumla ya [JINA LA MIFUGO] iliyochinjwa ambayo iliuzwa katika mwaka wa marejeleo.~~

**Swali la 15b: ~~Ni bei gani kwa kila kilo ya nyama iliyouzwa kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?~~ Je, wastani wa bei kwa kilo ya nyama ya [JINA LA MIFUGO] iliyouzwa katika mwaka wa kilimo moja tu 2022/23 ilikuwa Shilingi ngapi?"**

~~Iwapo [JINA LA MIFUGO] lolote limeripotiwa kuwa liliuzwa katika Swali la 15, uliza na urekodi jumla ya mapato kutokana na mauzo ya [JINA LA MIFUGO] iliyochinjwa (na si thamani ya [**JINA LA MIFUGO**]). Ikiwa kaya ilipokea mazao kama malipo au malipo mengine yoyote ya asili, thamani ya pesa taslimu ya malipo ya bidhaa inapaswa kuhesabiwa na kuongezwa kama sehemu ya jumla ya mapato kutokana na mauzo. Swali hili linataka kujua~~ Iwapo mfugo wowote uliuzwa katika mwaka wa kilimo wa 2022/23, uliza wastani wa bei kwa kilo ya nyama kwa aina ya mifugo iliyouzwa katika mwaka wa kilimo wa 2022/23. Iwapo kaya imepokea mazao kama malipo au malipo mengine yoyote ambayo si ya fedha taslim kadiria thamani kwa shilingi ya kitu alichopata.

**Swali la 16: ~~Ni [JINA LA MIFUGO] ngapi zilitolewa kwa mfano kama mahari kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?~~ Je, ni [JINA LA MIFUGO] wangapi walitolewa na kaya hii/shamba hili (kwa mfano kama mahari, mchango kwa jamii, n.k.) katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

~~Uliza kama wanyama wowote walipewa wakati wa mwaka wa marejeleo na uandike nambari ya kila [JINA LA MIFUGO].~~ Swali hili linataka kujua idadi ya mifugo

ambayo ilitolewa na kaya/shamba bila ya malipo kwa mfano mahari, mchango kwa jamii, msaada n.k. katika mwaka wa kilimo wa 2022/23.

Muulize mhojiwa idadi ya mifugo iliyotolewa na kaya/shamba bila malipo. Jaza idadi ya mifugo iliyotolewa, kama hakuna jaza 0

## SEHEMU YA 13: UZALISHAJI WA MIFUGO

Sehemu hii inashughulikia gharama za uzalishaji zinazolipwa na kaya/shamba kwenye maji, malisho, upandishaji, chanjo, na matibabu ya mifugo katika kipindi cha kumbukumbu mwaka wa kilimo 2022/23.

**Swali la 00: Jina la Msimbo LS**

**Swali la 00: AINA YA MIFUGO/KUKU JAMII YA NDEGE**

*Imeratibiwa katika CAPI kwa aina zote za mifugo:*

**Swali la 1a: Je, kaya/shamba hili limelipa kiasi gani cha maji kwa ajili ya [KIKUNDI CHA MIFUGO] katika msimu wa mvua mwaka wa kilimo 2022/23?**

Kwa kila [KIKUNDI CHA MIFUGO], uliza na urekodi ni kiasi gani kaya/shamba ililipa maji kwa matumizi ya mifugo katika msimu wa mvua wa mwaka wa kumbukumbu. *Ikiwa hakuna gharama iliyotumika, rekodi 0*.

**Swali la 1b: Je, kaya/shamba hili limelipa kiasi gani cha fedha kwa maji kwa ajili ya [KIKUNDI CHA MIFUGO] wakati wa kiangazi mwaka wa kilimo 2022/23?**

Kwa kila [KIKUNDI CHA MIFUGO], uliza na urekodi ni kiasi gani kaya/shamba kililipa maji kwa matumizi ya mifugo wakati wa kiangazi wa mwaka wa kumbukumbu. *Ikiwa hakuna gharama iliyotumika, rekodi 0.*

**Swali la 2a: Je, kaya/shamba hili limetumia kiasi gani cha fedha kununua malisho/mabaki ya mazao/malisho/bidhaa za viwandani/mizizi na jamii yake/virutubisho kwa ajili ya [KIKUNDI CHA MIFUGO] kwakati wa msimu wa mvua mwaka wa kilimo 2022/23?**

Kwa kila [KIKUNDI CHA MIFUGO], uliza na urekodi ni kiasi gani kaya/shamba kililipa kwa ajili ya malisho kwa matumizi ya mifugo katika msimu wa mvua wa mwaka wa kumbukumbu. *Ikiwa hakuna gharama iliyotumika d, rekodi* 0.

**Swali la 2b: Je, kaya/shamba hili limetumia kiasi gani cha fedha kununua chakula cha mifugo/mabaki ya mazao/malisho/bidhaa za viwandani/mizizi na jamii zake/virutubisho kwa ajili ya [KIKUNDI CHA MIFUGO] wakati wa msimu wa kiangazi mwaka wa kilimo 2022/23?**

Kwa kila [KIKUNDI CHA MIFUGO], uliza na uandike ni kiasi gani kaya/shamba ililipa kwa ajili ya malisho ya matumizi ya mifugo katika msimu wa kiangazi wa mwaka wa kumbukumbu. *Ikiwa hakuna gharama iliyotumika, rekodi 0.*

**Swali la 3: Je, shamba hili lilitumia jumla kiasi gani cha fedha kwa kupandishia [KIKUNDI CHA MIFUGO] mwaka wa kilimo 2022/23?**
Kwa kila [KIKUNDI CHA MIFUGO], uliza na urekodi ni kiasi gani kaya/shamba kililipa kwa huduma za upandishaji mifugo katika mwaka wa kumbukumbu. *Ikiwa hakuna gharama iliyotumika, rekodi 0.*

**Swali la 4: Je, shamba hili lilitumia kiasi gani cha fedha kwa ajili ya chanjo na udhibiti dhidi wa minyoo, na wadudu wanaoeneza magonjwa kwa [KIKUNDI CHA MIFUGO] mwaka wa kilimo 2022/23?**
Kwa kila [KIKUNDI CHA MIFUGO], uliza na urekodi ni kiasi gani cha fedha kaya/shamba kililipa **kwa ajili ya chanjo na udhibiti dhidi wa minyoo, na wadudu wanaoeneza magonjwa** ya mifugo katika mwaka wa kumbukumbu. *Ikiwa hakuna gharama iliyotumika, rekodi 0.*

**Swali la 5: Je, shamba hili lilitumia jumla ya kiasi gani cha fedha kwa matibabu ya magonjwa ya [KIKUNDI CHA MIFUGO] katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Kwa kila [KIKUNDI CHA MIFUGO], uliza na urekodi ni kiasi ganicha ferdha kaya/shamba kililipa kwa matibabu ya magonjwa ya mifugo katika mwaka wa kumbukumbu. *Ikiwa hakuna gharama iliyotumika, rekodi 0*.

## SEHEMU YA 14: UZALISHAJI WA MAZIWA

Sehemu hii inalenga kukusanya taarifa kuhusu uzalishaji na mauzo ya maziwa katika kipindi cha kumbukumbu. Sehemu hii inatumika tu kwa kaya za wakulima waliofuga ng'ombe na mbuzi wa maziwa katika Mwaka wa Kilimo husika. *[Uliza kama s12q01a.Imejazwa geresho lolote kati ya (1,2,3, 4))]*

**Swali la 00: Jina la Kikundi cha Code LS**

**Swali la 00: Jina la Mifugo**

**Swali la 1: Je, kaya/shamba ilizalisha/lilizalisha maziwa ya [JINA LA MIFUGO] katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Kwa kila mfugo, muulize mhojiwa kama yupo mfugo aliyekamuliwa katika mwaka wa Kilimo husika na ujaze geresho linalohusika.

**Swali la 2: Je, shamba hili lilitunza kumbukumbu ya kiasi cha maziwa yaliyozalishwa kutoka kwa [JINA LA MIFUGO] katika Mwaka wa Kilimo 2022/23?**
*Swali la 2 litaulizwa kwa wamiliki wa mashamba makubwa pekee (IF Holding_TYPE=2).*
Kama Swali la 1=1, muulize mhojiwa kama shamba lilihifadhi kumbukumbu kama taratibu zinavotakiwa.

**Swali la 3: Ni kiasi gani cha maziwa kilizalishwa kutoka kwa [JINA LA MIFUGO] katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

Kama Swali la 2=1, muulize mhojiwa akutajie kiasi cha maziwa yaliyozalishwa na [JINA LA MIFUGO] katika mwaka wa kilimo husika na jaza kiasi.

**Swali la 4a: Wakati wa msimu wa Mvua katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, ni [JINA LA MIFUGO] wangapi walikamuliwa maziwa?**

Ikiwa (Qn 1=1 && Holding_TYPE==1) au Qn 2=0, Muulize mhojiwa idadi ya mifugo iliyokamuliwa katika msimu wa mvua wa Mwaka wa Kilimo husika.

**Swali la 4b: Wakati wa msimu wa Kiangazi katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, ni [JINA LA MIFUGO] wangapi walikamuliwa maziwa?**

Ikiwa (Qn 1=1 && Holding_TYPE==1) au Qn 2=0, Muulize mhojiwa idadi ya mifugo iliyokamuliwa katika msimu wa kiangazi wa mwaka wa Kilimo husika.

**Swali la 5a: Katika msimu wa mvua wa mwaka wa kilimo 2022/23, kwa wastani [JINA LA MIFUGO] alikamuliwa maziwa kwa siku ngapi?**

Ikiwa Swali la 4a limejibiwa, muulize mhojiwa akutajie wastani wa idadi ya siku ambazo mfugo alikamuliwa katika msimu wa mvua.

**Swali la 5b: Katika msimu wa kiangazi wa mwaka wa kilimo 2022/23, kwa wastani [JINA LA MIFUGO] alikamuliwa maziwa kwa siku ngapi?**

Ikiwa Swali la 4b limeijibiwa, muulize mhojiwa akutajie wastani wa idadi ya siku ambazo mfugo ulikamuliwa katika msimu wa kiangazi.

**Swali la 6a: Je, wastani wa uzalishaji wa maziwa kwa [JINA LA MIFUGO] kwa siku katika msimu wa mvua ilikuwa ni kiasi gani?**

Ikiwa Swali la 5a limejibiwa, muulize mhojiwa wastani wa maziwa yaliyozalishwa kwa ng’ombe/mbuzi mmoja kwa siku katika msimu wa mvua.

**Swali la 6b: Je, wastani wa uzalishaji wa maziwa kwa [JINA LA MIFUGO] kwa siku katika msimu wa kiangazi ilikuwa ni kiasi gani?**

Ikiwa Qn 5b limejibiwa, muulize mhojiwa wastani wa maziwa yaliyozalishwa kwa ng’ombe/mbuzi mmoja kwa siku katika msimu wa kiangazi.

**Swali la 7: Katika mwaka wa kilimo 2022/23 ni asilimia ngapi au ni sehemu gani ya maziwa ya [JINA LA MIFUGO] yaliyozalishwa yalitumiwa na kaya hii?**

Kama Swali la 1 ni “Ndiyo”, muulize mhojiwa akadirie ni aslimia ngapi au ni sehemu gani ya maziwa yaliyozalishwa yalitumiwa na kaya katika mwaka wa Kilimo husika.

**Swali la 8: Katika mwaka wa kilimo 2022/23, je, kaya hii/shamba hili liliuza/iliuza maziwa ya [JINA LA MIFUGO]?**

Kama Swali la 1 ni “Ndiyo”, muulize mhojiwa kama kuna kiasi chochote cha maziwa kati ya kile kilichozalishwa katika mwaka wa kilimo husika kiliuzwa na shamba/kaya.

**Swali la 9a: Katika mwaka wa kilimo 2022/23, ni asilimia ngapi au sehemu gani ya maziwa ya [JINA LA MIFUGO] yaliyozalishwa yaliuzwa na kaya/shamba hii/hili?** Kama Swali la 8 ni “Ndiyo”, muulize mhojiwa akadirie ni asilimia ngapi au ni sehemu gani ya maziwa yaliyozalishwa katika mwaka wa kilimo husika yaliuzwa na kaya/shamba.

**Swali la 9b: MDADISI MUULIZE MHOJIWA KAMA ANGEPENDELEA KUTAJA JUMLA YA THAMANI AU BEI KWA KIPIMO.**
***Haya ni maelekezo kwa mdadisi***. Eleza kwa mhojiwa kuwa unataka kukadiria jumla ya thamani ya kiasi cha maziwa kilichokamuliwa kutoka kwa ng’ombe au mbuzi na kuuzwa katika mwaka wa kilimo husika, halafu muulize kama angependelea kutoa taarifa ya jumla ya thamani au bei kwa kipimo. Chagua geresho linalohusika.

**Swali la 9c: Je,** kaya/shamba hii/hili ilipata/lilipata jumla ya kiasi gani kwa kuuza maziwa ya **[JINA LA MIFUGO] Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23.**
Swali hili litaulizwa ikiwa mkojiwa katika swali 9b alijibu “1” (JUMLA YA THAMANI) yaani kutoa thamani ya maziwa yaliyouzwa katika mwaka wa kilimo husika. Muulize mhojiwa thamani ya jumla ya maziwa ambayo kaya/shamba iliuza/liliuza katika mwaka wa kumbukumbu.

**Swali la 9d: Je, nini wastani wa bei ya maziwa ya [JINA LA MIFUGO] kwa lita iliuza katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Swali hili litaulizwa ikiwa mhojiwa alichagua kutoa bei kwa kipimo cha maziwa yaliyouzwa katika mwaka wa kilimo husika, yaani, katika swali 9b alichagua geresho “2” (Bei kwa Kipimo). Muulize mhojiwa bei kwa kipimo cha maziwa ambayo kaya iliuza katika mwaka wa kilimo husika.

## SEHEMU YA 15. UZALISHAJI WA MAYAI

Sehemu hii inalenga kukusanya taarifa kuhusu uzalishaji na mauzo ya mayai katika mwaka wa Kilimo 2022/23. Sehemu hii itahusisha kaya zinazofuga kuku (kuku wa kienyeji na wakisasa) katika mwaka wa kilimo husika. *[Uliza kama s12q01a. Imejazwa geresho kati ya 6 au/na 7).*

**Swali la 00: Geresho la kundi**

**Swali la 00: Jina la Mfugo**

**Swali la 1a: Je, katika kaya hii/shamba hili kuna [JINA MIFUGO] yoyote alitaga mayai katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

Kwa kila (JINA MA MFUGO) mfugo muulize mhojiwa kama kuna mayai yoyote yaliyotagwa katika mwaka wa kilimo husika, kisha jaza geresho husika.

**Swali la 1b: Je, ni [JINA LA MIFUGO] wangapi walitaga mayai katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

Muombe mhojiwa akutajie idadi ya kuku waliotaga mayai katika mwaka wa kilimo husika. Ikiwa Swali la 1a=1, Mtake mhojiwa akutajie idadi ya kuku waliotaga mayai.

**Swali la 2: Je, kaya hii/shamba hili ilitunza/lilitunza kumbukumbu ya idadi ya mayai yaliyozalishwa katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

Swali la 2 *litaulizwa kwa wamiliki wa mashamba makubwa pekee* (IF Holding_TYPE=2). Kama Swali la 1a=1, muulize mhojiwa kama shamba lilihifadhi kumbukumbu ya uzalishaji wa mayai.

**Swali la 3: Je ni mayai mangapi [JINA LA MIFUGO] walitaga katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

Ikiwa Swali la 2=1 au kama swali linahusu kuku walioboreshwa, Muombe mhojiwa akupe jumla ya kiasi cha mayai yaliyotagwa na kuku katika mwaka wa kilimo husika, na kisha jaza thamani na kipimo kilichotajwa na Mhojiwa. Yaani idadi kwa yai moja moja au trei (mayai 30).

**Swali la 4: Katika mwaka wa kilimo 2022/23, kwa wastani [JINA LA MIFUGO] alitaga mitago mingapi?**

Swali hili linahusu kuku wa kienyeji (kuku walioboreshwa hawana muda wa kutaga), kama Qn 1a=1 kwa ngazi ya kaya/mkulima mdogo au Qn 2=0, muulize mhojiwa wastani wa idadi ya mitago ya kuku wa kienyeji waliotaga katika mwaka wa kilimo husika.

***Kumbuka***: Kwa wastani kuku wa kienyeji hutaga mitago 3 hadi 4 kwa mwaka na kwa kila mtago hutaga yai 1 hadi mayai 30 (wastani mayai 15 kwa kuku).

**Swali la 5: Katika mwaka wa kilimo 2022/23, je ni wastani wa mayai mangapi yalitagwa na [JINA LA MIFUGO] kwa mtago?**

Swli hili litaulizwa ikiwa swali la 4 limejibiwa. Mtake mhojiwa akuambie kwa wastani wa idadi ya mayai yaliyotagwa na kuku wa kienyeji kwa mtago mmoja, kisha jaza idadi na kipimo alichotaja mhojiwa (Idadi ya yai moja moja au kwa kreti).

**Swali la 6: Katika mwaka wa kilimo 2022/23, ni asilimia ngapi au ni sehemu gani ya mayai ya [JINA LA MIFUGO] yaliyotagwa yalitumiwa na kaya hii/shamba hili?**

Swali litaulizwai iwapo Swali la 1a=1, mtake mhojiwa akadirie asilimia ngapi au ni sehemu gani ya mayai yalitumiwa na kaya kama vile kula au kutoa kama zawadi katika mwaka wa kilimo husika.

**Swali la 7: Katika mwaka wa kilimo 2022/23, je kaya hii/shamba hili liliuza mayai ya [JINA LA MIFUGO]?**
Swali hili litaulizwa ikiwa Swali la 1a=1, Muulize mhojiwa kama kuna kiasi cha chochote cha mayai yaliyozalishwa katika mwaka wa kilimo husika yaliuzwa na shamba/kaya.

**Swali la 8a: Katika mwaka wa kilimo 2022/23, ni asilimia ngapi ya mayai ya [JINA LA MIFUGO] yaliuzwa na kaya hii/shamba hili?**
Swali hili litaulizwa ikiwa Swali la 7=1, mtake mhojiwa akadirie, ni asilimia ngapi ya mayai ya MFUGO yaliyozalishwa na kaya/shamba katika mwaka wa kilimo husika yaliuzwa.

**Swali la 8b: MDADISI: MUULIZE MHOJIWA IKIWA ATAPENDELEA KUTOA JUMLA YA THAMANI YA MAPATO AU BEI KWA KIPIMO (YAI MOJA AU KRETI).** ***Haya ni maelekezo kwa mdadisi***. Mweleze mhojiwa kuwa unataka kukadiria jumla ya thamani ya mayai yaliyouzwa katika mwaka wa kilimo husika. Je angependelea kutoa thamani ya jumla ya mayai yaliyouzwa au bei ya kila yai au bei kwa kreti.

**Swali la 8c: Kaya hii/shamba hili lilipata kiasi gani cha fedha kwa kuuza mayai ya [MIFUGO] katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Swali hili litaulizwa ikiwa mhojiwa alichagua kutoa JUMLA YA THAMANI ya mayai yaliyouzwa katika mwaka wa kilimo husika, Ikiwa kama mhojiwa alichagua geresho la kutoa JUMLA YA THAMANI ya mayai yaliyouzwa katika swali la 8b (8b=1).

**Swali la 8d: Je, wastani wa bei ya yai la [MFUGO] lililouzwa katika mwaka wa kilimo wa 2022/ 23 ilikuwa kiasi gani?**
Swali hili litaulizwa ikiwa mhojiwa alichagua kutoa bei ya wastani ya yai moja moja au bei ya wastani kwa kreti aliyouza mayai katika mwaka wa kilimo husika. Swali hili litaulizwa ikiwa swali la 8b alichagua geresho "2" kutaja bei ya yai moja au bei ya kreti aliyouza katika mwaka wa kilimo husika.

## SEHEMU YA 16: MAZAO MENGINE YA MIFUGO

Sehemu hii inalenga kukusanya taarifa za uzalishaji na mauzo ya mazao mengine ya mifugo (kama vile asali, ngozi, wanyamakazi na huduma za upandishaji mifugo) katika mwaka wa kilimo 2022/23.

**Swali la 1: Je, kaya hii/shamba hili lilizalisha aina yoyote ya bidha au kutoa huduma za mifugo zifuatazo katika mwaka wa kilimo 2022/23, yaani kuanzia Oktoba 2022 hadi Septemba 2023?**
Kwa kila bidhaa iliyoorodheshwa, muulize mhojiwa kama kaya/shamba ilizalisha/lilizalisha asali ya nyuki wakubwa/wadogo, ngozi za wanyama

wakubwa/wadogo, samadi au kutoa huduma ya wanyama kazi, kukodisha wanyama wa kupandishia katika mwaka wa kumbukumbu.

**Swali la 00: Geresho la Bidhaa**

**Swali la 00: Aina ya Bidhaa**

**Swali la 2a: Je, kaya hii/shamba hili lina mizinga mingapi ya nyuki ya asili?**
Swali hili litaulizwa ikiwa kaya/shamba ilizalisha/lilizalisha asali ya nyuki wakubwa/wadogo. Muombe mhojiwa akutajie idadi ya mizinga ya asili ya nyuki inayomilikiwa na kaya/shamba.

**Swali la 2b: Je, kaya hii/shamba hili lina mizinga mingapi ya nyuki kisasa?**
Swali hili litaulizwa ikiwa kaya/shamba ilizalisha asali ya nyuki wakubwa/wadogo. Muombe mhojiwa akutajie idadi ya mizinga ya nyuki kisasa inayoendeshwa na kaya/shamba.

**Swali la 3: Je, ni kiasi gani cha [AINA YA BIDHAA] kilizalishwa katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Muulize mhojiwa akutajie kiwango cha bidhaa iliyozalishwa katika mwaka wa kilimo husika, kisha jaza idadi.

**Swali la 4: Je, kaya hii/shamba hili liliuza [AINA YA BIDHAA] yoyote katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Muulize mhojiwa kama aliuza bidhaa yoyote iliyozalishwa katika mwaka wa kilimo iliuzwa na shamba/kaya.

**Swali la 5: Je, kaya hii/shamba iliuza/liliuza kiasi gani cha [AINA YA BIDHAA] katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Ikiwa Swali la 4 kaya/shamba iliuza [AINA YA BIDHAA], muulize mhojiwa akadirie asilimia ngapi au ni sehemu gani ya [BIDHAA AINA] yote aliyozalisha katika mwaka wa kilimo husika iliuzwa na kaya/shamba.

**Swali la 6a: MDADISI: MUULIZE MHOJIWA IKIWA ANGEPENDELEA KUTAJA JUMLA YA THAMANI AU BEI KWA KIPIMO**.
Ikiwa kaya/shamba ilizalisha asali ya nyuki wakubwa/wadogo, ngozi za wanyama wakubwa/wadogo, samadi, muulize mhojiwa kama anapendelea kuripoti jumla ya thamani ya mapato au bei ya kila bidhaa moja aliyouza katika mwaka wa kilimo husika.

**Swali la 6b: Je, kaya/shamba hili lilipata kiasi gani cha fedha kwa jumla kwa kuuza [AINA YA BIDHAA] katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

Ikiwa kaya/shamba ilitoa/lilitoa huduma ya wanyama kazi, kukodisha wanyama wa kupandishia, muulize mhojiwa akadirie jumla ya mapato kutokana na huduma hizi katika mwaka wa kilimo husika na kisha jaza jibu lake.

**Swali la 6c: Je, jumla ya thamani ya [AINA YA BIDHAA] zilizouzwa katika mwaka wa kilimo 2022/23 ilikuwa kiasi gani?**
Ikiwa Swali la 6a aliuza, muulize mhojiwa akadirie jumla ya thamani kutokana na mauzo ya bidhaa hizi katika mwaka wa kilimo husika.

**Swali la 6d: Je, wastani wa bei ya [BIDHAA] kwa [KIPIMO] iliuzwa kiasi gani katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Swali hili litaulizwa ikiwa Swali la 6a=2, (BIDHAA kwa kipimo) muulize mhojiwa akadirie bei BIDHAA iliyouzwa katika mwaka wa kilimo husika na kisha jaza jibu sahihi.

## SEHEMU YA 17: UKUZAJI WA VIUMBEMAJI

Sehemu hii inakusanya taarifa juu ya ukuzaji na mauzo ya viumbemaji katika mwaka wa kilimo 2022/23. Haihusishi viumbemaji vilivyovuliwa au kuvunwa kutoka katika vyanzo vya asili vya maji kama vile bahari, maziwa, mabwawa na mito, bali inahusisha viumbemaji ambavyo vinafugwa kwenye mabwawa, visimba n.k.

**Swali la 1a: Je, katika mwaka wa kilimo 2022/23, kaya hii/shamba hili ilijishughulisha/lilijushughulisha na ukuzaji wa viumbe maji vifuatavyo?**
Kwa kila aina ya kiumbemaji iliyoorodheshwa, muulize mhojiwa kama alijishughulisha na ufugaji wa AINA YA KIUMBE MAJI katika mwaka wa Kilimo husika, kisha jaza maresho yote yanayohusika.

**Swali la 00: Aina ya Kiumbe Maji**

**Swali la 1b: Je, ni kipi chanzo kikuu cha vifaranga cha [KIUMBEMAJI] vilivyozalishwa katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Ikiwa kaya/shamba limejihusisha na ukuzaji wa mwatiko, sato, trout, kamongo na kambare muulize mhojiwa vyanzo vikuu vya vifaranga vya samaki, kisha jaza weka geresho linalostahili.

**Swali la 2: Je, kwa ujumla ni kiasi gani cha [VIUMBEMAJI] kilivunwa katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Muombe mhojiwa akutajie kiasi kwa kilogramu za viumbemaji waliovunwa katika mwaka wa kumbukumbu.

**Swali la 3: Katika mwaka wa kilimo 2022/23, ni asilimia ngapi au sehemu gani ya [VIUMBEMAJI] iliyozalishwa ilitumiwa na kaya hii?**

Muulize mhojiwa akadirie ni asilimia ngapi au ni sehemu gani ya jumla ya kiasi kilichozalishwa katika mwaka wa kilimo husika kilitumiwa na kaya/shamba.

**Swali la 4: Katika mwaka wa kilimo 2022/23, je kaya/shamba iliuza/liliuza kiasi chochote cha [VIUMBEMAJI] waliovunwa?**
Muulize mhojiwa kama kuna viumbemaji waliovunwa katika mwaka wa kilimo husika wakauzwa na kaya/shamba.

**Swali la 5: Katika mwaka wa kilimo 2022/23, asilimia ngapi au sehemu gani ya [VIUMBEMAJI] iliozalishwa iliuzwa na kaya hii/shamba hili?**
Swali hili litaulizwa ikiwa Swali la 4 limejibiwa ndio kaya/shamba iliuza/liliuza JINA LA KIUMBEMAJI. Mtake mhojiwa akadirie ni asilimia ngapi au ni sehemu gani ya jumla ya viumbemaji waliozalishwa na kaya/shamba katika mwaka wa kilimo 2022/23 viliuzwa na kaya/shamba.

**Swali la 6a: Mdadisi: MUULIZE MHOJIWA IKIWA ANAPENDELEA KUTOA MAJIBU YAKE KWA JUMLA YA THAMANI YA MAPATO ALIYOINGIZA YA BAADA YA KUUZA JINA LA KIUMBEMAJI AU BEI KWA KIPIMO.**
Swali hili litauliwa ikiwa Swali la 4 limejibiwa ndio kaya/shamba iliuza/liliuza JINA LA KIUMBE MAJI, muulize mhojiwa kama anapendelea kutaja jumla ya thamani ya mapato au bei kwa kipimo.

**Swali la 6b: Je, ni jumla kiasi gani kilipatikana kutokana na mauzo ya [VIUMBEMAJI] yaliyofanywa na kaya/shamba katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Muombe mhojiwa akadirie jumla ya mapato yaliyotokana na mauzo ya viumbemaji yaliyofanyika katika mwaka wa kumbukumbu.

**Swali la 6c: Je, wastani bei kwa kilogram ya [VIUMBEMAJI] waliouzwa katika mwaka wa kilimo wa 2022/2023 ilikuwa kiasi gani?**
Swali hili litaulizwa ikiwa Swali la 6a ametaja bei kwa kipimo, muombe mhojiwa akutajie bei ya bidhaa iliyouzwa kwa kipimo katika mwaka wa kilimo husika.

## SEHEMU YA 18: NGUVUKAZI

Sehemu hii inakusanya taarifa zinahusu makundi mbalimbali ya nguvukazi katika sekta zote za kilimo na sekta zinazohusiana na kilimo. Sehemu hii inapaswa kujibiwa na mwanakaya anayefahamu zaidi shughuli za kilimo za kaya na wanakaya wengine wenye ufahamu kuhusu maelezo haya wanaweza kumsaidia mhojiwa mkuu.

**Swali la 00: Namba ya mwanakaya**
***Imeshaprogramiwa kwenye CAPI: Nakili kutoka kwenye orodha ya wanakaya wote walio na umri wa miaka 6 na kuendelea.***

**Swali la 1: Je, miezi mingapi [JINA] alifanya kazi shambani kwa katika mwaka wa kilimo wa 2022/23?**

CAPI itatoa orodha ya wanakaya waliojihusisha na shughuli za kilimo katika mwaka wa kilimo husika. Ikiwa kama alijibu "ndio" katika swali la 5 sehemu ya 2. Kwa kila mwanakaya, muulize mhojiwa ni miezi mingapi mwanakaya huyo alifanya kazi shambani katika mwaka wa kilimo wa kilimo husika.

**Swali la 2: Katika miezi hiyo kwa wastani, [JINA] alifanya kazi kwa siku ngapi kwa kila mwezi?**

Ikiwa mwanakaya alitaja idadi ya miezi aliyofanya kazi katika swali la kwanza, muombe akutajie wastani wa idadi ya siku alizofanya kazi kwa kila mwezi.

**Swali la 3: Katika siku hizo kwa wastani, [JINA] alifanya kazi shambani masaa mangapi kwa kila siku?**

Ikiwa mwanakaya alitaja idadi ya siku alizofanya kazi katika swali la pili, muombe akutajie wastani wa masaa aliyofanya kazi kwa kila siku.

**Swali la 4: Je, shughuli gani ya kilimo [JINA] alifanya kazi katika mwaka wa kilimo wa 2022/23?**

Muulize mhojiwa shughuli gani ya kilimo alifanya katika mwaka wa kilimo husika (shughuli zinazokusudiwa ni uzalishaji wa mazao, ufugaji wa mifugo na ukuzaji wa viumbemaji), jibu zaidi ya moja linakubalika.

**Swali la 5a: Je, miezi mingapi [JINA] alifanya kazi katika shuguli za mazao katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

Ikiwa mhojiwa alijibu "mazao" katika swali la 4 muulize mwanakaya ni miezi mingapi ambayo mwanakaya huyo alifanya kazi katika shughuli za mazao katika mwaka wa kilimo husika.

**Swali la 5b: Katika miezi hiyo kwa wastani, [JINA] alifanya kazi kwa siku ngapi katika shughuli za mazao kwa kila mwezi?**

Ikiwa mwanakaya alifanya shughuli za mazao katika swali la 5a, muombe akutajie wastani wa idadi ya siku alizofanya kazi kwa kila mwezi.

**Swali la 5c: Katika siku hizo kwa wastani, [JINA] alifanya shughuli ya mazao masaa mangapi kwa kila siku?**

Ikiwa mwanakaya alitaja idadi ya siku alizofanya kazi katika swali la 5b, muombe akutajie wastani wa masaa aliyofanya shughuli za mazao kwa kila siku.

**Swali la 5d: Je, [JINA] amefanya kazi katika shughuli za mifugo kwa miezi mingapi katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

Ikiwa mhojiwakama alijibu “mifugo” katika swali la 4 muulize mwanakaya ni miezi mingapi ambayo mwanakaya huyo alifanya kazi katika shughuli za mifugo katika mwaka wa kilimo husika.

**Swali la 5e: Katika miezi hiyo kwa wastani, [JINA] alifanya kazi kwa siku ngapi katika shughuli za mifugo kwa kila mwezi?**

Ikiwa mwanakaya alifanya shughuli za mifugo katika swali la 5d, muombe akutajie wastani wa idadi ya siku alizofanya kazi kwa kila mwezi.

**Swali la 5f: Katika siku hizo kwa wastani, [JINA] alifanya shughuli za mifugo masaa mangapi kwa kila siku?**

Ikiwa mwanakaya alitaja idadi ya siku alizofanya kazi katika swali la 5e, muombe akutajie wastani wa masaa aliyofanya shughuli za mifugo kwa kila siku.

**Swali la 5g: Je, miezi mingapi [JINA] alifanya kazi shuguli za ukuzaji wa viumbemaji kwa katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

Ikiwa mhojiwa kama alijibu “viumbemaji” katika swali la 4 muulize mwanakaya ni miezi mingapi ambayo mwanakaya huyo alifanya kazi katika shughuli za ukuzaji viumbemaji katika mwaka wa kilimo husika.

**Swali la 5h: Katika miezi hiyo kwa wastani, [JINA] alifanya kazi kwa siku ngapi katika shughuli za ukuzaji wa viumbemaji kwa kila mwezi?**

Ikiwa mwanakaya alifanya shughuli za ukuzaji viumbemaji katika swali la 5g, muombe akutajie wastani wa idadi ya siku alizofanya kazi kwa kila mwezi.

**Swali la 5i: Katika siku hizo kwa wastani, [JINA] alifanya shughuli ya ukuzaji wa viumbemaji masaa mangapi kwa kila siku?**

Ikiwa mwanakaya alitaja idadi ya siku alizofanya kazi katika swali la 5h, muombe akutajie wastani wa masaa aliyofanya shughuli za ukuzaji wa viumbemaji kwa kila siku.

**Swali la 6a: Katika mwaka wa kilimo wa 2022/23, kaya hii/shamba hili iliwatumia wafanyakazi wowote kati ya wafuatao?**

Kwa kila aina ya wafanyakazi iliyoorodheshwa, muulize mhojiwa kama kaya/shambani ilitumia wafanyakazi wasiolipwa, wafanyakazi wa kubadilishana au wafanyakazi wa kulipwa kwenye shughuli za kilimo.

**Swali la 00: Aina ya wafanyakazi**

**Swali la 00: Shughuli ya Kilimo (Mazao, Mifugo, Ukuzaji wa Viumbe Maji n.k.)**

**Swali la 6b: Je, kuna [AINA YA WAFANYAKAZI] waliofanya kazi katika za [AINA YA SHUGHULI] katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

Muulize mhojiwa kama kaya/shamba ilitumia wafanya kazi wasiolipwa, wafanyakazi wa kubadilishana au wafanyakazi wa kulipwa kwenye shuguli ya mazao, mifugo na ukuzaji wa viumbemaji katika mwaka kilimo husika

**Swali la 7: Je, ni [AINA YA WAFANYAKAZI] wangapi walifanya kazi katika za [AINA YA SHUGHULI] katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

Ikiwa mhojiwa alitumia "wafanyakazi kutoka nje ya kaya" katika swali la 6b muulize ni wafanyakazi wangapi walifanya kazi katika shughuli husika katika mwaka wa kumbukumbu.

**Swali la 8: Katika mwaka wa kilimo wa 2022/23, kwa wastani ni kwa miezi mingapi [AINA YA WAFANYAKAZI] walifanyakazi katika shughuli za [SHUGHULI]?**

Ikiwa mhojiwa alitumia "wafanya kazi kutoka nje ya kaya" katika swali la 6b muulize kwa wastani ni miezi mingapi walifanya kazi katika shughuli husika katika mwaka wa kilimo husika.

**Swali la 9: Katika miezi hiyo, ni wastani wa siku ngapi kwa mwezi [AINA YA WAFANYAKAZI] walifanya kazi katika shughuli za [SHUGHULI]?**

Ikiwa mhojiwa alitaja idadi ya miezi katika swali la 8 muulize ni wastani wa siku ngapi kwa mwezi walifanya kazi katika shughuli husika katika mwaka wa kilimo husika.

**Swali la 10: Je, katika siku hizo, kwa wastani ni masaa mangapi kwa siku [AINA YA WAFANYAKAZI] walifanya kazi katika shughuli za [SHUGHULI]?**

Ikiwa mhojiwa alitaja wastani wa siku katika swali la 9 muulize ni wastani wa masaa mangapi kwa siku walifanya kazi katika shughuli husika katika mwaka wa kilimo husika.

**Swali la 11: Je, uliwalipa [AINA YA WAFANYAKAZI] kwa kazi walizofanya katika shughuli za [SHUGHULI]?**

Ikiwa kaya/shamba ilitumia wafanyakazi wa kubadilishana/kulipwa katika swali la 6a muulize mhojiwa kama aliwalipa kwa fedha taslim au kwa bidhaa.

**Swali la 12: Katika mwaka wa kilimo wa 2022/23, ni jumla kiasi gani ulilipa kwa pesa taslimu [AINA YA WAFANYAKAZI] kwa kazi waliofanya katika shughuli za [SHUGHULI]?**

Ikiwa mhojiwa aliwalipa katika swali la 11, muulize mhojiwa ni kiasi gani cha fedha taslim aliwalipa wafanyakazi husika kwa aina ya shughuli husika katika mwaka wa kilimo husika.

**Swali la 13: Katika mwaka wa kilimo wa 2022/23, uliwalipa [AINA YA WAFANYAKAZI] jumla ya kiasi gani kwa kwa njia ya bidhaa au huduma badala ya fedha kwa kazi waliofanya katika shughuli za [SHUGHULI]?**

Ikiwa mhojiwa aliwalipa katika swali la 11, muulize mhojiwa akutajie thamani ya bidhaa au huduma aliowalipa wafanyakazi husika kwa aina ya shughuli husika katika mwaka wa kilimo husika.

MDADISI: SWALI LA 13 LINAPOJIBIWA, USIJUMULISHE MALIPO YA FEDHA TASLIM YALIYOLIPWA KWA [AINA YA WAFANYAKAZI] KWA AJILI YA SHUGHULI ZA [AINA YA SHUGHULI] KWENYE (SW 12). KADIRIA THAMANI YA BIDHAA AU HUDUMA ILIOLIPWA KATIKA FEDHA YA TANZANIA (TZS). JAZA 0 IKIWA HAKUNA MALIPO YA BIDHAA AU HUDUMA BADLA YA FEDHA YALIYOFANYIKA.

## SEHEMU YA 19: GHARAMA NYINGINE

Sehemu hii inakusanya taarifa za gharama za huduma nyingine ambazo kaya/shamba zilitumia katika shughuli zao za uzalishaji. Hizi ni pamoja na gharama zinazohusiana na mitambo, usafiri, kukodi au kukodisha ardhi ya shamba na majengo, ukarabati na matengenezo, huduma kama vile maji na nishati, kodi na bima na nyengine zilizotajwa katika sehemu hii. Sehemu hii pia inahusika na taarifa za upatikanaji wa mikopo rasmi na isiyo rasmi kwa ajili ya shughuli za kilimo.

**Swali la 1a: Katika mwaka wa kilimo wa 2022/23, kaya hii/shamba hili ilitumia/lilitumia au ilipokea/lilipokea vitu au huduma yoyote kati ya zifuatazo?**
Kwa kila vitu au huduma iliyorodheshwa, muulize mhojiwa kama kaya/shamba ilitumia/lilitumia chochote kati ya hizo katika mwaka wa kilimo 2022/23. Kisha chagua zote zinazohusika.

**Swali la 00: GERESHO LA KITU**

**Swali la 00: KITU / HUDUMA**

**Swali la 1b: Je, kaya/shamba ililipia/lililipia [KITU/HUDUMA] katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Muulize mhojiwa kama walilipia [KITU/HUDUMA] iliyochaguliwa katika swali la "**1a**" katika mwaka wa kilimo husika.

**Swali la 2: Kiasi gani cha fedha kwa ujumla kililipwa kwa ajili ya [KITU/HUDUMA]?**
Ikiwa Swali la 1b alijibu "ndio", muulize mhojiwa ni kiasi gani cha fedha kwa ujumla walilipa.

**Swali la 3: Je, malipo haya ni ya muda gani?**
Ikiwa Swali la 2 limejibiwa, mhojiwa uliza kipindi cha malipo kama ni ya mwaka, mwezi, siku au msimu wa kilimo. Yaani malipo haya yaliyofanyika katika swali la 3 ni muda gani,

Mfano kaya imelipa sh 40,000 TZS kwa kukodi mashine, muulize haya ni malipo yam waka, mwezi, siku au msimu msimu wa kilimo. Kisha utachagua geresho linalohusika kutoka orodha ya mageresho yafuatayo.

SINGLE-SELECT s19q03_unit

| | |
|---|---|
| 01 | ○ Mwaka |
| 02 | ○ Mwezi |
| 03 | ○ Siku |
| 04 | ○ Msimu wa kilimo |

**Swali la 4a: Je, katika mwaka wa kilimo wa 2022/23, kaya/shamba hii/hili ilipata/lilipata au ingeweza/lingeweza kupata mkopo rasmi au usio rasmi kama ingehitaji/lingehitaji kwa ajili ya kujikinga majanga?**

Muulize mhojiwa kama angalau mwanakaya mmoja wa kaya alipata au angeweza kupata mkopo rasmi au usio rasmi kama angehitaji kwa ajili ya kujikinga na majanga katika mwaka kilimo 2022/23.

**Swali la 4b: Ni nani katika kaya hii alikuwa na uwezo wa kupata au alipata mkopo rasmi au usio rasmi?**

Ikiwa Swali la 4a jibu ni "Ndio" muulize mhojiwa ni nani kati ya wanakaya wenye umri wa miaka 15 na zaidi waliopata au kupokea mkopo rasmi au usio rasmi.

**Swali la 5: Je, katika mwaka wa kilimo wa 2022/23, mwanakaya hii/shamba hili ilitumia au ilikuwa na uwezo wa kutumia bima kwa ajili ya kukabiliana?**

Muulize mhojiwa kama angalau mwanakaya mmoja wa kaya/shamba aliweza kupata au kautumia bima kwa ajili ya kujikinga namajanga katika mwaka wa kilimo husika na jaza geresho husika.

**Swali la 6a: Katika mwaka wa kilimo 2022/23, je kaya hii/shamba hili limechukua mkopo fedha taslimu au mkopo usio wa kifedha kwa ajili ya shughuli za kilimo/ ufugaji mifugo/ ukuzaji viumbemaji?**

Muulize mhojiwa kama angalau mwanakaya mmoja alichukua fedha taslimu au mkopo usio wa kifedha katika mwaka wa kilimo husika, kisha jaza geresho linalohusika.

**Swali la 6b: Je, nani katika kaya alichukua mkopo kwa madhumuni ya kilimo?**

Ikiwa Swali la 6a jibu ni "Ndio" muulize mhojiwa ni nani kati ya wanakaya wenye umri wa miaka 15 na zaidi alichukua mkopo kwa madhumuni ya kilimo na uchague wanakaya wote wanaohusika.

**Swali la 6c_taslimu: Je, kwa ujumla ni kiasi gani cha fedha kilipokelewa kama mkopo katika mwaka wa kilimo 2022/23?**

Ikiwa Swali la 6a jibu ni “Ndio” muulize mhojiwa jumla ya kiasi cha fedha taslimu kilichopokelewa kama mkopo kwa ajili ya **shughuli za kilimo/ ufugaji mifugo/ ukuzaji viumbemaji** katika mwaka wa kilimo husika.

**Swali la 6c_Malipo yasio ya fedha: Je, kwa ujumla ni vitu vya thamani gani au malipo yasio ya fedha taslim yalipokelewa kama mkopo katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Ikiwa Swali la 6a jibu ni “Ndio” muulize mhojiwa jumla ya thamani ya vitu au mikopo isiyo ya fedha taslimu iliyopokelewa kwa ajili ya **shughuli za kilimo/ ufugaji mifugo/ ukuzaji viumbemaji** katika mwaka wa kilimo husika. *MAAGIZO YA MDADISI: KAMA HAKUNA KIASI KILICHOPOKELEWA, ANDIKA 0. KADIRIA THAMANI KATIKA TZS*.

**Swali la 6d: Je, riba ya mkopo kwa mwaka ilikuwa kiasi gani?**
Ikiwa Swali la 6a jibu ni “Ndio” muulize mhojiwa kiwango cha riba kwa mwaka cha mkopo uliochukuliwa kwa ajili ya **shughuli za kilimo/ ufugaji mifugo/ ukuzaji viumbemaji**.
*MAAGIZO YA MDADISI: IKIWA KUNA MIKOPO KADHAA, ANDIKA KIWANGO CHA WASTANI.*

**Swali la 6d: Kiasi_Jumla ya kiasi kilichorejeshwa katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Ikiwa Swali la 6a jibu ni “Ndio” muulize mhojiwa ni jumla ya kiasi gani cha mkopo kilirejeshwa katika mwaka wa kilimo husika.

**Swali la 6e: Je, ni nani aliekuwa mtoaji mkopo mkuu?**
Ikiwa Swali la 6a jibu ni “Ndio” muulize mhojiwa chanzo kikuu cha mkopo, kisha jaza geresho linalohusika.

**Swali la 7: Ni sababu gani kuu tatu zilizokufanya utafute mkopo**
Ikiwa Swali la 6a jibu ni “Ndio” muombe mhojiwa akutajie sababu kuu tatu za zilizomfanya kutafuta mkopo, kisha jaza mageresho husika.

**Swali la 8: Je, ni sababu gani kuu ilipelekea kaya/shamba isichukue/lisichukue mkopo?**
Kama Swali la 6a jibu ni “Hapana”, muulize mhojiwa sababu kuu ambayo kaya/shamba haikuchukua/halikuchukua mkopo, kisha jaza geresho husika.

**Swali la 9a: Katika mwaka wa kilimo uliopita 2022/23, je kaya hii/shamba hili ililipa/lilipa mkopo wowote wa fedha au vitu kwa madhumuni ya shughuli za kilimo/ ufugaji mifugo/ ukuzaji viumbemaji.**
Ikiwa Swali la 6a jibu ni “Ndio” muulize mhojiwa kama kaya imelipa fedha taslimu au vitu uliochukuliwa kwa ajili ya **shughuli za kilimo/ ufugaji mifugo/ ukuzaji viumbemaji** katika mwaka wa kilimo 2022/23 na kisha jaza geresho husika.

**Swali la 9b_Taslimu: Kiasi gani cha fedha kwa ujumla kilichorejeshwa katika mwaka wa kilimo 2022/23?**
Iwapo swali la 9a jibu ni "ndio", muulize mhojiwa jumla ya kiasi cha fedha kilichorejeshwa.

**Swali la 9b_yasio fedha: Ni kiasi gani cha fedha kilicholipwa katika mwaka uliopita wa kilimo 2022/23?**
Iwapo swali la 9a jibu ni "ndio", muombe muhojiwa akadirie thamani ya vitu vilivyorejeshwa kama malipo ya mkopo kwa ajili ya kilimo ambacho vimelipwa.

MAAGIZO YA MDADISI: IKIWA NI BIDHAA, MWAMBIE MHOJIWA AKADIRIE THAMANI YA FEDHA

**SEHEMU YA 20: USAJILI WA SHAMBA**
Sehemu hii inalenga kukusanya takwimu za usajili rasmi wa mashamba makubwa.

**Swali la 1: Je shamba hili limesajiliwa kwenye rejista rasmi? (Kama vile rejista za kampuni za kilimo, rejista ya kodi, n.k.)**
Muulize mhojiwa kama shamba limesajiliwa katika rejista rasmi na weka geresho la ndiyo kama limesajiliwa na Hapana kama halijasajiliwa.

**Swali la 2A na 2B: Tafadhali ainisha aina ya usajili na andika nambari ya usajili**
Ikiwa **Swali la 1**=1, muulize mhojiwa aina ya rejista ambayo shamba limesajiliwa katika swali 2A. Kama shamba limesajiliwa kwa jina la biashara weka geresho "1" na weka geresho "2" kama usajili wa shamba ni wa kampuni wenye hisa, kisha muulize na jaza nambari ya usajili katika swali 2B. Orodha ya mageresho ya aina za rejista zitatolewa katika CAPI.

### 3.4 Mwisho wa Mahojiano

*Maelekezo kwa Mdadisi:* Mwisho wa mahojiano, chukua dakika chache na kamilisha sehemu ifuatayo:
**Swali la 1. Hali ya Mhojiano: jaza geresho linalohusika.**

**Swali la 2. *(Kama Swali la 1=2), Sababu ya kutokukamilisha mahojiano***: Jaza geresho linalohusika

**Swali la 3. Muda wa kumalizika kwa mahojiano**: Jaza tarehe, saa, dakika zilizotumika hadi kukamilisha mahojiano.

**Swali la 4. Mahali yalipofanyika Mahojiano:** Andika mahali palipofanyikia mahojiano kwa kuchagua geresho linalohusika.

**Swali la 5. Kuchukua Majira nukta ya mahali palipo fanyiwa mahojiani kwa kutumia GPS: Soma majira nukta ya mahali ulipofanyia mahojiano kwa kutumia GPS.**

## 3.5 Baada ya Mahojiano

Unapohitimisha mahojiano, mshukuru mhojiwa kwa kutenga muda wake na kukubali kuhojiwa, na pia mshukuru kwa taarifa alizokupatia. Muulize kama ana maswali yoyote anayotaka kuuliza au anahitaji ufafanuzi zaidi kuhusiana na mahojiano yaliyofanyika na mpe majibu kwa maswali ambayo utaweza kuyajibu kama huwezi kuyajibu mjulishe kwa upole. Kumbuka kwamba muda wako katika mahojiano ni kidogo. Epuka majadiliano marefu.

# 4 Mwongozo wa kutumia CAPI/SUSO na Kifaa cha GPS na Mfumo wa CAPI kwenye Kishikwambi

## 4.1 Matumizi ya Mfumo wa CAPI katika Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2023 (AASS 2023).

CAPI ni kifupisho cha ***C****omputer* ***A****ssisted* ***P****ersonal* ***I****nterviewing*. Ni njia ya kufanya mahojiano na mtu binafsi inayojumuisha usaidizi wa kompyuta au kifaa cha elektroniki kama vile kishikwambi au simu. Mara nyingi, mdadisi atakuwa akimsomea maswali mhojiwa kutoka kwenye dodoso la kielektroniki, na kurekodi majibu kwenye dodoso la kielektroniki. CAPI imekuwa njia inayotumika zaidi katika kufanya mahojiano, kwa vile ina faida nyingi ikilinganishwa na matumizi ya karatasi [PAPI], mathalan, kuongezeka kwa ubora wa takwimu, takwimu kufika kwa wakati, vipengele vya ziada (kunasa taarifa mbali mbali, GPS, muda), kupungua kwa gharama za utafiti n.k. Utafiti wa kilimo wa mwaka 2023 (AASS 2023) mfumo ujulikanao kama Survey Solutions CAPI utatumika katika kusimamia zoezi zima la utafiti. Survey Solutions (SuSo) ni programu ya CAPI iliyotengenezwa na Benki ya Dunia na inatolewa bila malipo ili kutoa ufumbuzi wa kupunguza gharama na kutoa njia uendelevu za kufanya tafiti mbalimbali.

## 4.2 Utunzaji wa Jumla wa Kishikwambi na vifaa vingine

Katika mfumo wa CAPI, kishikwambi ndicho kifaa kikuu ambacho mdadisi hutumia uwandani. Kishikwambi kinatolewa kwa kila mdadisi kwa madhumuni ya kufanya mahojiano tu. Matumizi mengine yoyote ya vishikwambi (kuangalia ujumbe wa meseji, facebook, burudani za mtandaoni, nk) **hayaruhusiwi** kabisa. Mdadisi anatarajiwa kutunza kishikwambi na vifaa vingine ailivyopewa (chaja, USB cable, cover la Kishikwambi ). Uharibifu wowote au upotevu wa vifaa lazima utolewe taarifa kwa msimamizi mara moja. Vishikwambi na vifaa vingine lazima virejeshwe Ofisi ya Taifa ya Takwimu mara tu baada ya zoezi la ukusanyaji wa taarifa kukamilika. Ikiwa mdadisi atakumbana na matatizo ya kishikwambi wakati wa kukusanya taarifa (kishikwambi kuzima ghafla bila kutarajia, kishikwambi kutotunza moto na kutakiwa kuchaji mara kwa mara, n.k) toa taarifa mara moja kwa msimamizi wako.

## 4.3 Kuanza: Washa Kishikwambi na ingia kwenye Programu ya Usaili wa Mdadisi

**Washa** kishikwambi kwa kubonyeza kitufe cha kuwashia, shikilia kitufe cha kuwashia hadi skrini iwake. Kwenye kishikwambi bonyeza kitufe kilichoandikwa "**Interviewer**", kinapaswa kuwa na alama ya bluu na nyeupe. Kama inavyoonekana kwenye kielelezo 1 hapo chini.




***Kielelezo 1***

Mara tu baada ya kufungua programu, ukurasa wa kuingia utaoneshwa kama inavyoonekana kwenye kielelezo 2 (a)




***Kielelezo 2***

Ingiza anwani ya seva *https://suso.nbs.go.tz~~:9700~~/* katika sehemu ya kuingilia (Synchronization point ), andika jina ulilotumia kujisajili na neno la siri (nywila). Unaweza

kuangalia neno siri ulililoliandika kwa kutumia alama ya jicho iliopo kwenye kona ya kiboksi. Wakati wa kuandika anwani ya seva, kuwa makini kuandika "https". Kila mdadisi atatumia utambulisho utakaotolewa na NBS, ili ufuatiliaji uwe rahisi.

Mdadisi atakapokuwa anaingia kwenye mfumo huu kwa mara ya kwanza. lazima awe na huduma ya intaneti. Lakini, unapoingia kwa mara ya pili, nenosiri pekee ndilo litakalohitajika kwa sababu programu itakumbuka jina la mtumiaji na mdadisi hataweza kulibadilisha baadaye. Ni vyema kutambua kwamba huduma ya intaneti haihitajiki katika hatua hii.

Mara tu baada ya kufanikiwa kuingia, mdadisi atatakiwa kubadilisha nenosiri (kielelezo 2(b) hapo juu). **Muhimu**: Madadisi anapaswa kukumbuka utambulisho wake wa kuingia kwenye mfumo. Utambulisho haupaswi kuandikwa kwenye kifaa. Baada ya kuingia, bofya kwenye kitufe cha uoanishaji (synchronization button) ambacho kimeonyeshwa kwenye kisanduku cha rangi ya blue (kielelezo 2c).

Uoanishaji (synchronization) taarifa hutoa maelekezo kwa wadadisi kupata maelekezo juu ya masuala mbalimbali kuhusu utafiti (mfano, madodoso ya kujaza), kutuma mahojiano yaliyokamilika kwa Wasimamizi na kupokea tena mahojiano ambayo hayajakamilika na/ au yaliyokataliwa kutoka kwa Msimamizi. Uoanishaji huhitaji huduma ya intaneti (mfano, WiFi au 3G/4G).

Kama uoanishaji taarifa ~~umevurugika~~ haukukamilika kwa sababu yoyote~~a makosa~~, unapaswa kurudiwa hadi utakapofanikiwa. Wadadisi wanaweza kuwasiliana na Wasimamizi kama watapata matatizo ya uoanishaji. Wasimamizi na Wadadisi wanapaswa kuwa na uelewa wa jumbe za matatizo ya kawaida na namna ya kuzitatua. Mara nyingi, tatizo linakuwa ni upatikanaji wa huduma ya intaneti. Katika hali hiyo, wadadisi lazima wahakikishe kuwa kifaa chao kimeunganishwa na intaneti. Mathalan:

Kama kasoro ya 'hakuna huduma' au **"No network"** itaonekana, mdadisi analazimika kuhakikisha kuwa kishikwambi kimeunganishwa na intaneti kabla ya kukioanisha tena. Wakati wa uonishaji taarifa h~~H~~akikisha kuwa kishikwambi chako hakipo katika mfumo wa *airplane mode.* (Kitufe hiki kipo sehemu ya mpangilio wa Menyu chini ya "wireless and Networks").

- Kama uoanishaji ulivurugika na ukajitokeza ujumbe "Uoanishaji ~~ulivurugika~~haukukamilika -hakuna mawasiliano na Msimamizi" **"Synchronization was interrupted - no connection to the Survey Solutions Supervisor"0**, Mdadisi atalazimika kuchunguza kisanduku cha uoanishaji. Kuchunguza kisanduku hiki, atabonyeza kwenye vidoti vitatu ambavyo vimepangwa wima katika kona ya mkono wa kulia, na kubofya kwenye mpangilio

au “settings”. Halafu, atalazimika kuchunguza URL na kubofya kwenye eneo linalotakiwa kufanyiwa mabadiliko.

- Ikiwa ujumbe wa kasoro ya “Uoanishaji itaonesha muda uliisha” **(“Synchronization was interrupted-timeout”)** utajitokeza, Mdadisi atalazimika kubofya vidoti vitatu ambayo vimepangwa wima katika kona ya mkono wa kulia, na kubofya kwenye mpangilio au “settings”. Halafu atalazimika kuongeza muda wa seva wa kutafuta taarifa iliyoombwa au “Server Response timeout”.

## 4.4 Mtiririko wa ~~Vitendo~~ Kazi kwa Wadadisi

~~Kwa ufupi , m~~Mdadisi ~~anatarajiwa~~

1. W~~Kuw~~asha Kishikwambi
2. Anzisha Mfumo wa mahojiano
3. Ingia (na hu~~h~~isha kama kuna ulazima~~ikiwa inahitajika~~)
4. ~~Kuo~~Oanisha na Seva ili kupata kazi na kutuma kazi zilizokamilika~~(ikiwezekana)~~ kila ~~unapoanza~~ siku
5. Chagua dodoso unalohitaji kufanyia kazi. Hii inaweza kuwa: dodoso lililokataliwa/kurudishwa na msimamizi , dodoso uliloanza mahojiano, au dodoso jipya.
6. Nenda kwenye kaya kwa ajili ya mahojiano
7. Fanya mahojiano
8. Maliza kwa kuchagua neno ~~kuonesha kuwa~~ “Complete” ikimaanisha mahojiano yamekamilika
9. Oanisha kishikwambi kila mara fursa inapojitokeza, ili kumpatia Msimamizi mahojiano yaliyokamilika na kupokea maoni na maelekezo mengine kutoka kwa Msimamizi.

### Maelezo ya jumla juu ya Mfumo wa CAPI

Kielelezo mkono wa kulia kinaonesha picha ya jumla ya jinsi m~~M~~fumo wa CAPI unavyofanya kazi. ~~wa fumbuzi wa matatizo ya utafiti au Survey Solutions CAPI kielelezokinaonesha kuwa,~~ D~~d~~odoso la kielektroniki likishaandaliwa na kukamilishwa na wafanyakazi wa Makao Makuu, watalisambaza dodoso hilo kwa Wasimamizi. Wasimamizi watasambaza kazi kwa wadadisi, ambao ndio wahusika wakuu katika kufanya mahojiano. Vivyo hivyo, mahojiano yaliyokamilishwa



yatawasilishwa kwa wasimamizi kwa ukaguzi na yakikubalika yatatumwa Makao Makuu kwa ajili yauthibitisho wa mwisho.

### 4.5 Kuboresha Mfumo

Kwa wadadisi, uchunguzi wa Programu ya Interviwer App inasaidia kujua kama kuna kazi au toleo jipya la dodoso limetumwa na msimamizi. Hatua za kufanya hivyo zinajadiliwa hapa chini.

Kwanza, bofya vitufe vitatu kwenye sehemu ya juu ya kulia ya skrini na uchague ***Diagnostics***




***Kielelezo 3***

Baada ya kuchagua ***Diagnostics* link,** skrini inayofanana na iliyoonyeshwa hapa chini itajitokeza. Gusa chaguo la **"Angalia toleo jipya"** ili kubaini ikiwa kuna toleo jipya zaidi la dodoso la mdadasi tofauti na lile lililopo kwenye kishikwambi.




***Kielelezo 4***

Ikiwa programu ya Mdadisi itakua imeboreshwa, kidokezo cha angalia kwa toleo jipya kitasema hivyo.




***Kielelzo 5***

Kama kuna toleo jipya la *"Interviewer Application"*, bofya kwenye kitufe cha kuhuisha au *UPDATE* kuipakua na kuingiza kwenye kishikwambi:




***Kielezo 6.***

## 4.6 Muhtasari wa Dashboard ya Mdadisi

Sehemu hii inajumuisha taarifa kuhusu kutembea kati ya tabo (navigation tabs), hali za mahojiano, namna ya kutengeneza mahojiano mapya, namna ya kukamilisha mahojiano, na namna ya kurejea kwenye mahojiano. Dashibodi ya Mdadisi hutoa mhutasari wa jumla wa kazi zako ambazo umepewa na hatua zilipofikia. Tabo ambayo imeoneshwa juu ya dashibodi hutanzua mahojiano kwa kuzingatia kiwango cha ukamilifu wa mahojiano yenyewe.

**Kuvinjari kati ya tabo na tabo (Navigation between tabs)**

Kuvinjari kati ya tabo tofauti za kompyuta, mdadisi anaweza ama kubofya kwenye tabo iliyopo kwenye safu ya juu au kuitembeza kulia au kushoto. Kuwasaidia wadadisi kutofautisha kati ya tabo tofauti, rangi ya dashibodi itabadilika kulingana na tabo ambayo mdadisi yupo wakati huo. Mwingiliano *(Interface)* utaainishwa kwa rangi ya ~~kijivu~~ Zambarau kwa ajili ya 'Tengeneza Tabo Mpya' (*Create New Tab*), bluu kwa ajili ya 'Tabo iliyoanzishwa (*Started tab)*, kijani kwa ajili ya 'Tabo iliyokamilika' (*Complete tab)*, na nyekundu kwa ajili ya 'Tabo iliyokataliwa (*Rejected tab)*.

**Maelezo ya Kazi**

Dodoso~~Kadi~~ l~~y~~a kielektroniki la kila kazi litakuwa na namba juu. Namba hii italingana na namba ya kazi ambayo mtumiaji wa Makao Makuu na Msimamizi pia atatumia kuitambua kazi. Pembeni ya namba ya kazi, kutakua na idadi ya madodoso ambayo yatakua yamesalia kwa ajili ya kukamilishwa na mdadisi. Idadi hii itapungua kadri mdadisi atakavyokua anakamilisha mahojiano zaidi.

Zaidi ya hapo, kila ~~kadi~~ Dodoso litakuwa na taarifa ya utambulisho wa kila kazi au mahojiano. Utambulisho wa eneo ukionesha ~~Vigeu (variables) vitatu vya kwanza vya utambuzi,~~ Mkoa, Wilaya, na Kata/Shehia ut~~vi~~taoneshwa kwenye ~~kadi~~ dodoso kwa kila kazi au mahojiano. ~~Kuonesha taarifa nyingine za utambuzi, bofya mara moja kwenye kadi ya kazi.~~




***Kielelezo 7***

Picha 2 zinazofuata ni picha zenye maelezo ambayo yanatoa muhtasari wa **Dashboard** ya Mdadisi na Programu ya Mahojiano. Tafadhali kumbuka kuwa "~~kadi~~dodoso za kielektroniki"zinazooneshwa kwenye sampuli za skrini hizi si nakala halisi za ~~kadi~~ dodoso tutakalotumia hivyo kunaweza kuwa na ~~zinazotumiwa kwa CAS na~~ hutofauti~~ana~~ kidogo katika muonekano.



1. Interviewer login name
2. Synchronization button to exchange data with server, requires connection.
3. Menu button to logout, access settings, search for interviews, etc.
4. Pages with interviews: create new, started, rejected, completed, (with number of interviews in parentheses).
5. Cards correspond to interviews, show interview key, assignment number, name of the survey, date started, and identifying fields, and other info.
6. Click the dots to expand the card, show more identifying fields, OPEN button.
7. Click the OPEN button to return to the started interview.
8. Android tablet buttons (may vary by device and OS): Back, Home, Switch application
9. Banner color differs by page: gray for assignments, blue for started, green for completed, red for rejected.
10. Menu of actions to an interview, in this case Discard.
11. Number in parentheses (v1) denotes the version of the questionnaire if multiple were used.
12. The set of identifying fields may vary from survey to survey and is determined by the questionnaire author.
13. Swipe horizontally to switch between the pages of the dashboard.
16:59
4 interviews for SergiyRadyakin
Create New
Started (2)
Rejected (1)
Completed (1)
Interviews which have been started but not completed
You need to complete it to be synchronized
#95-00-40-57
Assignment 130427
Living Conditions Survey (v1)
Started on Sep 29, 16:58
Discard
Address:
Los Angeles CA 4312 Hollywood Blvd Apt. 22
Respondent:
Jennifer O'Donnell
#64-62-73-04
Assignment 130425
Living Conditions Survey (v1)
Started on Sep 29, 16:59
Address:
Washington DC 123 Main St Apt 329
Respondent:
John Smith
OPEN
You can interrupt any interview by switching from interviewing mode to the dashboard. Interrupted interviews can be resumed from the started page.
Synchronize often, whenever an opportunity arises. Do not accumulate the completed interviews on the tablet!
Charge your tablet fully before the start of the working day!
Save battery power by switching off Bluetooth, WiFi, and adjusting screen brightness!
Logging in with your credentials to a new device (re-linking) destroys the data on the old device!
Completed interviews can be edited only before the synchronization. At synchronization, the completed interviews are removed from your tablet! If you need to modify anything later, ask your supervisor to reject the interview back to you.


***Kielelezo 8***




***Kielelezo 9***

## Hali za mahojiano

Kuna hali nne zinazowezekana kwenye Dashboard:

i. **Tengeneza Mpya (Create New):** Tabo hii itaonesha kazi zote ambazo mdadisi anazo. Wadadisi wanaweza kutengeneza mahojiano mapya ya kazi zao. Kuanzisha mahojiano mapya, Wadadisi watabofya kwenye kitufe cha bluu cha Anza Kazi (***Start)*** Ikiwa mahojiano yote yanayohitajika kwa kazi yatakua tayari

yametengezwa, basi **Anza** itakuwa na rangi ya kijivu. Dashboard itakuwa ya ~~kijivu~~ Zambarau ukiwa kwenye tabo hii.




***Kielelezo 10***

ii. **Yameanza (Started):** Tabo hii inaorodhesha mahojiano ambayo yameanzishwa lakini bado hayajakamilishwa. Kufungua mahojano ambayo hayajakamilika, bofya tu mara moja kwenye ~~kadi~~ dodoso l~~y~~a mahojiano unayotaka ili kuona taarifa zote za awali ~~panua kadi hiyo~~ na baada ya hapo bofya kwenye kitufe cha **Fungua** (***Open)***. Dashibodi itakuwa bluu inapokuwa kwenye tabo hii.




***Kielelezo 11***

iii. **Limekamilika**: Tabo hii ina mahojiano ambayo Mdadisi ameyawekea alama kuwa yamekamilika. Mahojiano katika tabo ya **Imekamilika** yatatumwa kwenye seva wakati Mdadisi atakapooanisha (synchronize). Kufungua mahojiano ambayo yamekamilika, bofya mara moja tu kwenye kadi kwa mahojiano utakayochagua ~~ili kupanua kadi~~ na kisha bofya kitufe cha **Fungua (*Open*)**. Kumbuka d~~D~~ashibodi itakuwa ya kijani u~~i~~napokuwa katika tabo hii.



*Kielelezo 12*

iv. **Limekataliwa:** Tabo hii ina mahojiano yaliyokataliwa ambayo msimamizi amehakiki, akagundua kuwa yana mapungufu~~makosa~~, na kuyarudisha kwa mdadisi ili kuyasahihisha. Kufungua mahojiano yaliyokataliwa, gusa mara moja kwenye ~~kadi~~ dodoso ~~kwa mahojiano utakayo yachagua ili kupanua kadi~~ kisha uguse kitufe cha fungua. Ukiwa kwenye tabo hii,, dashibodi itakuwa na rangi ya nyekundu.




*Kielelezo 13*

**Jinsi ya kutengeneza mahojiano mapya**

**Hatua ya 1**

Kwenye tabo ya tengeneza upya, tafuta ~~kadi~~ dodoso l~~y~~a kazi utakayoichagua, na tumia taarifa za utambuzi kutafuta kazi inayostahili. Gusa kwenye kadi ili kuona taarifa zote za utambulisho. Hii pia itaonesha Anza. Gusa kitufe cha bluu kwa ajili ya kuanza kazi na anza mahojiano mapya.




*Kielelezo 14*

Ikiwa dodoso ni kubwa, skrini ya upakiaji inaweza kuonekana kabla ya ukurasa wa jalada la dodoso kuonekana kama inavyoonyeshwa kwenye mchoro hapa chini;




**Hatua ya 2**

Mdadisi ataona taarifa zote za utambulisho wa mahojiano hayo mapya. Iwapo taarifa za ~~kigeu chochote cha~~ za utambuzi haz~~k~~ikutolewa na makao makuu, mhojiwa anapaswa kujaza taarifa hizo kabla ya kuanza mahojiano. Baada ya kujaza taarifa zote muhimu za utambulisho, bofya kwenye tabo ya buluu **Anza** chini ya skrini.




***Kielelezo 15***

**Hatua ya 3**

Utaona mhutasari wa taarifa zote za utambuzi na viunganishi kwa maoni/maswali ambayo yaliachwa na Msimamizi na watumishi wa makao makuu. Pitia taarifa na hakikisha kila kitu kiko sahihi, na kisha bofya kwenye kitufe cha bluu cha ***Start*** chini ya skrini kuanza mahojiano. Kuangalia maoni, bonyeza kwenye kiunganishi cha swali chenye rangi nyekundu.




***Kielelezo 16***

**Jinsi ya kutoka kwenye mahojiano**

Bofya kwenye kitufe cha menyu (*menu)* sehemu ya juu kulia na chagua Dashibodi.




***Kielelezo 17***

Utaelekezwa namna ya kurudi nyuma kwenye dashibodi. Mahojiano ambayo hayajakamilika sasa yanaweza kupatikana chini ya kitufe cha ***Anza***, na unaweza kuchagua kazi nyingine yoyote.

**Namna ya kuanza tena mahojiano**

Nenda kwenye tabo ya Anza kwenye Dashibodi. Tafuta mahojiano ambayo ungetaka kuendeleza na bofya kwenye kadi yake kuonesha taarifa zote za utambuzi. Kisha, gusa kitufe cha buluu ili uendelee na mahojiano. Sehemu ya kwanza ya dodoso itafunguka kwenye ukurasa wa mdadisi. Hata hivyo, kazi zako zote za hapo awali zitakuwepo.

## 4.7 Uoanishaji (Synchronization)

Sehemu hii ina maelezo ya kutuma mahojiano yaliyokamilika na upokeaji wa mahojiano mapya. Kitufe cha uoanishaji ndiyo njia ya Mdadisi kuanzisha mabadilishano ya taarifa kati ya kishikwambi chake na kompyuta ya Msimamizi. Uoanishaji hufanya kazi mbili. Kwanza, husukuma kazi yoyote iliyokamilishwa kwenda kwa msimamizi kwa ukaguzi Zaidi.Pili, huvuta kazi zote mpya na zana za kukusanya taarifa kwenye kishikwambi cha mdadisi. Baada ya uoanishaji kukamilika, idadi ya kazi mpya zilizopokelewa, idadi ya mahojiano yaliyokamilishwa yaliyotumwa, na kadhalika zitaonekana vizuri.




*Kielelezo 18*

**Kwa nini taarifa zangu hazioanishwi?**

**Hitilafu**: Hakuna huduma ya mtandao. Kagua mpangilio wa mtandao *(network settings).*




*Kielelezo 19*

Ili kutatua:

- Angalia muunganisho wako wa Wifi au 3G/4G/LTE kupitia sehemu ya miunganisho ya mtandao ya menyu ya mipangilio kwenye kifaa chako.
- Hakikisha kuwa Wifi imewashwa. Hakikisha kuwa umeunganishwa kwenye mtandao.

**Kwa nini taarifa zangu hazioanishwi?**

**Hitilafu:** Hakuna mawasiliano na survey solution supervisor. Tafadhali hakikisha kuwa tovuti inapatikana.




***Kielelezo 20***

**Kutatua:**

- Kagua URL ya seva. Gusa kwenye kitufe cha menyu ya programu kwenye kona upande wa kulia. Bofya kwenye mpangilio na uangalie URL ya seva chini ya URL ya Msimamizi. Ukiona kuna tatizo, gusa sehemu ~~yoyote~~ husika ili kufanya mabadiliko.
- Ikiwa URL ya seva ni sahihi, tafadhali mjulishe Msimamizi/Makao Makuu kuhusu hitilafu hiyo.

**Kwa nini taarifa zangu hazioanishwi?**

**Hitilafu**: Muda umeisha wakati wa kuunganisha kwenye tovuti ya *Survey solution supervisor.* Angalia mtandao kama unapatikana.



*Kielelezo 21*

- **Ili kutatua:** Angalia mpangilio wa muda wa kuisha kwenye seva. Gusa kitufe kwenye menyu ya programu kwenye kona upande wa kulia. Bofya kwenye Mipangilio na uguse sehemu ya muda kuisha, *(Server Response timeout field)*. Katika dirisha litakalofunguka, unaweza kuongeza idadi ya sekunde zinazoruhusiwa.

## 4.8 Udhibiti wa ubora na kuweka alama za ukamilifu wa mahojiano

### Kukagua kama maswali yote yamejibiwa

Udhibiti ubora huanza na madadisi. Mdadisi anapaswa kufanya kila lililo ndani ya uwezo wake kuhakikisha kuwa maswali yote yanajibiwa. Programu ya mdadisi inatoa njia tatu za kufanya hivi.

*Njia ya kwanza* ni njia ya zamani ambayo mtu anaweza kutumia dodoso la karatasi. Mdadisi kwa urahisi hupekua na kupitia dodoso akitafuta maswali ambayo hayajajibiwa au majibu ambayo yameibua jumbe nyekundu za kasoro.

*Njia ya pili*, ambayo inahusu ukamilifu, ni kutumia paneli ya uongozaji (navigation panel) kama kipimo cha maswali yoyote ambayo bado yanahitaji kujibiwa. Kila kipengele katika paneli ya uongozaji kina geresho ya rangi. Kijani inaonesha kwamba sehemu imekamilika-kwamba maswali yote yamejibiwa na hakuna swali lenye jibu ambalo siyo halali. Bluu huashiria kutokamilika (kwamba, baadhi ya maswali hayajajibiwa). Nyekundu huashiria kwamba swali moja au zaidi lina jibu ambalo siyo sahihi.




*Kielelezo 22*

Njia ya tatu ni kuelekea kwenye moduli iliyopo kwenye kidirisha cha uongozaji chenye jina *imekamilika* (*Complete*). Unapoingia kwenye skrini hiyo, idadi ya maswali ambayo hayajajibiwa na yasiyo sahihi yataoneshwa. Mdadisi anaweza kutambua maswali ambayo hayajajibiwa kwa kufungua kidirisha cha uongozaji *(navigation panel)* kama

kilivyooneshwa na kwenda kwenye kasoro ambazo zinawekwa alama ya kibendera kwa kubofya kila moja kwenye skrini ya *Imekamilika*.




*Kielelezo 23*

**Kukagua kama majibu yote ni sahihi**

Mbali na kuthibitisha kuwa dodoso limejibiwa kikamilifu, mdadisi anatakiwa ahakikishe kuwa majibu yote yana maana. Kuna njia mbili za kufanya hivi. Wakati wa kujaza dodoso, mdadisi ataona ujumbe wa hitilafu wakati wowote ule ambao majibu yatakayotolewa yatakua si sahihi. Jibu batili linaweza kuwa lile ambalo liko nje ya majibu fulani yanayotarajiwa au linalokinzana na jibu lililotolewa mahali pengine. Kwa kadiri iwezekanavyo, Mdadisi anapaswa kusahihisha makosa yoyote mara tu yanapojitokeza.

Baada ya kumaliza kujaza dodoso, mdadisi anapaswa kukagua kujihakikishia kuwa hakuna makosa ambayo ameyasahau kuyarekebisha. Ili kufanya hivyo, mdadisi anaweza kufuata itifaki sawa na njia ya tatu hapo juu ili kuhakikisha kuwa maswali yote yamejibiwa.

**Kuthibitisha kukamilika kwa mahojiano**

Mahojiano hayatahesabika kuwa yamekamilika kwa kuwa tu maswali yote yamejibiwa. Ili dodoso lionekane kuwa limekamilika, ni lazima mdadisi atumie kidirisha cha uongozaji (navigation panel) kwenda kwenye sehemu inayoonesha Kamilisha. Mara tu akiwa kwenye skrini hiyo, mdadisi anatakiwa kubofya kitufe cha Imekamilika (Complete). Hii itaashiria dodoso kukamilika na litaonekana kwenye Dashbodi ya mdadisi.




***Kielelezo 24***

### 4.9 Kupitia sehemu mbalimbali za dodoso

Wadadisi wanapaswa kufuata kikamilifu itifaki ya utafiti wakati wa kujaza dodoso:

- Kufuatia mpangilio wa dodoso
- Kuuliza maswali yanayotangulia kabla ya maswali ya baadaye
- Kukamilisha sehemu zinazotangulia kabla ya sehemu za baadaye

Lakini wadadisi mara kwa mara wanaweza kuhitaji kuangalia sehemu zaidi ya moja ya dodoso (k.m. kukagua kazi zao, kuangalia kati ya safu mlalo za orodha ikiwa mhojiwa atasahihisha jibu la awali, kuwasilisha moduli huru kama mhojiwa mkuu wa moduli hiyo yupo).

Mdadisi anaweza kuangalia dodoso kwa njia kadhaa:

**Ndani ya sehemu**

Kuangalia juu na chini ndani ya kundi moja la maswali




*Kielelezo 25*

## Kati ya sehemu na sehemu

Mdadisi anaweza kuhama kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa kutumia kidirisha cha uongozaji (navigation panel) kinachopatikana kila mara, ikiwakilishwa na mistari mitatu ya mlalo ambayo, inapobonyezwa, hupanuka na kuwa jedwali shirikishi la yaliyomo kwenye dodoso.




*Kielelezo 26*

## 4.10 Maoni

Maoni yanaweza kuachwa kwa swali lolote. Hii itafaa kueleza majibu ambayo umethibitisha lakini yanaweza kuonekana kuwa ya ajabu "strange" au yasiyo sahihi kwa msimamizi wako.

Ili kuandika maoni, bonyeza kitufe kwa muda kwenye swali linalohusika. Baada ya sekunde chache, sehemu ya maoni ambayo unaweza kuandika maoni yoyote marefu kwa mpangilio wowote itaonekana.




*Kielelezo 27*

Maoni yanaweza pia kuachwa na Msimamizi wako kwa ajili yako. Maoni hayo mara nyingi yanaweza kuwa maswali kwa majibu ambayo umeandika.

Wakati mhutasari unaweza kujumuishwa kwenye maoni juu ya dodoso zima, maoni halisi kwa kila swali yataonekana pembeni mwa maswali yaliyotolewa maoni. Kutafuta maoni hayo, bofya tu kwenye kitufe chekundu cha swali kwenye ukurasa wa jalada wa hoja ya utafiti *(survey case cover page)* ambapo utaelekezwa kwenye swali na maoni.




*Kielelezo 28*

## 4.11 Kujibu aina zote za maswali

~~Zana~~ Programu ya Mdadisi “Interviewer Application” inaruhusu aina tofauti za maswali:

- Tarakimu
- Maandishi
- Chaguo moja bayana/ Chaguo nyingi bayana **(***single-select categorical/multi-select categorical)*
- Orodha
- Tarehe
- GPS

Kama Mdadisi, unapaswa kujua namna ya kujibu kila swali. Kila aina ya swali limefafanuliwa kwa ufupi hapa chini kwa kutumia vielelezo.

### Tarakimu

Maswali yanayochukua jibu la tarakimu yana sehemu ya jibu la tarakimu iliyo wazi. Sehemu hiyo inapoguswa, kitufe cha tarakimu huonekana ili anayehoji aweze kujaza jibu la kitarakimu linalofaa.




***Kielelzo 29***

### Maandishi

Maswali ya maandishi yana sehemu ya jibu la maandishi ya wazi. Sehemu hiyo inapoguswa, kitufe cha maandishi huonekana ili anayehoji aweze kujaza jibu la maandishi linalofaa.




*Kielezo 30*

**Bayana: Chaguo Moja**

Maswali bayana yenye chaguo moja (Single select categorical questions) yana majibu mbadala yenye vitufe vya radio. Kujibu swali la aina hii, Mdadisi hubofya kwenye kitufe cha radio ambacho kinahusiana na jibu llinalofaa zaidi.




*Kielelezo 31*

**Bayana: Chaguo nyingi (Multi Select)**

Maswali bayana yenye chaguo nyingi (Multi select categorical question) yana jibu zaidi ya moja kwa kuchagua kwenye “check boxes”. Kujibu swali la aina hii, mdadisi hubofya kwenye vidirisha vyote vinavyostahili. Majibu yaliyochaguliwa yataonesha alama ya vema kwenye kisanduku.




*Kielezo 32*

**Bayana: Chaguo Nyingi katika mpangilio wa Ndiyo/Hapana (Multi-Select in Yes/No Mode)**

Maswali bayana yenye chaguo nyingi yana vitufe viwili kwa ajili ya kila kipengele, kimoja ambacho kinaashiria "ndiyo" na kingine "hapana". Kujibu maswali ya aina hii, mdadisi hubofya kwenye kitufe kinachohusiana na jibu ambalo linalofaa kwa kila kipengele.




*Kielelezo 33*

**Bayana: Machaguo ya kujiachia**

Ikiwa maswali hayajajibiwa, machaguo haya huonekana sawa na maswali yanayohitaji majibu ya maandishi au tarakimu. Kila swali lina sehemu wazi ambapo jibu linaweza kuwekwa. Hata hivyo, ili kujibu maswali haya, mdadisi hugonga kwanza kwenye kidirisha na kisha kuchagua jibu bayana linalofaa zaidi kutoka kwenye menyu kunjuzi (drop-down menu). Kuchagua chaguo la jibu kunaweza kufanywa ama kwa kugonga chaguo moja kwa moja au kwa kuandika ili kupunguza chaguo za jibu na kisha uchague inayofaa zaidi.




***Kielelzo 34***

## Orodha

Bofya kwenye kisanduku cha maandishi tupu na utumie kibodi kuingiza jibu. Zaidi ya hayo, vipengele vya ziada vinaweza kuongezwa kwenye orodha hadi idadi ya mwisho ya vipengele inayokubalika itimie.




*Kielelezo 35*

Ili kufuta vipengele kutoka kwenye orodha, bofya alama ya X. Hata hivyo, chukua tahadhari: kufanya hivyo kunaweza kusababisha kufuta taarifa, ikiwa vipengele vya swali la orodha vimeunganishwa na orodha (kwa mfano, majina ya wanakaya, ambayo kila mmoja ana safu yake katika orodha ya idadi ya watu wa kaya).

## Tarehe

Gusa kisanduku cha maandishi cha *weka tarehe*.




*Kielelezo 36*

Kisha, tumia dirisha linaloonekana kuingiza tarehe sahihi. Kulingana na kipi kinafaa zaidi, anayehoji anaweza kusogeza vipengele vya tarehe juu na chini (yaani, kutumia kitufe cha mkono wa kushoto cha ingizo la tarehe katika kielelezo hapa chini) au kuchagua tarehe kutoka kwenye kalenda (yaani, kutumia kipengele cha mkono wa kulia na kuingiza tarehe).




*Kielezo 37*

Baada ya kubofya kitufe cha *Nimemaliza*, tarehe itarekodiwa. Jibu lililorekodiwa litaoneshwa chini ya maandishi ya swali, kama inavyoonekana hapo juu.




***Kielelezo 38***

**Tarehe: Muda wa sasa**

Bofya kwenye kisanduku cha bofya ili urekodi kisanduku cha muda wa sasa.




***Kielelezo 39***

Kisha, muda wa sasa kwenye kishikwambi utaandikwa kiotomatiki.

**GPS**

Kwanza, bofya kisanduku cha maandishi. Hii itafungua sehemu ya kukujulisha kwamba kishikwambi kiinatafuta mahali ilipo GPS. Kufunga dirisha la GPS kutazuia kishikwambi kutafuta GPS. Ni muhimu kuzingatia kuwa kishikwambi kinaweza kuhitaji kuwa nje, kukiwa na anga wazi (bila paa au miti juu) ili kupata haraka alama za GPS.




***Kielelezo 40***

Kisha, kishikwambi kitarekodi chenyewe majiranukta ya GPS. Mahali ilipo GPS pataonekana mara moja chini ya boksi la maswali ya maandishi, pakionesha longitudo, latitudo, usahihi, na mwinuko kutoka usawa wa bahari*(altitude).*




***Kielelezo 41***

Ikiwa vipimo vya GPS siyo sahihi vya kutosha, unaweza kubofya tena kwenye kiboksi cha *andika GPS*. Kwa kufanya hivyo, utabadilisha vipimo vya zamani vya GPS na vipimo vya vya vipya GPS kusoma. Unaweza kuendelea kwa mtindo huu hadi utakapopata vipimo vya GPS vyenye usahihi zaidi.

**Angalizo:** Kishikwambi hakihitaji huduma ya intaneti kupata ramani/mahali ilipo GPS.

## 4.12 Ushabihianaji/mwingiliano(interface) na majibu ya maswali




*Kielelezo 42*

**Kujibu maswali:** Jinsi ya kujua kama umejibu swali




**Kielelezo 43**

Kuna njia chache ambazo wadadisi wanaweza kubaini ikiwa swali limejibiwa kwa ufasaha. Kwanza, swali huonyesha jibu fulani. Pili, kishikwambi hutetema kidogo na maswali huzungukwa na boda nyekundu, kama jibu ambalo limeandikwa siyo sahihi. Kutetema kunaweza kuzimwa kwa kwenda kwenye mpangilio wa ~~zana~~ program ya Mdadisi

(Interviewer's *settings)* na kuondoa kisanduku cha kuingiza alama ya kukubali au kukataa*(checkbox)* pembeni mwa 'Tetema kama jibu lisilo sahihi litatolewa'.

.




***Kielelezo 44***

Hata hivyo, hata baada ya swali kujibiwa, mdadisi anaweza kusubiri kabla ya kuhamia swali linalofuata. Wakati anayehoji anahitaji kusitisha, programu ya mdadisi itaonesha ujumbe ufuatao:




***Kielelezo 45***

Mdadisi anaweza kuondoa jibu katika swali lolote kwa kubofya X pembeni ya jibu lake.




***Kielelezo 46***

**Jinsi ya kufahamu iwapo umefanya kosa**

Baada ya jibu kurekodiwa, "Interviewer Application" hutathmini kiotomatiki ikiwa jibu linaendana na majibu mengine katika dodoso ~~au linawezekana kulingana na kile kinachojulikana kuhusu idadi ya watu katika utafiti~~. Ikiwa jibu haliendani au haliwezekani, jibu hilo linachukuliwa kuwa batili. Maswali yenye majibu batili yameainishwa kwa rangi nyekundu na yanaambatana na ujumbe wa hitilafu ambao utaonekana kuelezea tatizo (kama inavyoonekana hapo juu).

**Kuvitambua vikundi na orodha ya vipengele mbalimbali**

Vikundi na orodha/rosta ni makundi maalum ya maswali. Kwenye kishikwambi, zote mbili zinaonekana kama kitufe.




*Kielelezo 47*

Kitufe kinapobonyezwa, wadadisi huona maswali au safu mlalo ya orodha inayohusishwa na kitufe hicho.




Kuondoka kwenye safu ya orodha hiyo, Mdadisi analazimika kuchagua kitufe kilicho na jina la kikundi cha orodha (roster group) au sehemu kwenye eneo la chini la skrini.

Kukamilisha kikundi au orodha, Mdadisi hutakiwa tu kujibu maswali yote yanayohitajika. Kwa kikundi, hii ni rahisi. Kwa orodha, mchakato unahitaji maelezo kidogo.

Mdadisi analazimika kumaliza orodha ya safu kwa safu. Kwa kugonga kitufe kinachohusishwa na safu mlalo yoyote, mdadisi ataona maswali yote ya kipengele hicho kwenye orodha. Ili kurudi kwenye mwonekano wa orodha, bofya kitufe kilicho chini ya skrini (k.m., Huduma za ugani).




***Kielelezo 48***

## 4.13 Nini cha kufanyika iwapo utapokea mahojiano yaliyokataliwa

Mahojiano yaliyokataliwa yataonekana katika ukurasa wa 4 wa Dashibodi: ‘Imekataliwa’. Mahojiano yaliyokataliwa lazima yakaguliwe ili kuona maoni ya Msimamizi wa taarifa. Mdadisi anaweza kujaribu tena kufanya mahojiano ili kupata majibu ambayo yalikosekana au kusahihisha taarifa kama inavyohitajika. Kutegemea na hali, hili linaweza kutatuliwa kwa njia ya simu au kupitia kupitia mzunguko mwingine kwenye kaya. Baada ya tatizo/matatizo kutatuliwa, mahojiano yanapaswa kuwekewa alama ya kukamilika na kishikwambi kuoanishwa tena.

Ikiwa mdadisi haelewi sababu za kukataliwa, anapaswa kuwasiliana na Msimamizi wa wake kwa maelezo zaidi. Kitaalam, mchakato huu unaweza kurudiwa mara nyingi iwezekanavyo; hata hivyo, wahojiwa wanaweza kupunguza ushirikiano wao na kuacha kutoa taarifa

## 4.14 Miiko ya Kuttumia Kishikwambi wakati wa ukusanyaji wa takwimu

- Usifute programu ya “Interviewer” inayopatikana kwenye kishikwambi chako. Hii itasababisha kufuta taarifa iliyokusanywa kwenye kishikwambi chako.
- Kuweka Nywila ya muundo wowote (pattern/pin) ni marufuku kabisa.
- Usisakinishe (install) na kutumia program zingine kama vile WhatsApp, Facebook na YouTube.
- Usitumie kishikwambi kwa madhumuni mengine zaidi ya kukusanya taarifa za utafiti.
- Usitumie kishikwambi na mtu mwingine.
- Epuka kukiacha kishikwambi kwenye jua kali, maji au joto kali.